Ufafanuzi Wa Agano Jipya

Wagalatia - Wakolosai

Na Dorothy Almond

mwisho na Askofu Francis Ntiruka

www.africanpastors.org

Ufafanuzi Wa
Agano Jipya

Wagalatia - Wakolosai

Dorothy Almond

© African Pastors Fellowship 2010

Kimetolewa na:
AFRICAN PASTORS FELLOWSHIP
Station House, Station Approach, Adisham
Canterbury, Kent CT3 3JE
United Kingdom

www.africanpastors.org

WARAKA KWA WAGALATIA

YALIYOMO

Utangulizi
Mwandishi
a) „WAGALATIA " walioandikiwa ni watu gani?
b) Tarehe ya kuandikwa kwa waraka huu.
c) Sababu ya kuandikwa kwa waraka huu.
d) Umuhimu wa waraka kwetu sisi.

Ufafanuzi

1: 1-5	Salaam za Paulo kwa Wagalatia
1: 6-9	Wagalatia kuigeukia "injili nyingine"
1: 10-24	Asili ya Injili ya Paulo
2: 1-10	Maelezo ya Safari ya Pili alipokwenda Yerusalemu
2: 11-14	Paulo aligongana na Petro huko Antiokia na kumkemea
2: 15-21	Kuhesabiwa haki kwa kumwamini Kristo
3: 1-5	Ujinga wa Wagalatia
3: 6-8	Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani
3: 9-14	Tofauti kati ya Imani na Matendo
3: 15-29	Mahali na Shabaha ya Torati katika Mpango wa Mungu
4: 1-11	Kuwa watumwa ndipo Kufanywa kuwa Wana
4: 12-20	Paulo aliwasihi kwa upendo
4: 21-31	Wana wawili wa Ibrahimu - Ishmaeli na Isaka
5: 1-6	Wagalatia wapaswa kumchagua Kristo au Sheria
5: 7-15	Uhuru wa kweli
5: 16-26	Kuenenda katika Roho
6: 1-5	Mausia kadha
6: 6-10	Kupanda na Kuvuna
6: 11-18	Paulo kufunga Waraka; Fahari yake katika Msalaba wa Kristo, akichukua chapa zake

U T A N G U L I Z I

MWANDISHI: Ni Mtume Paulo. Amejitaja wazi 1:1 Ameeleza jinsi alivyoitwa kuwa Mtume 1:12ku. Amewaita Wagalatia "ndugu", aliwafahamu, maana ni yeye aliyeihubiri Injili kwao kwa mara ya kwanza, nao waliiamini kutokana na mahubiri yake

(a) "WAGALATIA" walioandikiwa ni watu gani?

Wengi huamini kwamba ni Wakristo wa "Makanisa ya Galatia" yaliyopandwa katika Safari Kubwa ya Kwanza ya Kueneza Injili, (Mdo.13 na 14) iliyofanyika na Paulo na Barnaba kama BK.46-48. Katika Safari hiyo walifikia Miji ya Antiokia wa Pisidia, Ikonio, Listra na Derbe. Miji hiyo ilikuwamo katika Jimbo la Kirumi lililokuwa na nchi za Pisidia, Frigia, na Likaonia ndani yake, na nchi ya Galatia kaskazini yake.

Wataalamu kadha hawakubaliani na wazo hilo kwa sababu walikuwako "Wagalatia" walio "Wagalatia" hasa kwa asili yao na kwa lugha yao. Hao waliishi kaskazini ya hao wengine. Hatuna habari kuhusu Injili kuhubiriwa kati yao.

Katika Ufafanuzi huo tunafuata wazo la kuwa hao Wagalatia walioandikiwa ni waamini wa makanisa yaliyopandwa na Paulo na Barnaba katika Safari Kubwa ya Kwanza. Paulo aliwaita "Wagalatia" kama jina la kujumlisha pamoja watu wa Pisidia, Frigia, Likaonia n.k.

Barnaba ametajwa 2: 1,13. Barnaba hakwenda na Paulo katika Safari zingine zilizofuata baadaye.

(b) Tarehe ya kuandikwa kwa waraka huu:

Kweli tarehe itategemea kama Wagalatia walioandikiwa ni wale walioishi kusini katika Jimbo la Kirumi au ni wale walioishi kaskazini. Kwa kuwa katika ufafanuzi huu tunafuata ni wale wa Kusini, basi, tarehe yaweza kuwa mapema hata pengine kabla ya Baraza Kuu la Yerusalemu B.K.49, (Mdo.15).

Katika Waraka Paulo alitaja Safari mbili za kwenda Yerusalemu. 1:18 - miaka mitatu baada ya Kuokolewa Kwake Ling. na Mdo. 9:26-30. Halafu alitaja kwenda Yerusalemu tena baada ya miaka 14. Je! Mara hiyo ni ile ya Matendo 11:30 alipokwenda na Barnaba wakipeleka msaada wakati wa njaa? Si wataalamu wote wanaofikiri hivyo: baadhi hufikiri ni wakati mwingine.

Wengine hufikiri ni wakati alipotoka Antiokia kwenda Yerusalemu kwa Baraza Kuu BK.49. Yawezekana alikuwa Antiokia alipouandika Waraka. Hakutaja habari wala uamuzi wa Baraza la Yerusalemu, kwa hiyo, huenda ni kabla ya Baraza kufanyika. Uamuzi wa Baraza ungalimsaidia sana katika mashindano yake na Wagalatia.

Kama ni hivyo twaweza kuweka tarehe kuwa kama BK.48/49 hivyo Waraka huu ni katika zile za kwanza kuandikwa na Paulo.

(c) Sababu ya kuandikwa kwa waraka huu

Ni dhahiri sana Paulo alikuwa amepokea habari kutoka makanisa ya Galatia kwamba wakristo walikuwa wakishambuliwa sana kuhusu imani yao. Inaonekana hao washambulizi walitoka mahali pengine 1:6-7.

Hasa washambulizi hao waliwafundisha kwamba ni lazima watahiriwe na kushika Torati ya Kiyahudi wakitaka kuwa Wakristo kamili - Taz. Gal. 4:10; 5:2-4; 6:12-15.

Washambulizi hawa huitwa Mayahudishi au Mayahudishaji (Judaizers). Mafundisho hayo yalikuwa kinyume kabisa cha Paulo na Injili aliyoihubiri. Yeye Paulo alikaza kwamba mtu awaye yote huokolewa kwa neema tu, kwa njia ya kumwamini Kristo Aliyesulubiwa, bila kuongeza lo lote. Mwanzoni Wakristo wa Galatia waliamini hivyo, wakabatizwa, na kupewa Roho 3:5,27.

Paulo alipowafikia mara ya kwanza walimpokea kwa mikono miwili 4:13-15; na kwa muda waliendelea vizuri katika imani 5:7; ndipo mabadiliko yalitokea walipofika hao Mayahudishaji na kufundisha "injili nyingine" ambayo machoni pa Paulo ilioukanusha ukweli wa Injili. Yawezekana mtu mmoja alikuwa kiongozi wao ambaye Paulo hakutaja kwa jina. Pengine huyo mtu au watu kadha walitoka Yerusalemu, Mama Kanisa Gal. 2:12-13; Mdo.15: 1,2,5,24.

Tujualo ni kwamba Paulo aliuandika waraka huu hali akiwaka moto moyoni mwake. Alitumia maneno makali 1:6 ku. 3:1 ku. 4:11, kusudi awaamshe Wakristo ili watambue hatari kubwa iliyopo. Alihesabu hao washambulizi ni adui "wa ukweli wa Injili".

Walisema vibaya juu ya Paulo, walijaribu kutia mashaka kwa mamlaka yake kwa kusema ya kuwa yeye Paulo hakuwa Mtume halisi kama wale wengine, wala hakuchaguliwa kama wao. Katika kumshambulia Paulo walikuwa wakiishambulia Injili aliyoihubiri.

(d) Umuhimu wa waraka kwetu sisi

Umuhimu wa Waraka ni katika Ukweli wa Injili kuwekwa wazi kabisa. Ni Injili hii inayotuweka huru. Ni Injili hii inayotupa nguvu, Ni Injili hii inayoleta baraka za msamaha wa dhambi na kuhesabiwa haki kwa imani peke yake, kutokana na Kifo cha Kristo Msalabani.

Daima tu katika hatari ya kutaka "nyongeza" kwa imani. Hali ya Kifarisayo imo ndani yetu, twataka sana kuleta "msaada" au kufanya kitu pamoja na kuamini. Kuokolewa kwa neema tu kunaua kabisa kiburi chetu, ni vigumu kukubali kwamba "sina cha mkononi".

Waraka huu husimamisha usawa wa wanadamu wote katika neno la "wokovu", wote huokolewa kwa neema tu kwa kumwamini Kristo, haidhuru ni Wayahudi au WaMataifa, wanaume au wanawake, au wa tabaka gani.

Hata hivyo kila kundi waweza kuwa na desturi zake. Si lazima Wayahudi wawa kama Wamataifa, wala Wamataifa wawe kama Wayahudi. Wokovu walio nao wamepewa bure na Kristo, hakuna astahiliye au awezaye kujistahilisha kwa njia ya desturi fulani au kwa matendo mema. Hata hivyo Paulo alisisitiza haja ya matendo mema kwa wale ambao tayari wameamini, hao wapaswa kumruhusu Kristo atawale maisha yao, ila hawataokolewa kwa matendo yao – Ef. 2:8-10. **Njia** ya kuokolewa ni njia ya neema na imani; **shabaha** ya wokovu ni tutende matendo mema. Imani ni zizi la kuokolewa, matendo mema ni matunda yake.

Waraka huu umegusa sana watu na kuleta mabadiliko na baraka katika Kanisa. Mmojawapo aliyeguswa sana ni Martin Luther katika karne ya 15. na Matengenezo ya Kanisa yalitokea. Pia John Wesley aliguswa sana na ujumbe wa Waraka huu, maisha yake yalibarikiwa sana, na Uamsho ulifuata kuhubiri kwake na baadaye dhehebu ya WaMethodisti lilitokea.

UFAFANUZI

1: 1-5 <u>Salaam za Paulo kwa Wagalatia</u>

k.1. Mara moja Paulo alijitambulisha kwao na kujiita Mtume. Alisisitiza asili ya Utume wake. Alitumwa na Yesu Kristo na Mungu Baba. Katika kufanya hivi alijiweka sawa na Mitume wengine. Ni ukumbusho wa yale yaliyompata njiani alipokuwa akienda Dameski, alipokutana na Yesu aliye Hai. Utofauti wa Utume wake na ule wa akina Petro, si katika kuwekwa na Bwana Yesu, ila wao waliwekwa na Yesu aliyekuwa hai kabla ya Kufa Kwake. Yeye aliwekwa na Yesu aliye hai baada ya Kufa Kwake. Kwa kusudi alimtaja Mungu Baba pamoja na Bwana Yesu - Utume wake ulitoka kwa Mungu Baba kwa njia ya Yesu Kristo, kwa hiyo mamlaka aliyo nayo ni Mamlaka ya Mungu. Si kwamba aliupinga "Utume" wa wale Mitume kumi na wawili, la, ila alidai utume wake unalingana na kuwa sawa na utume wao.

Kwa kusema hayo mwanzoni mwa barua hiyo ni wazi Paulo ana neno linalomchoma moyoni, naye ataendelea na neno hilo mbeleni.

k.2. Alituma salaam za ndugu waliokuwa naye, yawezekana ni waamini wa Antiokia wa Shamu, ikiwa alikuwa pale alipouandika waraka huo, ila hatujui kwa uhakika alikuwa wapi. Hakuwa peke yake, alifanya kazi kwa kushirikiana na wengine, nao walijiunga naye katika Waraka huu, na kuunga mkono "Injili" yake. Ila alijibagua kwa kujiita "Mtume" na kuwaita walio naye "ndugu".

"kwa makanisa ya Galatia" yaani sharika zile zilizotokea baada ya yeye kuhubiri katika miji yao. Hatujui kama aliandika zaidi ya nakala moja, au kama wataishirikishana hiyo nakala moja, au pengine kila sharika litainakilisha.

k.3. Huwatakia zile baraka ambazo alizitaja kila alipowaandikia waamini katika makanisa yao. Hizo ni baraka za Injili zilizo muhimu kwa kila mwamini. "Neema" na "Amani" zatoka kwa Mungu Baba na Bwana Yesu. "Neema" ni asili ya wokovu, na matokeo ya "neema" ni amani, upatanisho na Mungu.

k.4. Neema imedhihirika kabisa katika Kujitoa Kwake Bwana Yesu alipokufa Msalabani na kuwa dhabihu ya dhambi, kusudi, atupatanishe kwa Mungu na kutuokoa na dunia hii mbovu. Kwa Kifo hicho tumewekwa huru, hatumo tena chini ya utawala wa dhambi, na Shetani, na dunia hiyo mbovu. Iwapo bado tungali duniani, hata hivyo, twaonja baraka za wakati ujao.

Hayo yalikuwa mapenzi ya Mungu Baba na ya Bwana Yesu, walikuwa na nia moja na shabaha moja, wako pamoja.

k.5. Utukufu wa Baba na Mwana umedhihirika wazi kabisa katika mpango huo wa wokovu kwa njia ya neema.

Neno "Mtume" lina maana ya kuwa Mjumbe maalum, mwenye cheo cha pekee, aliye na mamlaka ya yule aliye juu yake na kumtuma. Mitume 12 walichaguliwa na Yesu Mwenyewe, waliitwa na kutumwa naye, walipewa mamlaka ya kufundisha na kuhubiri na kuponya katika Jina Lake. Walikuwa kundi dogo. Neno “Mtume” si neno kwa wote, maneno mengine kama “waamini” “watakatifu” “ndugu” yahusu wakristo wote. Ila neno “mtume” lilitumika kwa Wale 12 na kwa wachache wengine tu.

Hakuna wengine waliourithi Utume wao baadaye. Mfuatano wa Ki-Mitume ni kuwarithi kwa njia ya kuwa waaminifu kwa mafundisho yao yaliyomo katika Agano Jipya. Haiwezekani wengine wawafuate, wao walikuwa wa "kipekee" waliowekwa na Yesu kuhifadhi kweli zake na kuwakabidhi wengine habari zake kuhusu Alivyosema na Kufanya na Kufundisha kwa kuwa walikuwa mashahidi wa hayo.
Kwa hiyo Paulo alipodai kuwa Mtume alidai kuwa mmojawapo wa kundi hilo dogo. Hasa kwa sababu alikutana na Bwana Yesu baada ya Yesu Kufufuka. Ndiyo sababu twasema Mtume Paulo siye Paulo Mtakatifu.

1: 6-9 <u>Wagalatia kuigeukia "injili nyingine</u>"

Katika nyaraka zake kawaida ya Paulo ilikuwa kuanzia na maombi na sifa kwa wale anaowaandikia. Lakini sivyo alivyofanya katika Waraka huu. Alikuwa na hali nzito, alisukumwa kusema nao mara moja, maana neno fulani limemshangaza sana.

k.6-7. Ni nini iliyomshangaza kabisa? Alisema Wakristo wa makanisa ya Galatia wanamwacha (neno la nguvu) Yeye aliyewaita, yaani Mungu. Tena, kwa upesi, kwa kushawishiwa tu. Walikubali mafundisho (injili nyingine) ya

watu waliowafikia, mafundisho yaliyo tofauti na ya Paulo, na tofauti na yale waliyoyapokea yaliyowabadilisha kimaisha na kuwafanya kuwa Wakristo.

Lakini ukweli uliopo ni kwamba hamna "injili nyingine" ila wako waliotaka kuwasumbua na kuchanganya mawazo yao hata wakafikiri kwamba iko injili nyingine. Wanamwacha Mungu wa upendo, upendo uliomtuma Yesu Kristo ili Afe kwa ajili yao.

k.8-9. Wao wasiwajali wala wasiangalie cheo na sifa zao. Je! hao watu walioleta mafundisho hayo walitoka wapi? Huenda kwa Mama Kanisa huko Yerusalem.

Wasimpokee mtu yeyote, hata yeye, hata malaika, ikiwa analeta ujumbe ulio tofauti na ule waliosikia kwa Paulo mwanzoni. Pengine wale watu waliwavuta kuithamini Torati kwa kukaza kwamba ililetwa na malaika.

Kwa ukali alisema "na alaaniwe" yaani awe chini ya hukumu na ghadhabu ya Mungu. Paulo alirudia kusema "na alaaniwe". Alitaka kuwashtusha Wagalatia ili watambue uzito wa kosa lao. Hakusema kwa kumchukia mtu fulani ambaye pengine hakumpenda, wala hakusema kwa haraka - alisema kumhusu kila ye yote aletaye habari nyingine, hata ikiwa yule mtu ni yeye mwenyewe. Alisema hivyo akimwaza Mungu na kujua yeye ni mtumishi wake aliyepaswa kumpendeza. Jambo lingine, wataupoteza wokovu wao wasipopokea neema ya Mungu katika Yesu Kristo. Dhabihu ya Yesu ndiyo itoshayo kumwondolea mtu dhambi zake na kumleta katika uhusiano mwema na Mungu. Kwa matendo ya sheria, au kwa matendo mema, hakuna awezaye kuokolewa, hata ikiwa anakubali Kristo alikufa kwa ajili yake, maana ni kusema alivyofanya Yesu Msalabani, peke yake, haitoshi.

Jambo linalohalalisha Injili si mjumbe, bali ni ujumbe, kwa hiyo, uhalali wa mjumbe unatokana na ujumbe anaouleta.

Injili ni moja tu, na hii ni Injili inayopima na kuyahukumu mawazo ya kibinadamu.

1: 10-24 <u>Asili ya Injili ya Paulo</u>

Kwa hiyo, swali la kuuliza lahusu asili ya Injili aliyoihubiri Paulo.

k.10. Adui zake walimshtaki kuwa anajipendekeza kwa watu. Alili kana shtaka lao, akionyesha kwamba haiwezekani mtu amtumikie Kristo huku akiwa na shabaha nyingine ya kupendelea watu na kujipendekeza kwao. Alisema kwamba ye ye ni "mtumwa" wa Kristo na mtumwa ni mtu anayemtumikia mtu mmoja tu. Kweli alijitahidi kuishi kama Myahudi alipokuwa nao, ili asiwakwaze kwa neno lo lote isipokuwa katika Neno la Injili. Vivyo hivyo kwa WaMataifa alijihusianisha nao kwa njia zote ili asiwakwaze isipokuwa katika yale yaliyo ya lazima kwa upande wa Injili. I Kor. 9:19 ku.

Kwa hali zote alikuwa na nia na moyo wa kumpendeza Mungu, na aliwafundisha waamini kuishi vivyo hivyo - Ef. 6:6; Kol. 3:22; na I Thes. 2:4.

k.11-l2. Baada ya kulijibu shtaka la adui zake alidai kwa nguvu kwamba hakuipata Injili kwa wanadamu, bali moja kwa moja aliipata kwa kufunuliwa na Yesu Kristo. Pia, hakuifundishwa na wanadamu. Injili si mapokeo ya kufundishwa kama Torati.

Alipokutana na Yesu aliye Hai wakati wa kwenda Dameski Mungu aliuondoa ule "utaji" uliomzuia asimtambue Yesu kuwa Masihi wa kweli.

Ni vigumu kufikiri kwamba alipoishi Yerusalemu wakati aliposoma kwa Gamalieli alikosa kujua habari za Yesu. Vilevile alipowatesa Wakristo ni vigumu kufikiri kwamba hakufahamu mambo kadha kumhusu Yesu, kwa sababu ni vigumu kufikiri sababu za kuwapinga Wakristo kama hakuwa na ufahamu kiasi fulani juu ya imani yao.

Ila neno ambalo hakulifahamu kabla hajafunuliwa na Mungu kwa njia ya kukutana na Yesu ni Yesu kuwa Masihi wa kweli na Mwana pekee wa Baba.

k:13-14. Ni nini litakalowahakikishia Wagalatia juu ya asili ya Injili aliyoihubiri. Paulo aliendelea kuwaelezea kwa kuzungumzia maisha yake kabla ya kuokolewa. Kwanza, aliipenda na kuishikilia sana dini ya Kiyahudi na Torati, hata alipita wenzake wengi wa umri wake.

Pili alikuwa na juhudi kubwa katika kulipinga Kanisa, hata kiasi cha kutaka kulifuta kabisa.

Ilikuwaje apate badiliko hilo kubwa lililopindua maisha yake? Ni Mungu Mwenyewe aliyembadilisha, kwa sababu ni Mungu tu aliyekuwa na uwezo wa kumgeuza, maana alikuwa na shingo gumu. Hakuiamini Injili hata kidogo, wala hakutaka kuiamini.

k.15-24. Halafu upinduzi wa ajabu ulifanyika. Kwanza aliacha kuitegemea haki yake mwenyewe kwa njia ya kushika Torati, bali alikubali kuhesabiwa haki kwa imani katika Kristo. Pia, alijiunga na wale wakristo ambao hapo nyuma amewatesa vikali sana. Mungu alijiingiza kwa nguvu katika maisha yake na kumfunulia kwamba Yesu ni Hai baada ya Kuuawa Kwake. Kisha Mungu huyo alimwita azihubiri Habari Njema za Kristo kwa Wamataifa hasa.

Alifanyaje mara baada ya kukutana na Yesu? Je! alikwenda Yerusalemu kwa wale waliokuwa Mitume kabla yake ili ajifunze habari sahihi za Yesu Kristo? La! sivyo. Je! alikaa Dameski ili afundishwe na Anania na Wakristo wenzake? La! hata kidogo. Mara alihubiri katika masinagogi ya Dameski halafu bila kukawia, akaenda Arabuni. Miaka mitatu ilipita kabla ya yeye kwenda Yerusalemu.

Baada ya kuokolewa hakufundishwa Injili na wanadamu. Alifanya nini huko Arabuni? Hatujui. Wengine huwaza kwamba alikwenda kuhubiri. Wengine huwaza kwamba alitulia huko akiyachunguza Maandiko ya Agano la Kale na

kufundishwa na Roho wa Mungu siri zake. Hata wengine hufananisha miaka hii mitatu na muda waliokaa Mitume na Bwana Yesu.

Alipokwenda Yerusalemu baada ya miaka mitatu alikaa siku 15 tu, alikwenda kuwatembelea akina Petro na wenzake, ili wamfahamu si wamfundishe. Allonana na wawili wa Mitume, Petro na Yakobo ndugu yake Bwana Yesu. Kwa hiyo ni uongo kwa adui zake kusema aliipata Injili kwa Mitume. Tena hao walikiri kwamba Injili aliyoihubiri ni sawa na yao k.24.

Alikuwa mhubiri wa Injili kwa mapenzi ya Mungu. Mungu alikuwa amemchagua alipokuwamo tumboni mwa mamaye (Yer. 1:5) Alimchagua, si kumjua Kristo tu, bali pia amhubiri Kristo, na hasa kwa WaMataifa.

Wagalatia walikuwa watoto wake kiroho, matunda ya Utume wake, na muhuri wa Utume huo. Ndiyo sababu aliwaka moto na kuwa mkali alipopata habari ya Mayahudishaji kuwashambulia waamini katika makanisa ya Galatia.

MASWALI

Mitume walikuwa wa pekee kwa njia gani na katika mambo gani? Kazi yao ya pekee ilikuwa nini?

Kwa sababu gani Paulo alidai kuwa Mtume halisi?

Eleza kwa nini "neema" ni baraka ya pekee kwa Mkristo?

Kwa nini "amani" ni tokeo la "neema"?

Katika kanisa lako au sharika lako kuna jambo b lote linalokufanya usikie wasiwasi? Likiwako, ni nini jambo hilo? na kwa nini unasikia wasiwasi?

Siku hizi hatusumbuliwi na Mayahudishaji na neno la Tohara na Torati. Je, unaona Jambo lo lote lililo hatari kwa Injili ya wokovu kwa neema peke yake?

2: 1-10 Maelezo ya Safari ya Pili alipokwenda Yerusalemu

k.1. Paulo alitaja safari ya pili alipokwenda Yerusalemu, iliyotokea baada ya miaka 14. (labda ni miaka 14 baada ya kuokolewa kwake). Alikwenda pamoja na Barnaba aliyekuwa Myahudi (aliyejulikana na watu wa pale) na Tito, Myunani, mtu asiyetahiriwa, mgeni kwao.

k.2. Kwa nini alikwenda? Kwanza ni Mungu aliyemwambia aende "kwa kuwa nalifunuliwa". Pengine alifunuliwa kwa njia ya unabii wa Agabo Mdo. 11:27 ku.? Mkazo wake ni kwamba hakwenda kwa kuitwa na Mitume.

Ndipo alisema "nikawaeleza Injili ile nihubiriwayo katika WaMataifa". Alichukua nafasi hiyo ili awaeleze kinaganaga Injili aliyoihubiri. Je! alikuwa akiogopa nini?

"isiwe labda napiga mbio bure, au nalipiga mbio bure". Maana yake nini? Bila shaka alikuwa akiwawaza Mayahudishaji ambao daima walikuwa wakijitahidi kuharibu sifa zake kwa njia mbalimbali. Walisema hakuwa Mtume halisi kama akina Petro na wenzake. Hakuwa na mamlaka iliyo sawa na yao. Injili yake ilitofautiana na yao.

Walijaribu kuleta mafarakano kati yake na wale Mitume wa Yerusalemu. Kama wangalifaulu kuwashawishi watu kumwonea Paulo mashaka, kazi yake ya kuieneza Injili ya kweli ya neema kwa Wagalatia na hata kwa Mataifa, ingalipoteza nguvu. Ndiyo sababu Paulo allona vema kuweka Injili aliyohubiri mbele yao. Hakuitwa nao kufanya hivyo, wala mkutano maalumu haukuitishwa. Alizungumza nao kwa faragha, na kwa wachache, hasa viongozi. Hata hivyo mazungumzo yao yalikuwa muhimu kwa maendeleo ya Injili ulimwenguni.

Tito, mmoja wa matunda yake katika WaMataifa alikuwepo. Je! watamkubali iwapo ni mtu asiyetahiriwa? Je! watakaza kwamba atahiriwe? Walimpokea Tito - neno muhimu. Paulo allona kwamba "ukweli wa Injili" ulisimamishwa k.5. Neno hilo litawapa moyo mkuu Wakristo wa Ki-Mataifa. Pia litapunguza nguvu ya Mayahudishaji kwa sababu hata katika Mama Kanisa la Yerusalemu, na mbele ya Mitume waliochaguliwa na Bwana Yesu Mwenyewe, Tito alipokelewa vizuri hali hakutahiriwa.

k.4. Ushindi huu haukutokea bila vita. Ndugu wa uongo (Paulo hakusema ndugu dhaifu) waliingia kwa siri wakimvizia Paulo ili waone atafanya nini kumhusu Tito. Waliingiaje? Pengine kwa kujifanya ni ndugu wa kweli, au kwa kujisukuma, au kwa hila fulani, tukumbuke mkutano haukuwa kwa watu wote.

Walikuwa wakipeleleza uhuru wa Mitume kufanya walivyoona ni haki kuhusu Injili. Hasa kusudi lao lilikuwa kumlazimisha Paulo amtahiri Tito. Pengine walidhani Paulo ataulegeza msimamo wake ili apate kibali cha Petro na wenzake. Labda walitumaini kushawishi baadhi ya Mitume wasimpokee Paulo asipokubali kubadili msimamo wake.
Paulo alitambua "ukweli wa Injili" uliguswa. Mtu awaye yote, ama ni Myahudi, ama ni Mmataifa, amewekwa uhuru mbali na Torati katika jambo la wokovu, kwa sababu Mungu humkubali na humhesabia haki bure kwa neema kwa njia ya mtu kumwamini Kristo na ya kuwa Alikufa kwa dhambi zake. Hivyo Tito, Mmataifa amekubaliwa na Mungu kwa kumwamini Kristo; Barnaba na Paulo, Petro na wenzake, walio Wayahudi, wamekubaliwa na Mungu kwa kumwamini Kristo Aliyesulibiwa. Haidhuru mtu ametahiriwa au hakutahiriwa, hili si kitu, iliyo lazima kwa wokovu ni mtu kumwamini Kristo na Msalaba wake.

k. 6-9. Paulo alikutana na nani na nani katika Mitume?

Alimtaja Petro (Kefa), Yohana, na Yakobo, ndugu yake Bwana Yesu (k.9) aliwaita "wenye sifa" k.2; "wenye sifa ya kuwa wana cheo" k.6; "wenye sifa

kuwa ni nguzo" k.9. Kwa nini aliwataja kwa lugha hiyo?; amekwisha kukubali walikuwa Mitume kabla yake 1:17. Tusifikiri shabaha yake ilikuwa kuwadharau, la. Pengine ni njia yake ya kuonyesha kwamba wale Mayahudishaji walikuwa wamezidi mpaka katika kuwainua kinyume chake. Aliwakumbusha kwamba iwapo wanazo sifa hizo za kuwa na cheo na kuwa nguzo, hata hivyo Mungu hajali cheo cha mtu bali moyo wake. k.6. Alisema hao hawakumwongezea kitu, nao hawakuona Injili yake ina upungufu au kasoro yo yote.

Hao wenye sifa hizo walimpokea Paulo kwa mikono miwili na kuunga mkono Injili na kazi yake, wakihesabu kwamba kama Petro alivyokabidhiwa kazi ya kuhubiri Injili kwa Wayahudi; vilevile Paulo alikabidhiwa kazi ya kuhubiri Injili ile ile kwa WaMataifa. Tusifikiri kuna Injili ya waliotahiriwa na Injili nyingine ya wasiotahiriwa, la, hata kidogo:ila kuna **kuhubiri** Injili **kwa** waliotahiriwa na kuna **kuhubiri** Injili **kwa** wasiotahiriwa.

Walikiri kwamba Paulo amepewa neema ya Mungu kwa kazi yake na walikuwa na moyo wa kushirikiana na yeye na Barnaba wakitaka waendelee na huduma yao kati ya WaMatifa. Kazi zao na yake ni moja, ila maeneo ya kazi ni tofauti.

k.10. Neno moja tu walitaka kwao - wakumbuke maskini, na Paulo aliitika kwa kusema alikuwa na bidii katika neno hilo. Waliwapelekea waamini wa Yerusalemu msaada wakati wa njaa Mdo. 11:27 ku. Baadaye Paulo aliongoza makanisa ya Ki-Mataifa kufanya changizo kwa ajili ya maskini waliokuwapo Yerusalemu (1 Kor. 16:1).

2: 11-14 Paulo aligongana na Petro huko Antiokia na kumkemea

Kwa nini Paulo alimkemea Petro uso kwa uso mbele za waamini? Sababu ilikuwa alipofika Antiokia Petro alishirikiana vizuri na waamini wa KiMataifa, akila nao bila shida. Tukumbuke jinsi Mungu alivyomtumia Petro kuwa wa kwanza kuwapokea WaMataifa, akina Kornelio na wenzake, na jinsi alivyomtayarisha kufanya hivyo kwa maono juu ya "kula" Mdo.10:15.

Mayahudishaji (tukumbuke ni Wakristo wa Kiyahudi) walifika Antiokia wakidai wametumwa na Yakobo, wakafundisha ya kuwa lazima hao waamini wa Ki-mataifa watahiriwe. Petro aliwaogopa akaacha kula na wakristo wa Kimataifa. Hata waamini wengine wa Kiyahudi wakafuata kielelezo chake. Hata Barnaba pia alivutwa kufuata kielelezo cha Petro. Huyo Barnaba alijulikana sana katika Kanisa la Antiokia na kati ya waamini wa Ki-Mataifa. Aliaminika sana na Kanisa la Yerusalemu, maana mwanzoni mwa Kanisa la Antiokia alitumwa kwao na kutoa ripoti nzuri juu yao Mdo. 11:22-26, na ni yeye aliyemtafuta Sauli (Paulo) na kumleta Antiokia na kwa kufanya kazi pamoja walijenga imani za waamini wote wa Kanisa la Antiokia, na bila shaka walikuwa na "meza moja" yaani Wakristo wote walishirikiana katika kula kwa furaha na uhuru.

Machoni pa Paulo, Petro na wale wengine walikosa kutenda sawasawa na ile kweli ya Injili k.14. Katika Injili ya kweli wote huwa sawa, wote huokolewa kwa neema tu kwa kumwamini Kristo, kwa hiyo kubagua kwa kula na Wayahudi na kutokula kwa WaMataifa ni kutokutenda sawa na Injili ya neema. Pia ni unafiki k.13. Kwa kweli kwa imani Petro aliamini Injili ya kweli ila kwa tendo hilo alikuwa amekosa kuifuata, kwa sababu ya woga.

Paulo alisimama imara wala hakujali kwamba ni Petro aliyekosa, Petro aliye nguzo, mtume aliyechaguliwa na Bwana Yesu Mwenyewe na kuwekwa kuwa "mwamba". Si kwa sababu alisikia wivu juu yake. Alijua Mungu amemtumia sana kuvuta Wayahudi kumwamini Kristo. Ila katika jambo hilo la kuacha kula na waamini wa KiMataifa amekosa na kosa hilo likiachwa litaleta vurugano kubwa na ufa katika Kanisa. Bwana ni Mmoja, Injili ni moja, kwa hiyo lazima "meza" iwe moja tu. Petro alikwenda kinyume cha maono aliyopewa na Mungu Mwenyewe Mdo.10:9-20; 44-48; 11:2-18.

Ni wazi kwamba bado aliiamini Injili ya kweli ya kuokolewa kwa neema tu k.14b. ila alisukumwa na wale Mayahudishaji wa Yerusalemu kufanya kinyume chake. Ni woga uliomfanya atende kwa unafiki, yaani alifanya kinyume cha alivyoamini.

Neno la Tohara kwa Wakristo wa KiMataifa lilitengenezwa katika Baraza Kuu la Kanisa lililofanyika Yerusalemu kama BK.49. Mdo.15:1-2; na katika Baraza hilo Petro alisimama imara. Bila shaka alisaidiwa kwa kukemewa na Paulo. Katika Baraza hilo Yakobo alikana kwamba ni yeye aliyewatuma hao Mayahudishaji GaI. 2:12: Matendo 15:24.

Twajifunza mambo mawili makubwa: (I) Twapaswa kuishi maisha yanayopatana na Injili; (2) Twapaswa kuishindania ukweli wa Injili kwa pande zote mbili - ukweli wa imani na utekelezaji wake kimaisha.

2:15-21: <u>Kuhesabiwa Haki kwa kumwamini Yesu Kristo:</u>

Katika sehemu hiyo Paulo amesema kama Myahudi, akitoa ushuhuda mkali. Kwa ujuzi wake wa kibinafsi alipokuwa Myahudi aliishi kwa jitihada kubwa katika kuishika Torati, akitafuta kupata haki kwa kutii sheria zake. Ila hakufaulu kupata haki aliyoitafuta. Walakini alipomwamini Kristo alipewa bure haki kamili, aliletwa katika uhusiano mwema na Mungu na kusikia amani moyoni. Neno "kuhesabiwa" hutokea mara nne katika k.16 na k.17.

Kuhesabiwa haki kwa imani ni fundisho kubwa, la maana sana, ni kiini cha Injili. Neno "kuhesabiwa" lina maana gani? ni neno la "uhakimu" la kumtangazia mtu kuwa "hana hatia", tena "kuwa na haki". Ni tendo la Mungu kwa mwenye dhambi; kumsamehe na kumhesabu kuwa hana hatia, na zaidi kumpokea na kumtendea kama ni· mwenye haki. Mungu aweza kufanya hivyo kwa sababu Yesu alihesabiwa mwenye dhambi alipozichukua dhambi zetu mwilini mwake pale Msalabani. Aliadhibiwa badala yetu ili sisi tusiadhibiwe dhambi zetu 2 Kor.5:19-21; Is. 53:5-6.

Wayahudi walijaribu kuisimamia haki yao kwa kutii sheria za Mungu Ru. 10:3, lakini hakuna aliyeweza kufaulu kushika kwa ukamilifu sheria za Mungu. Ni Yesu peke yake ambaye amefaulu kumtii Mungu kwa ukamilifu; hakuwa na dhambi, hakujua dhambi, wala hakufanya dhambi. Kwa hiyo kumwamini Yesu Kristo ni kujikabidhi Kwake ili tushirikishwe utii wake, na maisha yake yasiyokuwa na dhambi, na Kifo Chake cha mwenye dhambi alipobeba dhambi zetu na Kufa kwa ajili zao.

k.17 ku. Watu walihofu kwamba fundisho hilo litafanya watu wasijali jinsi walivyoishi. Paulo alisema "hasha" kwa wazo hilo. Katika kuhesabiwa haki twaunganika na Kristo na kuletwa kwenye uhusiano wa ki-binafsi na Mungu. Hivyo mtu hubadilika sana kimaisha, huwa ni kiumbe kipya, ni kama mtu ambaye amekufa kwa maisha yake ya nyuma na kufufuka kwa maisha mapya. Kwa hiyo atawezaje kurudia maisha ya nyuma ikiwa ameunganika na Kristo Aliyesulubiwa na Kufufuka, maana Kristo ataishi ndani yake. k.20.

k.21. Ikiwa mtu ataweza kuokolewa kwa matendo ya sheria kwa kweli Kristo alikufa bure; lakini Kristo hakufa bure.

Tukitafuta kuisimamia haki yetu mwenyewe twamwudhi Mungu na Yesu Aliyekufa kwa ajili yetu, na kukanyaga chini neema yake. Hamna njia mbili za kupata haki.

MASWALI

Je ilikuwa busara kwa Paulo kwenda Yerusalemu? Ni faida zipi zilizopatikana kwa safari hiyo?

Waonaje juu ya Paulo kumkemea Petro wazi mbele za watu? Zungumza kama ni wajibu wetu kushambulia yale matendo yanayokana "ukweli" wa Injili.

Katika kweli ya "meza moja" yaani Wayahudi na WaMataifa kushirikiana katika kula pamoja, waonaje juu ya madhehebu mengine ya Kikristo ambayo hayakaribishi wengine kwenye Meza ya Bwana? Je! neno hilo ni sawa?
Weka katika maneno yako mwenyewe fundisho la "Kuhesabiwa haki kwa Imani".

3:1-5 <u>Ujinga wa Wagalatia</u>

k.1-2. Lugha ya Paulo ni ya ajabu, ni lugha inayoonyesha jinsi alivyojisikia aliposhangazwa na mageuzi yaliyotokea katika imani ya Wakristo hao. "ni nani aliyewaloga" pengine alitambua ni hila ya Shetani aliye nyuma ya Mayahudishaji waliowashawishi: Yoh. 8:8:44.

Alipohubiri kwao kwa mara ya kwanza aliwaambia sana sana juu ya Yesu Kristo kusulibiwa, alisisitiza kabisa kwamba katika Kifo chake Kristo amefanya yote yaliyotakiwa kwa wokovu wao, iliyobaki wamwamini. Ni kama alifanya wamwone Kristo kwa macho yao ya kiroho pale Msalabani, akizibeba dhambi zao ili wao waipate Haki yake. Msalaba ni kiini cha Injili I Kor. 1:23; 2:2.

Je! waliuitikaje ujumbe huo wa Paulo? waliuamini na kumpokea Kristo maishani mwao na Mungu aliwapa Roho Mtakatifu, ili wawe na nguvu ya kuishi maisha mapya. Walionja nguvu hiyo katika maisha yao, walijua kwa ujuzi wa binafsi Injili ni "nguvu ya Mungu ya kuokoa" I Kor. 1:18.

Mungu aliwakubali iwapo hawakutahiriwa. Haikudhaniwa walihitaji neno lingine zaidi ya kumwamini Kristo. Kwa kifupi, waliokolewa kwa neema.

Ndipo wakaja Mayahudishaji waliowafundisha ya kuwa wapaswa kutahiriwa na kuishika Torati ili wakamilike ki-imani. Na Wagalatia waliwasikiliza na kuyakubali mafundisho yao. Paulo aliwauliza swali "mmekuwa wajinga namna hii? Ujinga gani? ujinga wa kuishi maisha ya Kikristo katika uwezo wa Roho halafu sasa kuendelea kwa uwezo wao wenyewe, si katika Roho bali katika mwili kwa kutahiriwa. Walitazamia kupata nini zaidi ya waliyopata mwanzoni? Paulo aliona ya kuwa badala ya kupata faida watapata hasara, hata ya wokovu wao.

k.4-5. Tena hapo nyuma walikubali kuteswa kwa imani yao, huku Mungu akiwapa msaada wa Roho Mtakatifu ili wawe na nguvu ya kuendelea vema. Pia Mungu alikuwa amefanya miujiza kati yao. Na hayo yote wakati walipomwamini Kristo tu.

Wakiacha kuishi kwa imani **peke yake na kuongeza** matendo ya sheria itakuwaje? wakianza kujitegemea kwa sehemu na kumtegemea Mungu kwa sehemu watafika wapi? Iwapo Paulo hakusema wazi ni kama alidokezea kwamba hawataonja nguvu ya Roho wala kuona matendo makubwa ya Mungu katika miujiza. Kwa nini? kwa sababu hayo yalitokea wakati walipomwamini Kristo bila nyongeza yo yote. Tusifikiri hao Mayahudishaji walifuta neno la imani, la siyo, ila walileta nyongeza ya tohara na matendo ya sheria. Haiwezekani kuongeza kitu kwa neema, au neema si neema tena. Kuongeza kitu ni kumwudhi Mungu na kuidharau kazi ya Kristo Msalabani kama haikutosha.

3: 6-8 <u>Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani</u>

Bila shaka hao Mayahudishaji walisema sana juu ya uzuri wa Musa na Torati ambayo Mungu alimpa kwa njia ya malaika. Lakini Paulo aliwakumbusha habari za Ibrahimu aliyekuwa baba wa taifa. Paulo alionyesha kutoka Maandiko kwamba Ibrahimu anao wana wengi, baadhi yao wengi huwa WaMataifa, nao ni wale wote wenye imani katika Kristo.

Ibrahimu alihesabiwa haki kwa imani Mw.15:6, na kwa njia ya kuiamini ile ahadi aliyopewa na Mungu. Hivyo,.alipata kibali cha Mungu na kuletwa katika hali ya kushirikiana na Mungu. Aliahidiwa uzao usiohesabika, na ahadi hiyo alipewa kabla ya kutahiriwa, na miaka mingi kabla haijaja Torati. Alipoitwa Mungu alimwahidi "katika wewe Mataifa yote watabarikiwa" Mw. 12:3. Baraka gani? ya kuhesabiwa haki kwa imani na kupewa Roho. Ni akina nani watakaoirithi ahadi

hiyo? Ye yote yule amwaminiye Kristo (mzao wake) ama ni Myahudi, ama ni Mmataifa. Mw. 22:17-18; Mdo 3:25; Math. 8:11. Watoto wa kweli wa Ibrahimu si wale wa kimwili bali wale wa kiroho.

3: 9-14 Tofauti kati ya Imani na Matendo ya sheria matendo mema?

Swali kubwa ni "mtu awezaye kupata kibali cha Mungu na kuwa na uhusiano wema naye?"

k.10. Neno la kwanza ni kuona ya kuwa wale wanaoishi kwa kufanya matendo mema **ili** waokolewe huwa chini ya laana si baraka. Kwa nini? kwa sababu hakuna awezaye kuzitimiza sheria zote za Mungu, na kule kutokuzitimiza ni laana. Kama mtu angeweza kuzitimiza, kweli angebarikiwa na kupata kibali cha Mungu na kuishi kwenye uhusiano wema naye Lawi. 18:5. Kwa upande wa sheria neno kuu ni utendaji, kwa kuwa sheria hudai "fanya hii, usifanye hii". Mtu akikosa Mungu hawezi kumhesabia haki, maana ni mkosaji, ana upungufu katika kutimiza yote aliyodaiwa na sheria, atashinda hii na kushindwa na hii, kwa kuwa wanadamu wote ni wenye dhambi Ru. 3:22-23. Bila shaka hao Mayahudishaji walishangaa kusikia kwamba wako chini ya laana.

Neno la kushukuru ni kwamba Mungu amefaulu kupata njia ambayo kwayo mtu aweza kuipata ile haki anayodaiwa. Ni njia ya kuhesabiwa haki, yaani, kupewa haki ya Kristo bure kwa kumwamini.

Imewezekanaje? Ni kwa sababu Kristo alikubali kuchukua laana yetu na dhambi zetu pale Msalabani ili sisi tuondolewe laana hiyo ya dhambi zetu, na badala yake tupewe Haki ya Kristo Kol. 2:15; Kum. 21:23. maana ni Yeye peke yake aliyemtii Mungu kwa ukamilifu wote. Tukiisha kumwamini Yeye na kazi yake ya upatanisho Msalabani, basi Yeye huja kuishi ndani yetu kwa njia ya Roho na kutuushirikisha ushindi wake.

Kwa hiyo kuna mawili mbele yetu; baraka au laana, uzima au mauti, kuishi kwa imani au kuishi kwa matendo ya sheria au kwa mchanganyiko wa imani na matendo ya sheria; wa kutegemea kazi ya Kristo Msalabani tu, au kutegemea kazi zetu pia.

3: 15-29 Mahali na Shabaha ya Torati katika Mpango wa Mungu

Paulo aliendelea kwa kusema zaidi juu ya Ibrahimu, Musa na Torati. Mungu alifanya Agano lake na Ibrahimu na kumweka kuwa Baba wa taifa teule la Kiyahudi. Kwa sababu Mungu alitoa ahadi, itikio lililotakiwa kwa upande wa Ibrahimu lilikuwa kuiamini tu. Ahadi hii kwa sababu ni ahadi ya Agano haiondolewi au kubadilishwa na mambo ya baadaye. Agano hilo lilihusu "mzao" wa Ibrahimu k.16 na mzao huyo ni Kristo.

k. 17-18. Torati ilitolewa baadaye, lakini haikuletwa ili ibadili neno lo lote la ahadi.

k.19-21. Shabaha ya Torati: Kwa nini Torati ilikuja baada ya muda na baada ya hiyo ahadi ya Agano? Ililetwa ili watu watambue ni wakosaji wasioweza kulifikia lengo la "haki" inayodaiwa na Mungu. Tena iliingizwa kwa muda mpaka Kristo atakapokuja. Akija Kristo, ndipo haitahitajika. Paulo hakuidharau hiyo Torati, maana Mungu aliitoa kwa Musa mjumbe wake kwa njia ya malaika.

Kama ni hivyo upo uhusiano gani kati ya Torati na Ahadi? Yote mawili yametoka kwa Mungu; Mungu yule mmoja aliyeitoa ahadi kwa Ibrahimu ni Mungu yuleyule aliyeitoa Torati kwa Musa. Yote mawili yalilenga "Haki".

Tofauti ni katika "uwezo". Sheria haina nguvu ya kuhuisha, haina nguvu ya kumwezesha mtu kuishika. Ingekuwa na uwezo huo basi tungeweza kuipata Haki kwa njia yake, wala Kristo asingalikuwa na haja ya Kufa kwa ajili yetu.

Ajabu ni kwamba Injili **NI** "nguvu ya Mungu ya kuokoa" I Kor. 1:18. kwa imani Kristo huletwa kwetu ili aishi ndani yetu kwa njia ya Roho, hivyo twaushirikishwa ushindi wake.

Twaweza kufananisha Torati na Mbao unaotuonyesha ni njia ipi ya kuelekea na umbali wa maili kadha ya kusafiri, ni mzuri, ni msaada, hata hivyo, mbao hauna uwezo wa kutufikisha mahali pale tunapotaka kupafikia. Au ni mfano wa daktari anayetuambia ni ugonjwa gani tulio nao, bila kuwa na dawa za kuutibu.

k.24. Hapo Paulo amejumlisha kazi na mpaka wa Torati. Torati ilikuwa kiongozi, ilitoa nuru ya kutuelimisha mapenzi ya Mungu na kututayarisha kumpokea Kristo. Ru. 3:20: 4:15: 7:7 Kristo alipokuja Torati ilitimiza kazi yake.

3:25-29. Katika Kristo Mungu ametufanya kuwa watoto wake kwa sababu tumemwamini Kristo, na katika kubatizwa tumemvaa Kristo; tumekubali kuwa wafuasi wake. Yeye ni kiongozi wetu, hatuna haja ya uongozi wa Torati.

Kuokolewa kwa neema kwafanya tofauti za watu kuwa si kitu. Tofauti za ukabila, za tabaka, za wanadamu kuwa wa kiume na wa kike, hizo hazihesabiwi. Tu wazao wa Ibrahimu, tumeirithi ahadi ya baraka ya kuhesabiwa haki kwa imani.

MASWALI

Je, siku hizo wako wakristo wanaofanana na Wagalatia ambao walianza maisha yao ya kikristo kwa kumwamini Yesu Kristo na kazi yake aliyoifanya pale Msalabani kuwa yatosha, ndipo baadaye wametaka kuweka "nyongeza" wakidhani watakuwa Wakristo bora zaidi? Kama unafiriki kwamba wa namna hiyo wako, sema ·ni akina nani? na ni nini wanaiotaka kuongeza?
Zungumza ni kwa njia gani Amri Kumi zinamhusu Mkristo wa leo.

4: 1-11 <u>Kuwa watumwa ndipo Kufanywa kuwa Wana</u>

Paulo aliendelea na hoja yake kuhusu Torati na Injili. Iwapo ahadi ya urithi ilikuwepo watu hawakuweza kuuingia urithi wao haoi Kuja kwa Kristo. Paulo alitumia mfano wa mtoto ambaye ni mrithi wa mali ya babaye, lakini wakati wa kuwa mtoto yu chini ya watunzaji, anaishi kwa kuongozwa nao na kuambiwa la kufanya, hana uhuru, hana tofauti na mtumwa, hana budi kungojea wakati wa kurithi ulioamriwa na babaye.

Vivyo hivyo katika mambo ya kiroho. Wakati wote wa Agano la Kale ahadi ya urithi iliyotolewa kwa Ibrahimu ilikuwapo. Lakini watu walikuwa chini ya Torati, mfano wa mtoto ambaye bado hajaufikia wakati wa kurithi.

k.4. Mambo hayo yalibadilika kabisa alipokuja Yesu Kristo. Tangu Kuja Kwake watu waweza kuuingia urithi wao. Waweza kuondoka katika hali ya kuishi chini ya Torati na kuingia katika hali ya kufanywa kuwa wana wa Mungu na kuishi kama "wana" wakimwita Mungu "Baba" na kuishi katika familia yake. Wakiwa wana ni warithi wa ahadi za Mungu, wahesabiwa haki kwa imani, wasamehewa dhambi zao, wapewa Roho, na kuonja uzima wa milele.

Uwezekano wa kuondoka chini ya sheria na kuishi kama wana hutokana na Ukombozi alioufanya Yesu Kristo alipokuwa Msalabani. Kwa kazi yake hali yetu imebadilika, hatuwi tena watumwa, hatuishi kwa madai ya Torati; pia, tu wana, tunaishi kwa nguvu ya Roho Mtakatifu. Torati ilikuwa nje yetu, andiko tu, lisilo na nafsi, mfano wa kitu baridi kisichotia mtu moyo wala joto. Roho yu ndani yetu kama Mfariji, mwenye Nafsi, akitutia nguvu na moyo wa kumpendeza Mungu.

Mungu alimtuma Mwana wake ili tupate kuwa wana. Alimtuma Roho ili tulipofanywa kuwa wana tuhakikishiwe uana wetu. Rumi 8:15-16. Ni Mungu aliyefanya hayo yote kwa njia ya Yesu kuchukua laana ya Torati na adhabu ya dhambi zetu mwilini mwake pale Msalabani.

Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Pia alikuwa mwanadamu kweli, aliyezaliwa na mwanamke. Alizaliwa kwa Myahudi, kwa hiyo alikuwa chini ya Torati. Katika maisha yake yote alimtii Mungu kikamilifu, akawa Mwenye haki: hakuna mwanadamu aliyemtangulia wala aliyemfuata ambaye amefaulu kutimiza madai yote ya sheria.

Mambo hayo matatu yatosha kumstahilisha kuwakomboa wanadamu. Asingalikuwa mwanadamu asingaliweza kukomboa wanadamu. Asingalikuwa mwanadamu mwenye haki asingaliweza kuwakomboa wanadamu walio na dhambi, na asingalikuwa Mwana wa Mungu asingaliweza kukomboa wanadamu kwa Mungu ili wawe wana wake.

4:8-11. Hao Wakristo wa Galatia walikuwa wameonja katika maisha yao uzuri wa kuwa "wana". Ila sasa wamekuwa katika hatari ya kurudia hali ya utumwa kwa kurejea kuishi kwa matendo ya sheria na kuishi kwa kujali mambo

manyonge yasiyo na faida kwao wala uwezo wa kuwaokoa. Ni ajabu kufikiri kwamba aliye "mwana" atataka kuwa "mtumwa", ila kwa ujanja wa Mayahudishaji itatokea kuwa hivyo wakikubali mafundisho yao.

k.11. Paulo alihofu kwamba taabu zake zote za kuleta Injili kwao kwa kuvumilia shida za usafiri, na ugumu wa maisha, na mateso aliyoyapata, na upinzani wa wale waliojaribu kuharibu sifa zake na kazi zake za Injili - taabu hizo zote zitakuwa bure ikiwa Wagalatia watakubali kushawishiwa na Mayahudishaji, na kuupoteza uhuru walioupata katika Kristo kweli watakuwa wajinga kabisa kabisa!!.

4: 12-20 <u>Paulo aliwasihi kwa Upendo</u>

Katika sehemu hiyo Paulo alisema nao kwa upendo kwa kuwafunulia jinsi alivyojisikia moyoni mwake. Aliwaita "ndugu" na kuwasihi wawe kama yeye. Hakueleza wawe kama ye ye katika mambo gani. Bila shaka alitaka wamwamini Kristo peke yake na kuishi kwa neema ya Mungu, waishi kama "wana" si kama watumwa. Alipokuja kwao alijihusianisha nao bila kujali yeye ni Myahudi na wao ni WaMataifa, wala hakujifanya kuwa mkubwa (I Kor.9:20-22). Yeye hakuwa na neno lo lote juu yao. Alikumbuka jinsi walivyompokea kwa mikono mwili, kama alikuwa malaika, hata Yesu Mwenyewe.

k.13-15. Inaonekana alipofika kwao alishikwa na ugonjwa fulani ulioharibu sura yake. Iwapo sura yake haikupendeza hao Wagalatia hawakumdharau, walikuwa tayari hata kuyang'oa macho yao - maneno hayo yamefanya watu kufikiri Paulo alikuwa na shida ya macho. Au labda ni usemi uliotumika wakati ule. Walisikia ni baraka kubwa naye kuwa haidhuru alikuwa na shida hiyo.

k.16: Ila sasa anapowaandikia hali hiyo yote imebadilika. Walimwona kama ni adui yao - kwa nini? kwa sababu imempasa awaambie kweli ambazo hawakupenda kuzisikia. Kwa nini kweli hizo hawakupenda kuzisikia? Ni kwa sababu Mayahudishaji wameleta mafundisho yaliyogongana na ukweli wa Injili ya neema iliyohubiriwa na Paulo. Paulo hakuwa na njia nyingine isipokuwa kuusimamia ukweli wa Injili. Asipofanya hivyo watajikuta wako utumwani.

k.17. Huenda wale Mayahudishaji waliwalainisha Wagalatia kwa kuwapaka mafuta kusudi waukamate usikivu wao. Si vibaya wawe na shauku juu yao ikiwa shabaha yao ni kuwaleta kwenye uhuru wa wana wa Mungu. Hata Paulo alikuwa na shauku juu yao. Lakini wale Mayahudishaji hawakuwa na shabaha njema; walitaka kuwavuta kwao si kwa Kristo. Wangalifaulu kuwavuta kwao wangaliwatumikisha wafanye walivyotaka wao.

Katika k.12 Paulo aliwaita Wagalatia "ndugu zangu" na katika k.19 aliwaita "vitoto vyangu". Alisema kama mama, lakini si kwamba alitaka wamwonee shauku, au ya kuwa atawale imani yao, la, ila nia yake alitaka "Kristo aumbike ndani yao" zaidi ya Kristo kuwa ndani yao alitaka wafanane na Kristo ndiyo shabaha ya kuokolewa kwetu Rumi 8:29-30. Paulo alisikia utungu, yaani

maumivu, ili wazaliwe tena. Lugha hiyo huonyesha mzigo aliokuwa nao kwa ajili yao.

Kwa hiyo tofauti kubwa kati yake na Mayahudishaji ni dhahiri Wao walitaka kutawala imani na kuwa mabwana juu ya Wagalatia ila Paulo alitaka Kristo aumbike ndani yao. Kwa sababu ya shida hiyo ambayo imezuka katika makanisa ya Galatia Paulo alitamani sana kuwa pamoja nao, kwa maana alisikia wasiwasi sana juu ya uaminifu wao kwa Injili ya neema. (Mdo. 20:29- 30)

4: 21-31 Wana wawili wa Ibrahimu - Ishmaeli na Isaka

Paulo ali~~endelea na hoja yake juu ya Neema na Ma~~tendo ya Sheria kwa kuutumia mfano wa Ibrahimu. Ibrahimu alipewa ahadi ya kupata "mwana" atakayezaliwa kwa uwezo wa Mungu kwa kuitimiza ahadi yake.

Muda ulipoendelea na huyo mwana hakuonekana, basi, Sarai alimshauri bwana wake amchukue Hajiri, mjakazi wake, na kuzaa naye. Hajiri alipochukua mimba akamdharau Sarai, ndipo Sarai akamlaumu Ibrahimu na kumtesa Hajiri, hata Hajiri akakimbia pamoja na Ishmaeli mtoto wake. Mungu alimtokea jangwani akamwambia arudi kwa Sarai. Akarudi. Ibrahimu na mkewe walizidi kuzeeka na uwezekano wao wa kuzaa mtoto ulikwisha. Ndipo Mungu alimtokea Ibrahimu na kumwambia kwamba mwakani Sarai atamzaa mwana. Ikatokea hivyo, na ahadi ya Mungu ilitimia. Wakati wa sikukuu ya kumwachisha mtoto Sarai akamwona Hajiri akimdhihaki, akaumizwa. Ikambidi Ibrahimu awafukuze Hajiri na Ishmaeli. (Mw.16; na 17:15-22: 21:1-21).

Katika matukio hayo Paulo aliona kwamba yalikuwepo maagano mawili; moja la utumwa na moja la uhuru; moja linalotokea kwa matendo ya mwili; moja linalotokea kwa ahadi na uwezo wa Mungu. Moja la sheria lisemalo "fanya hii, usifanye hii" na moja la neema lisemalo "Mungu atatenda hili na hili" moja ni Agano la Kale, na moja ni Agano Jipya.

Tena Paulo aliona ulinganifu kati ya Hajiri kumwudhi Sarai na Mayahudishaji waliomwudhi yeye na waamini wa Injili ya neema. Pia katika tendo la Ibrahimu kumfukuza mjakazi Hajiri na mtoto wake, na Mungu kuondoa Agano la Kale na Kuingiza Agano Jipya, kwa kuwa mtoto wa mjakazi hatarithi kabisa bali mwana wa mwungano ndiye atakayerithi.

Mayahudishaji ni mfano wa Hajiri na Ishmaeli mtoto wake, na Paulo na waamini wa Injili ya neema ni mfano wa Isaka. Ni Isaka aliyemrithi babaye, na waliookolewa kwa neema ni wazao wake kiroho.

Kwa nini Paulo aliutumia mfano huu iwapo waamini wengi wa Galatia hawakuwa Wayahudi kwa asili? Ni kwa sababu ya mafundisho ya Mayahudishaji waliokaza sana Tohara na Torati na Musa na hao Wagalatia wameanza kutaka kuwa chini ya Torati, eti! Ukristo wao uwe kamili!! Uongo mkubwa!!

Mpaka leo wako wengi ambao hufikiri kwamba njia ya kupata kibali cha Mungu ni njia ya kushika sheria, nao hutenda mema kwa shabaha ya kumvuta Mungu awapokee, lakini kweli iliyopo ni kwa sisi kuamini alivyofanya Mungu kwa njia ya Yesu, tumpokee Yeye, ndipo tutafurahi na kuonyesha shukrani zetu kwa njia ya matendo mema. Ni mizizi inayobeba matawi si matawi yanayobeba mizizi - mizizi ni imani, na matawi ni matendo mema. Ef. 2:8-10.

MASWALI

Kwa njia gani twafanywa kuwa "watoto wa Mungu"? twajaliwa baraka zipi tunapokuwa watoto Wake?

Ni kwa sababu zipi Kazi alizofanya Yesu Msalabani zilikubalika na Mungu? Kama mwingine angalikufa msalabani Je? tokeo lake lingalikuwa wokovu? Eleza. Mayahudishaji walikuwa na shabaha gani hasa? Je! mapasta na viongozi wa Kanisa wapata majaribu hayo? Wajifunze nini kutokana na kielelezo cha Paulo?

5: 1-6 <u>Wagalatia wapaswa kuchagua Kristo au Sheria</u>

k.1. Paulo aliona jambo kuu la "uhuru" limefungamana katika habari hiyo. Katika Kristo wamewekwa uhuru na uhuru huo wataupoteza wakikubali mashauri ya Mayahudishaji na kutahiriwa. Budi wasimame imara. Wameondolewa nira ya Torati, wamefanywa kuwa "wana" wenye kibali cha Baba, hawawi tena watumwa wa kujistahilisha kwa Baba 3:13.

2-6. Ni nini itakayotokea wakitahiriwa? watapata faida gani? watapata hasara gani? Paulo alisema hasara ni kutengwa na Kristo, na kuondoka katika hali ya neema. Kristo hatawafaidia neno, kwa sababu katika Kristo tohara si kitu. Tena, wakichagua Torati watawajibika kushika sheria zote. Paulo aliyekuwa Myahudi, ambaye hapo nyuma aliona fahari juu ya Tohara Fil: 3:4-6; hali akijitahidi sana kushika sheria zote alijua njia hiyo ni ya kushindwa tu.

Lakini sivyo ilivyo kwa imani. Kwa imani wahesabiwa haki, wapewa Roho, na kwa Roho wawezeshwa kuishi kwa upendo ambao ndio kutimiza torati kikamilifu. Imani inayookoa ni imani iliyo hai, imani inayofanya kazi.

5: 7-15 <u>Uhuru wa kweli</u>

Katika sehemu hiyo Paulo alidokezea kwamba huenda ni mtu mmoja aliye nyuma ya jitihada za Mayahudishaji na kuwatia nguvu, k.7 "ni nani" k.9 "yeye anayewafadhaisha atachukua hukumu yake awaye yote".

k.9. Mafundisho ya Mayahudishaji yalikuwa yakienea na wasipotahadhari waamini wote watanaswa. Ndiyo sababu Paulo aliwaandikia ili awasaidie Wagalatia wasizidi kuteleza.

k.10. Paulo alitumaini "katika Bwana" hao watu hawatafaulu na ya kuwa Wagalatia watatambua kosa lao na kujirekebisha. Aliamini kwamba kiongozi wao atapatwa na hukumu ya Mungu.

Inaonekana hao Mayahudishaji walithubutu kudai kwamba hata Paulo alihubiri habari za Torati, lakini yeye akakana kabisa. Alishuhudia kwamba kama angalihubiri tohara angaliepa mateso.6:12: Paulo alisema sababu moja ya wao kuhubiri tohara ilikuwa wasiudhiwe, wala kuteswa.

Yeye alimhubiri Kristo na Msalaba wake, na ya kwamba ni Kristo peke yake ambaye amefanya **yote** yaliyotakiwa kwa wokovu; iliyobaki ni kwa watu kuamini Kito Chake kimetosha. Ila ujumbe huo wa Msalaba unakwaza, maana watu hawapendi kuambiwa kwamba hawawezi kufanya lo lote kwa wokovu wao, na ni lazima Waje kwa Kristo na Msalaba wake na mikono mitupu.

Kuhubiri matendo mema ni kuwaambia watu waweza kuchanga kitu kwa wokovu wao. Ujumbe huo huwafurahisha na kulisha kiburi chao.

k.12. Paulo alipowaza hao Mayahudishaji na kuona hasara wanaoleta kwa hao Wagalatia alitaka wajifanye kuwa matowashi na kutoweka nchini. Maneno hayo huonyesha mzigo na upendo wa Paulo kwa Injili na waamini wake. Wivu juu ya Utukutu wa Kristo ulikuwa sehemu ya upendo wake kwa Kristo na Kazi yake

k.13-15. Ni Mungu aliyewaita katika Injili, kwa neema yake, na shabaha yake ilikuwa wasaidiane katika upendo. Wakiishi kwa upendo, ambao Roho atamimina mioyoni mwao watatimiza sharti kuu la Torati, la upendo Ru. 5:15; 13:8-10. Wakiutumia uhuru wao vibaya watazidi kugombana na kuumana na mwishowe wataangamizana.

5: 16-26 <u>Kuenenda katika Roho</u>

Paulo alikaza haja ya kuwa na Roho, kuenenda na Roho, na kuongozwa na Roho, kusudi wazae matunda ya Roho. Mwili una nguvu wa kudai tamaa zake zitimizwe, lakini wapaswa kufanya vita na hizo tamaa. Wakiongozwa na Roho hawana haja ya uongozi wa sheria.

Ndipo Paulo aliorodhesha matendo ya mwili, na kusema wazi kwamba wafanyao hayo hawataurithi uzima wa milele k.21.

Matendo ya mwili ni uasherati n.k. bali pia yagusa eneo la dini - ibada ya sanamu, uchawi n.k. pia yagusa uhusiano kati ya watu - ugomvi, wivu, hasira n.k. pamoja na kugusa mambo ya kiasi katika kula na kunywa - ulevi, ulafi. Kisha Paulo aliorodhesha tunda la Roho ambalo wanaoongozwa na Roho huzaa. Tunda la Roho kwa upande wa Mungu ni upendo, furaha, na amani. Kwa upande wa uhusiano wetu na watu ni uvumilivu, utu wema, na fadhili:
Uaminifu, upole na kiasi huthibitisha ukweli wa mtu na uwezo wake wa kujitawala. Mkristo wa kweli ni yule aliyeusulibishwa mwili pamoja na mawazo

yake mabaya na tamaa zake. Ni mtu anayejihesabu ni mtu kwa dhambi ili amwishie Mungu.

Kwa hiyo uhuru tulio nao ni uhuru "katika Kristo" si uhuru wa kufanya dhambi bali ni uhuru mbali na nguvu za dhambi. Pia ni uhuru mbali na sheria na hukumu yake ili tusishtakiwe na dhamiri, kusudi tuwe huru kumtii Mungu kwa furaha na kwa moyo. Tumekubaliwa naye kwa neema, kwa hiyo hatuna hofu mbele zake, twaweza kumkaribia wakati wo wote bila wasiwasi tukijua Kristo amekuta kwa ajili yetu.

Wengi ambao hudhani wako huru ni watumwa wa dhambi na tamaa zake.

Siri kubwa ni Roho Mtakatifu. Katika sehemu hiyo Paulo amemtaja mara saba. Roho hutulinda ili tuwe huru kwelikweli.

MASWALI

"Nimeokolewa kwa neema, kwa hiyo naweza kufanya nipendavyo". Zungumza usemi huu, ukionyesha hali ya uhuru wa kweli katika Kristo.

Eleza kwa nini Mkristo apaswa kufanya matendo mema, na uhusiano kati ya matendo mema na kuokolewa kwa neema tu.

Kwa nini watu huona shida katika kuupokea wokovu kama kipawa kutoka kwa Mungu?

Kwa nini Roho ni muhimu sana katika maisha ya Mkristo? Ni mambo gani na maisha gani yanayothibitisha mtu kuwa ana Roho maishani mwake?

6: 1-5 <u>Mausia Kadha</u>

Paulo alifundisha kwamba ushuhuda mkubwa wa kuwa na Roho utaonekana katika uhusiano wetu na wengine: 5:25-26. Tutaonyeshaje upendo wetu kwa wengine?

6:1-5 Njia moja ni kwa jinsi gani tutakavyomfanyia mtu aliyeanguka katika kosa bila kukusudia. Tutamwinua na kwa upole kumrudisha. Si vema kumlaumu wala kuwa mkali. Tutajaribu kumsaidia katika hali ya kujua hata sisi wenyewe twaweza kuanguka tusipojihadhari. Si vizuri kumwacha mtu katika kosa Math. 18:15 ku. Watakaoweza kufanya hivyo ni wale wanaoongozwa na Roho. Tutakuwa wapole tukiutambua udhaifu wetu.

k.2. Ni wajibu wetu kuchukuliana mizigo Tukifahamu mtu fulani amelemewa na jambo fulani tushirikiane naye na tuubebe mzigo wake mzito kwa pamoja. Kwa njia hiyo twaitimiza sheria, huenda Paulo alitaja sheria katika kuiwaza kuwa mzigo mzito usiobebeka. Hatuna haja ya kulemewa na Torati nzito, ila tuna haja ya kusaidia ubebaji wa mizigo ya watu. Tuwe na mabega ya nguvu.

k.3. Kama hatuoni vema kuwasaidia wengine kwa kubeba mizigo yao, huenda ni kwa sababu hatutaki kunyenyekea. Labda shida yetu ni kujiona kwamba haifai tujishushe hivyo. Paulo alisema kwa mtu wa namna hiyo asidanganyike, maana yeye si kitu iwapo anajiona ni bora.

k.4-5. Yampasa mtu aipime kazi yake mwenyewe, wala asijilinganishe na mwingine na kujiona ni bora. Akitambua ya kuwa kazi yake ni nzuri, vizuri, ila awaze hivyo mwenyewe tu wala asijisifu kwa wengine. Kwa kuwa kila mtu ataulizwa ya kwake tu.

Twajibika kuwasaidia wengine kuibeba mizigo yao mizito, lakini "furushi letu" yaani mzigo wetu mdogo tulio nao twaubeba mwenyewe tu. Katika siku ya hukumu kila mtu atahukumiwa kuhusu mambo yake tu, wala hakuna atakayebeba hukumu ya mwingine.

6: 6-10 <u>Kupanda na Kuvuna</u>

Siri hii kubwa imo katika Uumbaji, pia katika maisha ya wanadamu. Mkulima anayetaka kuvuna lazima kwanza azipande mbegu ardhini, na mavuno yatategemea ni mbegu wa aina gani alizopanda na mahali alipopanda. Akipanda ngano, ngano atavuna, kufuatana na hali ya mbegu na ardhi kama zilikuwa nzuri au siyo, na kwa kiasi cha mbegu alichopanda. Mkulima akitaka mavuno mengi mazuri ni lazima apande mbegu nzuri kwa wingi katika ardhi nzuri.

Na kanuni hiyo huongoza maisha ya wanadamu kiadili na kiroho. Kazi ya kupanda ni ya maana zaidi ya kuvuna. Ayu. 4:8 na Hos. 8:8:7. Hii ni kanuni ya asili iliyowekwa na Mungu wala haibadiliki.

k.6. Mungu aliweka ya kwamba watumishi wa Neno lake watunzwe na wale wanaofundishwa Lu.110:7; I Kor. 9:11..

Ipo hatari kwa wahudumu kuwa wavivu, na kupata zaidi ya walivyostahili. Shida ni kwa sababu kazi zao huwa tofauti na kazi za kawaida. Hawawi chini ya uangalizi mkali, wapaswa kujisimamia, hakuna wa kuwaambia "leo, fanya hii na hii". Hali hiyo ya kujisimamia si rahisi.

Hata hivyo ni vizuri wahudumu wasiwe na haja ya kufanya kazi nyingine ili wapate ya kutosha kuishi; ni vema wawe na nafasi kubwa ya kushughulikia Neno la Mungu. I Tim. 5:5:17.

Ipo hatari nyingine. Pengine watu wa mtaa hutaka kumtawala mhudumu na kumsukuma afanye wanavyotaka, kwa sababu, eti, wanamlipa!! Pengine watamlaumu kwa mahubiri yake n.k. Akiwa mwaminifu katika kupanda Neno la Mungu anastahili kuvuna "mshahara" wake. Ushirikiano mzuri unatakiwa kati ya mkufunzi na wanafunzi wake. Wao hupata kwake chakula cha kiroho na yeye hupata kwao chakula cha kimwili.

k.7. Paulo aliwaonya "wasidangyike" "Mungu hadhihakiwi" Twaweza kujidanganya, lakini hatuwezi kumdanganya Mungu.

Haiwezekani kuepa kanuni hiyo ya kupanda na kuvuna. Tukifuata mambo ya mwili tutavuna uharibifu. Tukifuata mambo ya Roho tutavuna uzima wa milele. Katika sura ya 5 Paulo amekwisha kutaja vita iliyopo kati ya mwili na Roho. Ni juu yetu kupanda kwa Roho na kutokupanda kwa mwili, kwa kuwa uvunaji si jambo la bahati nasibu. Utu wetu wa zamani haukufutika tulipookolewa, kwa hiyo twapaswa kuusulubisha, yaani kuhesabu kwamba tumekufa kwa matakwa ya mwili - tuwe kama mfu, maana mfu haitiki anapoitwa. Tufanane na huyo mfu, tusiziitikie tamaa za mwili zinapotuita kwa nguvu wala tusijiweke mahali pa majaribu, tujitenge na wale wenye mashauri mabaya.

Kupanda kwa Roho ni kuwaza na kukaza nia zetu kwa Mungu Kol. 3:1-2. Tujitoe kwa maombi, kwa kujifunza Neno la Mungu, kwa ibada, kwa kusoma vitabu vitakavyotujenga kiroho, na katika maisha ya kila siku kufanya iliyo haki, na kwa maburudisho tucheze michezo mizuri na kufurahia uzuri wa uumbaji n.k. na kushirikiana na wale wenye maongezi yanayojenga.

k.9-10. "tusichoke katika kutenda mema" tusilegee, tusikate tamaa, kwa sababu upo muda kati ya kupanda na kuvuna. Mkulima huhitaji subira mpaka mimea imekua, na kuzaa, na kuiva, tayari kwa uvunaji.

Kwa hakika tutavuna mbeleni, kwa hiyo hapo kati tuendelee katika kutenda mema, na hasa kwa waamini wenzetu. Tutieni moyo wa kuendelea mpaka mwisho. Ru. 2:7.

Tutumie nafasi zote zilizopo katika kuwatendea watu mema. Ni wazi kwamba kuokolewa kwa neema kunatoa nafasi na wajibu wa kutenda mema, katika hali ya kujua tumeisha kukubalika na Mungu, hatuna haja ya wasiwasi ya kujistahilisha.

6: 11-18 <u>Paulo kufunga Waraka; Fahari yake katika Msalaba wa Kristo, akichukua chapa zake</u>

Hapo Paulo aliufunga Waraka. Alichukua kalamu kutoka mkalimani wake (desturi yake ilikuwa kutumia mkalamani) Alipenda kufunga nyaraka zake kwa mkono wake mwenyewe kama thibitisho la barua kuwa yake 2 The. 3:3:17.

Alisema herufi zake ni kubwa. Kwa nini ziwe kubwa? Labda alijitetea hali ya mwandiko wake kwa kuwa hakuzoea kuandika kama wale wenye kazi ya uandishi. Pengine ilikuwa shida ya macho, Gal. 4:13-15 au pengine ni kwa sababu alitaka kukaza mambo kadha muhimu, kwa hiyo aliandika kwa herufi kubwa ili auvute usikivu wa wasomaji wake.

k.12. Hayo mambo muhimu ni mambo gani? Ni tofauti kubwa kati ya yeye na Mayahudishaji ambayo hasa ilihusu kiini cha imani ya Kikristo. Je! imani hii yahusu mambo ya nje au mambo ya ndani? ya tohara, au ya kufanywa kiumbe kipya kwa ndani? Kwa Mayahudishaji jambo kubwa lilikuwa tohara, wakiwashurutisha hao Wagalatia. Hapo nyuma, waliokolewa kwa neema, sasa waambiwe lazima watahiriwe.

Paulo alionyesha kwamba shabaha yao haikuwa njema. Kwanza walitaka kuepa maudhi; pili, walikuwa wanafiki kwa sababu wenyewe hawakuishika torati; tatu, walitaka kuona fahari juu ya Wagalatia kwa upande wa mwili. Kwake Paulo, tendo la tohara liligusa mtu katika mwili wake; roho yake haikuguswa.

Ni kitu gani kilicho cha maana zaidi? Katika k.15 Paulo alijibu. "ni kiumbe kipya" kwa wale waliotahiriwa na kwa wale wasiotahiriwa. Tohara ni alama ya nje tu, inayotakiwa ni moyo wa ndani utahiriwe Ru. 2:29, na hii ni kazi ya Mungu. Kufanywa kuwa kiumbe kipya ni kazi ya Roho wa Mungu.

(Ubatizo wapaswa kuwazwa kama tohara kwa sababu ni nje ya mtu na unafanywa na wanadamu, ila tofauti kubwa ni Bwana Yesu aliagiza waamini wabatizwe ili waikiri wazi ile imani iliyomo moyoni).

k.14: Paulo aliweka tumaini lake lote katika Msalaba wa Kristo. Alikataa kabisa asione fahari katika jambo 10 lote lingine. Alikwisha kupita katika hali ya kutafuta haki kwa njia ya Sheria, akashindwa. Alipokutana na Bwana Yesu aliye Hai alijikabidhi Kwake, akapewa haki ya Kristo; na tangu hapo aliacha kuitegemea haki yake mwenyewe Fil. 3:3:4-11.

Alikuwa tayari kuudhiwa na kuteswa kwa ajili ya Kristo, aliamua kutokujali ulimwengu umfanyie nini, maana alijihesabu ni mfu kwa dunia, mwili, na dhambi.

k.16. "Israeli wa Mungu" ni wale wanaomwamini Kristo, walioupokea wokovu kwa neema, nao wameirithi ahadi kwa Ibrahimu na kuingia mahali pa "watu wa Mungu" yaani Israeli ya zamani, wao ni Israeli Mpya na taifa teule I Pet. 2:9- 10.

k.17. "chapa zake Kristo" ni nini? Twajua Paulo aliteswa sana kwa ajili ya Kristo (2 Kor. 11:23-25). Alipigwa mawe alipokuwa Listra, kiasi cha watu kufikiri amekufa. Mdo. 14:19. Pengine kovu za jeraha zingalizikionekana mwilini mwake. Liko wazo la kufikiri Paulo alijifananisha na mtumwa ambaye alichomwa alama mwilini mwake iliyoonyesha kwamba yeye ni mali ya bwana fulani. Huenda Paulo amewaza kwamba yeye amechomwa alama ya namna hiyo kwa njia ya mateso, na mateso hayo yalionyesha yeye kuwa mtumwa wa Yesu. Mayahudishaji waliona fahari ya tohara; bali yeye aliona fahari juu ya mateso aliyoyapata kwa ajili ya kumtumikia Kristo. Kwake alama inayouthibitisha ukweli wa imani ya mtu ni mateso si tohara 1Thes. 3:3:3.

Mwishowe Paulo alisema kwamba hataki kusumbuliwa zaidi. Daima Mayahudishaji wamemfuatafuata, wamejitahidi kuondoa mamlaka yake, wamejaribu kuharibu sifa zake na kazi yake.

Katika Waraka huo ametoboa wazi Injili ya neema. Mwishowe aliwakabidhi Wagalatia kwa neema ya Bwana Yesu. Kitu kikubwa ni NEEMA ya Kristo si Tohara wala Torati.

MASWALI

Tunao wajibu gani kwa wengine?

Mfano wa kupanda na kuvuna kunakusaidiaje?

Kwa nini maisha ya Kikristo ni maisha ya vita? na tufanye nini ili tushinde katika vita hiyo?

Mahali ulipo Je! wakristo wanateswa? na ikiwa wanateswa, wanateswa kwa njia gani? Je! mateso hayo ndiyo dalili ya uaminifu wao kwa Injili?

WARAKA KWA WAEFESO

YALIYOMO

UTANGULIZI

(a) Mji Mkuu wa Efeso
(b) Mwandishi
(c) Madhumuni ya Waraka
(d) Ujumbe wa Waraka

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam za Paulo
1: 3-14 Sifa kwa Makusudi ya Mungu na baraka katika Kristo
15-23 Maombi kwa kujaliwa ujuzi wa kiroho.

2: 1-10 Kuhuishwa kutoka kwa “wafu”
11-22 Upatanisho wa Wayahudi na WaMataifa

3: 1-13 Heshima ya kuwa watangazaji wa upatanisho huo
14-21 Maombi

4: 1-6 Kuudumisha umoja
7-16 Utofauti katika umoja
17-24 Maisha mpaya badala ya maisha ya zamani
25-5:2 Ukweli na upendo badala ya uongo na uchungu

5: 3-14 Nuru badala ya giza 15:21
Hekima badala ya ujinga
22-23 Uhusiano mwema wa mume na mke

6: 1-4 Uhusiano mwema wa wazazi na watoto
5-9 Uhusiano mwema wa mabwana na watumwa
10-20 Vita ya Kikristo
2l-24 Ujumbe wa mwisho na salaam za kuagana

U T A N G U L I Z I

(a) Mji Mkuu wa Efeso
Efeso ulikuwa mji mkuu wa Jimbo la Asia katika Dola ya Kirumi. Ulisitawi sana na bidhaa nyingi ilipitia bandari yake, ila wakati wa Waraka huu kuandikwa hali yake ilianza kupungua, hata hivyo mji huo uligusa maisha ya wengi wa sehemu zile kwa sababu kutoka pale mawazo mengi ya dini na falsafa yalienezwa. Ibada ya mungu mke Artemi (Diana kwa KiLatin) ilisitawi. Katika Mdo.19:27 twaona nguvu yake.

Ila kabla ya kuendelea ni vema tuseme machache kuhusu Kanisa la Efeso kuwa ndilo Kanisa hasa lililoandikiwa barua hiyo. Sababu moja kubwa inayosababisha tufikirie jambo hilo yahusu nakala kubwa za zamani za Maandiko, kwa kuwa hizo hazina neno “Efeso”. Pamoja na sababu hiyo iko nyingine inayohusu hali ya Waraka, maana hautaji watu binafsi ila Tikiko tu. Tena lugha yake isipokuwa katika sehemu chache ndogondogo si ya kibinafsi. Neno hilo lasumbua wengine maana Paulo alikaa pale miaka mitatu, tena alipoagana na wazee wa pale alisema nao kimoyomoyo na kwa lugha ya mapenzi (Mdo.20:17ku).

Baadhi ya wataalamu wafikiri kwamba Waraka uliandikwa kwa Kanisa la Efeso pamoja na makanisa ya eneo lile. Huenda yule aliyekwenda na barua alikuwa na nakala zingine na alipofika kanisa fulani alililiingiza jina la mahali pale au nakala ilikuwa moja ya kuyazungukia makanisa kadha. Labda ni nakala ya Efeso iliyohifadhiwa, ama kwa sababu Efeso ulikuwa mji mkuu wa eneo lile au ni kwa bahati tu. Ila si wataalamu wote wanaounga mkono mawazo hayo.

Yawezekana hali ya lugha yake imesababishwa na mambo makuu yaliyozungumzwa katika Waraka, maana Paulo alisema juu ya mambo makuu kuhusu mpango mzima wa Mungu juu ya vitu vyote vya mbinguni na duniani. Hakusema juu ya matatizo n.k. kwa hiyo hakuwa na haja ya kutumia lugha ya kibinafsi.

(b) Mwandishi
Ni Mtume Paulo kama alivyojitaja mwanzoni mwa Waraka. Wakati wa kuandika alikuwa kifungoni (3:1; 4:1; 6:20) huenda alikaribia mwisho wa kufungwa kwake BK.60/61. Tikiko alikwenda na barua hiyo na Paulo alisema kwamba Tikiko atawapasha habari zake. Pamoja na kwenda Efeso Tikiko alisafiri mpaka Kolosai pamoja na Onesimo aliyekuwa akirudi kwa bwana wake Filemoni. Tikiko alizichukua Waraka kwa Wakolosai na Waraka kwa Filemoni (Kol.4:7) Waraka kwa Waefeso hufanana sana na ule kwa Wakolosai, zaidi ya vifungu 55 vyalingana.

(c) Madhumuni ya Waraka
Inaonekana hayakuwapo matatizo ya imani au maadili, tofauti na Waraka kwa

Wagalatia na Nyaraka kwa Wakorintho ambazo ziliandikwa kwa shabaha ya kuyatatua matatizo yaliyokuwapo.

Wataalamu huhesabu Waraka huo kuwa wa kwanza kwa ubora wa hali yake. Umejaa mawazo ya hali ya juu ukisema juu ya Makusudi Makuu ya Umilele ya Mungu, makusudi ambayo hutimizwa katika Yesu Kristo na kutekelezwa kwa njia ya Kanisa na ndani yake. Kiini cha hayo yote ni Upatanisho uliofanyika pale Msalabani, Kristo alipokufa kwa ajili ya dhambi. Matokeo ya Upatanisho huo ni Uzima Mpya, Jamii Mpya, Maadili Mapya, na Uhusiano Mpya, mambo yanayozungumzwa humo.

Waraka waweza kugawiwa katika sehemu mbili. Sura ya I hadi ya 3 zahusu theologia, yaani imani yenyewe. Ndipo sura ya 4 hadi 6 zahusu maadili yanayopatana na imani hiyo.

(d) Ujumbe wa Waraka
Neno kuu la ujumbe lapatikana katika 1:9-10 “akiisha kutujulisha siri ya mapenzi yake, yaani kuleta madaraka ya wakati mkamilifu, atavijumlisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni, na vitu vya duniani pia, naam katika Yeye huyo”. Neno kuu ni upatanisho.

Kabla ya kumaliza sehemu hiyo ya utangulizi ni vema kusema kwamba ni vigumu kuusoma Waraka huo kwa upesi kwa sababu vifungu vyake ni virefu, maneno yanafuata maneno bila kituo. Kwa hiyo ni vizuri kurudiarudia kusoma sehemu zake. Kufanya hivyo ni msaada katika kuyafahamu yaliyoandikwa.

U F A F A N U Z I

1:1-2 Salaam za Paulo
Salaam hizo ni kama kawaida ya siku zile. Mwandishi alijitaja, ndipo walioandikiwa walitajwa, kisha salaam zenyewe. Ila Paulo aliinua hali ya salaam kwa kusema juu ya uhusiano wake na walioandikiwa na uhusiano wa yeye na wao na Mungu kwa njia ya Kristo, hivyo salaam zilipata hali ya kuwa baraka.

Paulo alijitaja kuwa Mtume wa Kristo Yesu, mtu aliyejaliwa heshima ya hali ya juu pamoja na kuupewa wajibu mzito kwa sababu ya utume alioupewa. Uhusiano wake na watu uliongozwa na kutawaliwa na jambo hilo. Alikaza kuwa hayo yote yalitoka kwa Mungu na mapenzi yake, si kwa kutaka kwake, kwa hiyo ni zaidi ya kuwa na ruhusa ya Mungu. Ni Mungu aliyemchagua kuwa Mtume, na kwa sababu hiyo alikuwa mali ya Mungu kufanya alivyotaka Mungu, hivyo alikuwa chini ya mamlaka yake hata alipokuwa akiuandika Waraka huo. Tukilinganisha na 1 Kor.15:9; Gal.1:13-15; 1 Tim.1:12-16 aliamini kabisa kwamba yeye mwenyewe hakustahili kuitwa kuwa Mtume. Pamoja na hayo

alikuwa mtu aliyetumwa na Yesu Kristo na ujumbe maalum. Ili alitimize lengo la kuchaguliwa kwake na kutumwa kwake alishirikishwa uwezo wa Kristo.

Wale walioandikiwa aliwaita “watakatifu”, neno linalotokea mara nyingi katika Agano Jipya, na asili yake ni katika Agano la Kale. Maana ya kwanza ya neno hilo ni kutengwa kwa ajili ya kumtumikia Mungu, mfano wa jengo fulani kutengwa na kuwekwa wakfu kwa ibada. Mkazo si katika hali ya utakatifu wa kumstahilisha mtu amtumikie Mungu. Hata hivyo walioitwa watakatifu na kutengwa hivyo watazamiwe kuishi maisha matakatifu. Waumini wote waitwa kuwa watakatifu, si wito kwa wachache tu wanaofikiriwa kuwa na hali bora kuliko wenzao, la. Paulo aliwasalimia kama watu waliomwekea Yesu tumaini lao na kuwa waaminifu Kwake.

Kwa kujumlisha twaweza kusema kwamba Mkristo hasa ni mtu aliye “katika Yesu Kristo” ambaye maisha yake yameungana na Kristo kama tawi na mti, au mzizi na udongo (Yn.15:1ku. Kol.3:1-3). Katika 1:1-14 maneno “katika Yesu Kristo” na “katika Yeye” yametokea mara 11. Mkristo ni mtu mwenye anwani mbili, moja ya hapa duniani, mahali anapoishi, pia ana anwani ya pili nayo ni “katika Kristo” akiishi “katika Kristo” maisha ya kiroho.

k.2 Ndipo Paulo aliwasalimia kwa maneno “neema” na “amani” baraka zitokazo kwa Mungu Baba na kwa Bwana Yesu Kristo. Paulo alipenda sana maneno hayo na alitumia mara nyingi kwa kuyataja pamoja. Maneno hayo yanajumlisha baraka kubwa za Wakristo. Neema husema juu ya kipawa cha bure cha Mungu, kipawa cha kukubalika naye bila masharti na bila kustahili. Kwa kibali hicho Wakristo wamejaliwa “amani ya Mungu”. Yesu Kristo ndiye “amani yetu” na “Yesu Kristo ndiye aliyefanya amani” (2:14,15) Amani hiyo haitawaliwi na mambo ya nje, kwa sababu imesababishwa na Kifo cha Kristo pale Msalabani. Neema na amani ni baraka za Injili.

Katika vifungu hivi viwili vya kwanza Yesu Kristo ametawala mawazo ya Paulo. Kwanza Paulo mwenyewe ni Mtume wa Yesu Kristo, ndipo walioandikiwa ni wale wanaomwamini Kristo, kisha neema na amani vyatoka kwa Kristo.

1:3-14 <u>Sifa kwa Makusudi ya Mungu na baraka katika Kristo</u>

Kuanzia k.3 moja kwa moja Paulo alianza kumsifu Mungu sana sana. Alitaja baraka juu ya baraka zitokazo kwa Mungu Baba bila kusimama. Katika Kigriki hamna vituo, ni kama kifungu kimoja kinachoendeleaendelea. Pia ni kama wimbo, wimbo mzuri sana. Inaonekana alipoanza kutaja baraka moja, mara aliwaza nyingine, halafu nyingine, halafu nyingine. Na baraka alizozitaja ni za kiroho zipatikanazo katika Kristo.

Baraka ya kuchaguliwa na Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, baraka ya kufanywa wana, baraka ya ukombozi na msamaha wa dhambi, baraka ya ufahamu wa mapenzi yake, baraka ya heshima ya Wayahudi na

WaMataifa kuwa Wake kwa usawa, na baraka ya kutiwa muhuri ya Roho Mtakatifu kama arabuni ya urithi wa baadaye.

Yapo mambo matatu katika wimbo huo. La kwanza ni kwamba Mungu, tangu milele hadi milele, hufanya kazi katika mambo yote kufuatana na makusudi yake makamilifu. Historia yote, wanadamu wote, na kila kilichopo mbinguni na duniani, vyote vimo katika makusudi hayo.

Jambo la pili ni kwamba makusudi yake hutimizwa katika Kristo, kwa hiyo kila baraka ambayo watu hushiriki ni kwa njia ya Kristo. Jambo la tatu ni kwamba kwa upande wa wanadamu lengo ni matokeo ya utendaji, ili wawe kwa "sifa ya Utukufu wake".

k.3 "atukuzwe Mungu" Katika Agano Jipya neno hilo limetumika kwa Mungu peke yake. Watu hubarikiwa wanapopata baraka zake. Mungu hutukuzwa anaposifiwa kwa baraka zote anazozitoa kwa ukarimu kwa watu wa ulimwengu huu. Zaidi ya yote Mungu hutukuzwa kwa kuwa ni Baba wa Bwana Yesu Kristo, maana Mungu amejifunua kwetu kwa ukamilifu kwa njia ya Kristo, Mwana wake, ambaye ni sura kamili ya Baba yake. (Rum.15:6; 1 Pet.1:3; Ufu.1:6; Yn.1:18; Ebr.1:1-3).

k.3 Katika "ulimwengu wa roho" usemi huo Paulo ameutumia mara kwa mara katika Waraka huo (1:20; 3:10; 6:12). Katika Efe.2:6 alisema kwamba tumefufuliwa na Kristo na tumeketi pamoja na Kristo katika "ulimwengu wa roho". Iwapo tunaishi hapa duniani, pia tunaishi mbinguni, hali tumeinuliwa juu. Kwa hiyo baraka tulizo nazo haziharibiki wala haziwezi kuvamiwa na wezi, nondo (Mt.6:1-20; 1 Pet.1:4)

k.4 Asili ya makusudi ya Mungu si katika ulimwengu huu, kwa kuwa yalikuwepo hata kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Fundisho la "uchaguzi" lapatikana katika sehemu zote za Maandiko. Zamani za Agano la Kale taifa la Israeli liliteuliwa na Mungu kwa kusudi maalumu ya kutayarisha njia ya Kristo kuja hapa duniani. Uchaguzi wao haukutegemea ubora wao, wala wingi wa watu wao, wala jambo lolote walilolifanya ila Mungu aliamua kuwateua, basi (Kum.7:6-8). Katika Agano Jipya uchaguzi hauhusu kabila au taifa fulani, bali ni kuhusu watu wowote, shabaha ya Mungu ilikuwa kuunda taifa jipya kabisa lililo na watu wa kila aina, kabila, n.k. Fundisho la uchaguzi halitajwi kama ni jambo la kujadiliwa, wala halipingi fundisho lingine katika Maandiko juu ya watu kuwa na hiari ya kuchagua. Ni fumbo ambalo Agano Jipya halilifumbui na akili zetu za kibinadamu zashindwa pia.

Katika maandishi yake Paulo aliutilia mkazo mambo mawili yaliyo tofauti. Moja ni makusudi makuu Mungu aliyoyakusudia tangu milele na ya pili ni uhuru wa wanadamu kuchagua. Hivyo aliwatangazia watu wote Injili ya neema. Wale walioipokea aliwaambia fundisho la uchaguzi, na alifanya hivi kwa sababu

mbili. Ya kwanza, alijua kwamba Mkristo huhitaji kujua hakika kwamba imani yake inategemea kabisa kazi ya Mungu, haina asili katika jambo lolote la upande wake. Yote ni kazi ya Bwana kulingana na mapenzi yake aliyokuwa nayo hata kabla hatujaumbwa. Sababu ya pili ni kwamba Mungu ametuchagua ili tuwe watakatifu na bila lawama mbele zake. Kwa hiyo, tumechaguliwa, si kwa kuokolewa tu, bali zaidi kwa kuishi maisha matakatifu (Efe.2:10; Kol.1:22; Yn.15:16; Rum.8:29; 2 The.2:13, 2 Tim.1:9; 1 Pet.1:2).

Tukirudia kutazama maneno aliyoyasema Paulo “kama vile alivyotuchagua katika Yeye” twaona kwamba Mungu alituchagua kabla hatujaumbwa ili tukombolewe na kazi ya Kristo ambayo ilikuwa bado haijafanyika”. Hilo ni fumbo kweli, na neema kubwa!!

“watu wasio na hatia mbele zake katika upendo” Lengo la maisha ya Mkristo ni utakatifu kamili (Mt.5:48) Kwa upande mmoja ni kujitoa kabisa kufanya mapenzi ya Mungu na kwa upande wa pili ni kuwa bila waa, wala doa wala kosa. Jambo hilo linatukumbusha habari za wanyama waliotolewa sadaka nyakati za Agano la Kale. Iliamriwa wawe wakamilifu, bila mawaa (Law.1:3,10; Ebr.9:14; 1Pet.1:19). Pia Paulo aliweka maneno “mbele zake” yaani usafi unaotakiwa ni kwa kipimo cha Mungu si cha wanadamu. Paulo mara kwa mara alishuhudia kwamba alijitahidi kuishi “mbele zake” (Rum.1:9; 2 Kor.4:2; Gal.1:20; 1 The.2:5) “katika upendo” maisha ya utakatifu hukamilishwa kwa njia ya upendo (1The.3:12ku). Baadhi ya wataalamu hufikiri kwamba maneno “katika upendo” yahusu k.5 kwa hiyo k.5 kisomwe “katika upendo alitangulia kutuchagua..” Labda ni hivyo.

k.5 Hapo tena mkazo ni kwamba mpango wa Mungu kwa watu wake ulipangwa katika umilele. Na mpango wake ni nini hasa? Ni kwa sisi kufanywa kuwa watoto wake kwa njia ya Yesu Kristo. Wanadamu waliumbwa ili washirikiane na Mwumba wake kama watoto na Baba yao (Mwa.1:26; Mdo.17:28) lakini dhambi ilipoingia heshima hiyo ya kuwa watoto ilipotezwa. Sasa, kwa neema, kwa njia ya Kristo, watu waweza kurudishiwa heshima ya “uana” (Yn.1:l2; Rum.8:15,23; Gal.4:5). Desturi ya kufanywa wana (adoption) ilikuwa desturi ya Kirumi si ya Kiyahudi. Desturi hiyo ni mfano mzuri wa mpango wa Mungu. Mtoto aliyefanywa kuwa mtoto wa familia fulani alihesabiwa sawa na mtoto aliyezaliwa katika familia hiyo. Ni heshima aliyopewa tu, kwa neema si kwa haki. Hayo yapatana kabisa na mapenzi ya Mungu. Mungu alipenda kufanya kwa njia ya neema.

k.6 “usifiwe utukufu wa neema yake” (k.12, 14) Utukufu wa Mungu ni nini hasa? Ni udhihirisho au mwangaza wa tabia zake jinsi alivyo hasa. Tabia zake zimedhihirishwa wazi kabisa, na neema ndiyo tabia yake kubwa. (Kut.33:18-20; 34:5-7) Wayahudi walichaguliwa ili waishi kwa sifa zake (Isa.43:21) vivyo hivyo, wale ambao Kristo amewapokea wapaswa kuonyesha tabia ya Baba yao, Baba wa neema, ili Baba atukuzwe kwa njia ya maisha yao mema. Kristo ni

Mpenzi wa Babaye, ni Mwana wa Pendo lake (Kol.1:13). Yeye ni mboni wa jicho lake, naye anaishi daima ndani ya Pendo la Babaye. Vivyo hivyo sisi tulio ndani ya Kristo twashirikishwa huo upendo wa Baba kwa Mwana wake, twaishi ndani ya upendo huo.

k.7 Hapo Paulo ametaja baraka moja kubwa ya neema, nayo ni ukombozi. Haja kubwa ya kwanza ya wanadamu wote ni msamaha wa dhambi. Katika Kristo, na kwa njia ya Kufa Kwake, msamaha umepatikana. Paulo alihesabu jambo hilo kuwa kubwa mno ambalo asili yake ni katika "wingi wa neema yake". Ukombozi huo ulimgharimia Kristo maisha yake, kwa kuwa alimwaga damu yake ili atukomboe (Rum.3:24; Kol.1:14; Mdo.20:28; 1 Kor.6.20; 1 Pet.1:18, 19; Ufu.5:9). Wakati wa Agano la Kale watu walifundishwa kwamba dhambi haiondolewi kwa urahisi, wakosaji walitakiwa kuchinja mnyama mzuri, asiye na mawaa, na kuimimina damu yake madhabahuni (Ebr.9:22). Maana ya neno la "ukombozi" ni kuweka huru, yaani mtu au kitu kutolewa chini ya utawala fulani. Dhabihu ya Kristo imetuweka huru mbali na utawala wa dhambi, ili tuwe Wake.

k.8 Paulo bado hajafikia upeo katika kuisifu neema ya Mungu katika Kristo. "alituzidishia hiyo katika hekima yote na ujuzi". Picha ni ya neema kuwa kama mto unaofurika maji, yaani baraka. Zaidi ya kuwapokea watu, na kuwafanya kuwa watoto wake, na kuwasamehe, Mungu huwajalia ufahamu wa makusudi yake, akiwatia nuru ya kutambua hizo baraka. Hekima na ujuzi ni kuelewa kichwani pamoja na kujua la kufanya, ili kweli za umilele ziletwe kwenye maisha ya kila siku.

k.9 Hayo yawezekana kwa sababu Mungu amelifunua lengo na shabaha ya kuumbwa kwetu na kuishi kwetu. Paulo ametumia maneno "siri ya mapenzi yake". Haina maana ya kuwa ni siri iliyofichwa ili isijulikane, la, bali ni "siri" isiyoweza kufahamika nje ya Mungu kuifunua. Tena ni siri ambayo haikujulikana hapo nyuma kabla ya Kuja kwa Kristo (Kol.1:26; 2:2; 4:3; Rum.16:25-27).

k.10 Ni nini hasa makusudi ya Mungu kuhusu wakati huo na nyakati zote hadi mpaka mwisho, wakati wa makusudi hayo kuufikia utimilifu, wakati ulioitwa "wakati mkamilifu" na Paulo. Hapo twaona kwamba mpango wa Mungu unahusu historia yote ya ulimwengu, kwa hiyo ni dhahiri kwamba historia ina maana na shabaha, nayo inasogea kwenye lengo tukufu lililoamriwa na Mungu. Ni nini hasa lengo la Mungu ambalo analitekeleza kila wakati?

Jibu ni katika maneno "kuvijumlisha vyote katika Kristo, vya mbinguni na vya duniani". Kujumlisha ni kuleta pamoja au kukusanya. Neno limetumika mara moja nyingine katika Agano Jipya (Rum.13:9). Kristo ni kichwa cha Kanisa (k.22) ila katika ulimwengu mafarakano yangalipo. Mbeleni mafarakano yote

yatakoma, umoja utapatikana katika Kristo. Kitu chochote kisichokubali kupatanishwa kitafutwa.

“Vitu vyote” kwanza ni waumini wote waliokufa pamoja na wale walio hai wakati wa mwisho.. Pamoja na malaika, na viumbe vyote, maana uumbaji utawekwa huru mbali na uharibifu (Rum. 8:18ku). Mpango wa Mungu ni kwa vitu vyote vilivyoumbwa kwa njia ya Kristo, na kwa ajili yake, ambavyo pia hushikana katika Yeye (Kol.1:16,17) viwekwa pamoja na kujumlishwa katika Kristo, naye ataviongoza na kuvitawala, kwa kuwa Yeye ni mrithi wa vyote (Ebr.1:2). Katika “wakati mkamilifu” mafarakano yatakoma na hali yoyote iliyo kinyume cha Kristo na tabia yake itakomeshwa.

Kwa hiyo ni vema tukumbuke kwamba hiyo kazi ya kujumlisha na kukusanya ni kazi inayofanyika katika mwenendo wa historia hata wakati wa sasa. Kila kitu kiliumbwa katika Kristo (Kol.1:16) lakini dhambi ilipoingia mafarakano na fitina vilitokea. Kwa Kifo chake cha Upatanisho uwezekano wa kila kitu kurudishwa kwenye uhusiano mwema na Mwumba wake upo, na kila kitu chaweza kuitimiza shabaha ya kuumbwa kwake. Kwa njia ya kumtii Kristo umoja utazidi (Kol.1:20). Kristo ni Wakili Mkuu katika nyumba ya Mungu na watumishi wake ni mawakili chini yake. Yeye huongoza kila kitu kwa hekima, hali akielewa wakati ufaao kwa kila jambo.

k.11-12 Katika vifungu hivi inaonekana Paulo aliwazungumzia Wayahudi, ndipo katika k.13 WaMataifa. Chanzo cha Mungu kutekeleza makusudi yake kilikuwa katika kuwateua Wayahudi kuwa watu wake. Hao walikuwa kama fungu lake, ili anyoshe njia kwa Kuja Kwake Kristo. Baada ya Kristo Kuja na kuufanya ukombozi WaMataifa pia waliingizwa katika mpango wa Mungu ili wawe watu Wake. Ndipo zaidi na zaidi Injili inahubiriwa kila mahali katika utekelezaji wa mpango huo wa kujumlisha yote katika Kristo. Waisraeli walichaguliwa kuwa “sifa ya Utukufu Wake” (Isa.43:21) Hawakuchaguliwa kwa faida yao au kwa sababu nyingine isipokuwa hiyo. Inatazamiwa kwamba ulimwengu wote utazitambua tabia njema ya Mungu, Mungu mwenye kujaa neema tele, Mungu Mtakatifu asiyeweza kuridhiana na dhambi hata kidogo, hata hivyo, ni Mungu ambaye hupenda wenye dhambi na kuwatamani sasa waje kwenye toba ili awasamehe dhambi zao. Neema ya Mungu huonekana wazi kabisa katika Msalaba wa Kristo.

“sisi tuliotangulia kumwekea Kristo tumaini letu” Labda maneno hayo yahusu waumini wa kwanza. Au pengine ina maana ya Wayahudi walioishi kabla ya Kristo kuzaliwa, kwa sababu walitumaini kumpata Masihi wakimngojea kwa hamu.(Mdo.28:20; Ling. Rum.1:16; 2:9ku).

Kwa vyovyote twajifunza kwamba historia si jambo la bahati nasibu. Mungu hufanya kazi ulimwenguni akiwa na Mapenzi yake yaliyokusudiwa katika

umilele, mapenzi yasiyobadilika, potelea mbali vipingamizi na vizuizi vifanyavyo kuyazuia. Hakika mwishoni ni Mapenzi yake peke yake yatakayosimama.

k.13-14 Hapo neno lahusu WaMataifa wanaomwamini Kristo, hao nao wameingizwa na kuushirikishwa urithi wa Watu wa Mungu kwa sababu wameweka tumaini lao kwa Kristo. Wamo "katika Kristo" sawa na waumini wa Kiyahudi, na kwa shabaha ileile ya kuwa "sifa ya utukufu wake". Waliiamini Injili ilipohubiriwa kwao nao wamejaliwa "wokovu" kwa kusamehewa dhambi zao nao huzishiriki baraka zote zipatikanazo katika Kristo. Pamoja na hayo wametiwa muhuri ya Roho Mtakatifu, thibitisho la kuwa mali ya Mungu, na kuwa wana wa kweli.

Zamani zile vitu vya watu vilitiwa muhuri ya kuonyesha ni mali ya mtu fulani. Kwa Wayahudi tohara ilikuwa muhuri, ila kwa Wakristo ni Roho Mtakatifu, isipokuwa wengine watauona ubatizo pia ni muhuri. Kazi kubwa ya Roho ni kuwathibitishia waumini "uana wao" (Rum.8:15ku. Gal.4:6). Roho ni mlinzi wa imani ya kweli na arabuni ya mema ya baadaye.

"Arabuni" ni neno lililotumika katika biashara kwa sehemu ya malipo iliyotolewa mwanzoni ndipo baadaye mtu alilipa sehemu iliyobaki. Mfano mwingine ni wa pete iliyotolewa na kupokelewa wakati wa kuposana ishara ya kufunga ndoa baadaye.

"ili kuleta ukombozi wa milki yake" maneno hayo yahusu matazamio ya mbeleni, wakati Mungu atakapojichukulia kabisa vyote vilivyo Wake, wakati wa kujumlisha vitu vyote.

1:15-23 <u>Maombi kwa kujaliwa ujuzi wa kiroho</u>

Baada ya sifa kuu kwa baraka za Mungu, Paulo aliwageukia wale wa kuandikiwa na kumshukuru Mungu kwa ajili yao pamoja na kuwaombea. Alianza "kwa sababu hiyo" ni maneno ya kuonyesha kwamba msingi wa shukrani na maombi yake ni katika zile baraka alizozitaja hapo nyuma.

Maneno "nilipopata habari za imani yenu" (Kol.1:6-8) Je! alikuwa ameletewa riporti juu yao? Tukikumbuka kwamba Paulo alifanya kazi pale Efeso kwa miaka mitatu ni vigumu kuona kwa nini aseme "nilipopata habari za imani yenu" kana kwamba hakuzijua. Ndiyo sababu wataalamu wengine huwaza kwamba Waraka huo uliandikwa, si kwa Efeso tu, bali kwa Efeso na makanisa mengine ya eneo lile. Iliyo wazi ni kwamba ni watu fulani hasa walioandikiwa kwa sababu alimshukuru Mungu kwa ajili yao na kuwaombea. Alitaja imani yao na upendo wao kwa waumini wenzao. Waliuonyesha ukweli wa imani yao katika kushirikiana vema na wengine.

Ilikuwa tabia ya Paulo kudumu katika maombi kwa ajili ya waumini katika makanisa, pia alimshukuru Mungu kwa ajili yao, hata ikiwa walikuwa na shida au matatizo. (1 The.5:17; Rum.12:12; Kol.4:2; 3:15-17; Efe.5:19ku. Flp.4:6). Tena alipowaombea alitaja mambo yaliyowahusu, hakuomba kwa jumla au kama hewani tu.

k.17 Alimwomba nani? Jibu ni “Mungu wa Bwana wetu Yesu Kristo na Baba wa utukufu” yaani Mungu ambaye Yesu alimfunua. “Baba wa utukufu” ni maneno ya kutukumbusha uwezo na ukuu Wake unaodhihirishwa katika uumbaji na uhifadhi wa viumbe vyote na zaidi sana katika Ukombozi. Tunapomkaribia Mungu katika maombi ni msaada mkubwa kumwaza kwa jinsi Paulo alivyomwaza, hivyo tutamcha na kuamini kabisa kwamba atajibu maombi yetu.

Aliomba waumini wapate nini? .Kwanza, alitaka “wawe na roho ya hekima na ufunuo katika kumjua Mungu”. Wajaliwe na Roho utambuzi wa baraka walizo nazo kwa njia ya Injili, kwa kuwa wakizitambua hizo vizuri watazidi kuzistaajabia na katika kushirikiana na Mungu watazidi kuuonja uzuri wao.(Yn.17:3; Flp.3:10).
k.18 Ndipo aliomba watiwe nuru ili wafahamu mambo matatu. Kukua kwao kiroho na kukua katika utakatifu kumefungamana na kukua kwao katika kumjua Mungu. Kristo kwa Kuja kwake alileta mwanga mkubwa unaowaangaza watu ndani ya mioyo yao na mwanga huo huwasaidia watu kuona vizuri ndani kwa macho ya kiroho, mfano wa kipofu kurudishiwa uwezo wa kuona kimwili (Mt.4:16; Yn.1:0; 8:12; 2 Kor.4:6).

Kwanza, wameitwa na Mungu kuja kwenye nuru (Rum.8:28) na wito huo huleta tumaini la uzima wa milele. Pili, nuru hiyo yawawezesha kuufahamu na kuutambua urithi wao, jinsi ulivyo wa thamani mno, utajiri wa hali ya juu (1 Pet.1:4ku), Hasa jambo litakalowasaidia ni ushirikiano wa waumini wao kwa wao, maana urithi ni wa wote si wa mtu mmoja mmoja, wala si wa wachache tu. la! Hivyo, wajengane.

Tatu, kwa nuru hiyo wapate kujua ukubwa wa uwezo wa Mungu katika maisha yao, maana ni uwezo uleule uliomfufua Kristo atoke kwa wafu na kuwa hai milele. Ni uwezo uleule uliompaza Kristo juu kabisa na kuviweka vitu vyote chini yake. Ni uwezo unaofanya kazi “utendaji wa nguvu za uweza wake”. Kumbe! ajabu ni kwamba sisi nasi twaushiriki uwezo uleule wa ufufuo. Kwa uwezo huo twahuishwa na kuonja maisha mapya, twaishinda dhambi na hatutawaliwi na hofu ya mauti.

k.21-22 Hapo Paulo amemtangaza Kristo kuwa Bwana juu ya yote - falme zote, mamlaka zote, nguvu zote, usultani na kila jina litajwalo, hata katika ulimwengu ujao. Kristo ni Mungu Mwana wa milele na baada ya kunyenyekezwa katika kufanyika mwanadamu hata akauawa, akapandishwa

juu (Efe.4:10; Flp.2:9-11). Mamlaka na enzi zote ni chini yake na zile zilizo kinyume chake zimevuliwa nguvu (Kol.2:15).

Katika Yeye sisi nasi twarudishiwa heshima ya "uana" nasi tutarithi pamoja naye (Rum.8:17; Ebr.2:5ku) Katika hali ya kuwa juu ya vitu vyote Kristo anao uhusiano wa kipekee na Kanisa ambalo limeelezwa kuwa Mwili Wake. Ajabu ni kwamba Kristo amewekwa juu ya vyote kwa ajili ya Kanisa. Uzuri ni kwamba Kanisa lina Kiongozi ambaye pia ni Kiongozi wa yote. Hilo ni faida kubwa kwa Kanisa na Kanisa laweza kuvishinda vipingamizi vyote kwa njia ya Kristo. Kristo alishinda kwa sababu alikuwa na mamlaka ya Mungu (Mt.8:9ku. 9:27; Yn.17:2) Ndipo aliwashirikisha wanafunzi wake mamlaka ileile kusudi wafanye kama Yeye alivyofanya (Mt.28:18-20; Mk.3:14; Yn.20: 21-23). Tukumbuke ya kuwa mamlaka hiyo ipo kwetu mradi tunafanya mapenzi yake.

k.23 Kusema Kanisa ni Mwili wa Kristo ni zaidi ya kusema ni ushirika wa wafuasi wake. Hasa ni mwungano wa Kristo na walio Wake, waumini ni viungo vyake, mfano wa mti na matawi (Yn.15:1ku). Uzima wa mti hupitia katika matawi, vivyo hivyo uzima wa Kristo hupitia katika watu wake. Ukamilifu wa Kanisa hutoka kwa Kristo. Kanisa ni chombo chake cha kuyatekeleza makusudi makuu ya Mungu. Linapaswa kumfunua Kristo kwa ukamilifu, kwa njia ya kila muumini kujazwa Roho na kuvitumia vipawa vyake kadiri alivyojaliwa, na kujitoa kabisa katika kufanya mapenzi ya Mungu.

2:1-10: <u>Kuhuishwa kutoka kwa "wafu"</u>

Katika sura ya I Paulo aliitaja nguvu ya Mungu iliyomfufua Kristo kutoka kwa wafu, naye aliomba kwamba waumini wajue nguvu iyohiyo maishani mwao kwa kadiri ileile (1:19).

k.1-3 "nanyi" ni WaMataifa na k.3. Wayahudi na watu wote. Shabaha ya kwanza ya Paulo ilikuwa kuweka wazi kabisa kwamba wote wamefanya dhambi na kuasi na kwa sababu hiyo wote huhitaji sana neema ya Mungu (Kol.1:21). Alisema "ninyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa na dhambi zenu". Wanadamu wote wameumbwa katika sura na mfano wa Mungu ili waishi kama watoto Wake, kwa kuufurahia ushirikiano mwema naye na kufanya yampendezayo. Kwa kutaja mauti ni wazi kwamba wanadamu wamepewa uhuru wa kumkubali Mungu au siyo. Ila walionywa sana kwamba wakimwasi Mungu, mauti itafuata (Mwa.2:17). Hiyo mauti ni ya namna gani? Ni mauti ya kimwili lakini si hiyo tu. Zaidi sana ni mauti ya kiroho iliyo nzito sana. Ni kuishi nje ya uzima wa Mungu kwa sababu ya kukosa ushirikiano naye. Mauti hiyo yagusa maisha ya sasa pamoja na maisha ya baadaye. Bila kushirikiana na Mungu hamna maendeleo yoyote kiroho. Bila uzima mpya kutoka kwa Mungu hamna kitu chochote cha kuleta msaada (Eze.37:1-14; Rum.6:23; 7:10, 24; Kol.2:13; Efe.4:18; Yn.3:3, 5:24).

Paulo alitaja “makosa” na “dhambi”. Maneno hayo yafafanua shida yetu ambayo ni kutokulifikia lengo litupasalo. Hata ikiwa mtu hafanyi dhambi kubwa, hata hivyo, akosa kutimiza alivyotazamiwa. Tena hali nyingine ya wanadamu ni kuteleza na kwenda kando ya njia iliyo sawa. Pia ni uasi, ni kukataa mapenzi ya Mungu na amri zake. Kwanza ni katika kufanya kinyume chake kuhusu maadili na pili ni kuukataa mpango wa Mungu kwa maisha.

Kwa hiyo Paulo amejumlisha matokeo ya hayo kwa maneno “mlikuwa wafu”. Hali hiyo ni hali halisi kiroho ya kila mtu. Wala hamna tumaini lolote nje ya mwujiza wa Mungu kwa sababu mtu mfu hawezi kamwe kufanya lolote ili aishi. Ni vema kushika kabisa kwamba kila mtu aliye nje ya Kristo ni mfu. Jambo hilo si hali ya wapagani tu, wala ya watu wasiostaarabika, wala ya watu wanaoishi kwa mapokeo yao ya mababa zao. La! hali hiyo ni ya kila mtu, wa kila rika, wa kila kabila, wa kila mahali, na wa kila wakati. Fundisho hilo lapatana na sura tatu za kwanza za Waraka kwa Warumi.
Neno “wafu” laweza kutumika kama neno la usemi kama lilivyo katika Mfano wa Mwana Mpotevu (Lk.15:32) “kwa kuwa huyo ndugu yako alikuwa amekufa naye amefufuka....” Lakini Paulo amelitumia kueleza hali ya kweli. “Ufu” huonekana katika watu kutokumwona Kristo kuwa wa maana au utukufu. Huonekana katika watu kutokusikia sauti ya Roho Mtakatifu. Katika watu kutokuutambua upendo wa Mungu na Kuwako Kwake. Pia hawana hamu ya kushirikiana na watu wa Mungu. Twaweza kusema kwamba hawana itikio lolote sawa na maiti isiyosikia wala kuitika.

Ndipo Paulo alitaja mambo matatu yanayogusa na kutawala maisha ya “wafu katika dhambi”. Kwanza ni “kawaida ya ulimwengu huu” maana yake mipango ya maisha ya hapo duniani uliopangwa bila kumjali Mungu au sheria zake. Wanadamu huishi bila kumjali Mungu kama Yeye hayupo. Kilicho cha thamani machoni mwao ni tofauti na kilicho cha thamani machoni mwa Mungu. Kwao fedha, vyeo, vitu n.k. ni vya thamani sana na kutafutwa sana. Kwa Mungu hasa kitu kikubwa ni tabia ya mtu (1 Yoh.2:15-17).

Ndipo Paulo alitaja “kumfuata mfalme wa uwezo wa anga” ambaye ni Shetani, yule mwasi mkubwa na mpinzani mkuu wa Mungu. Daima huyo hufanya kazi kwa nguvu akijitahidi kushawishi watu kuenenda kinyume cha Mungu. Paulo aliongeza kwa kusema “roho yule atendaye kazi sasa katika wana wa uasi” Shetani ni mkuu wa ulimwengu huu na mtawala wa enzi zote zinazowapotosha watu. Wanadamu, ama twatiwa nguvu na Mungu na kufanya yampendezayo au twajitia chini ya nguvu iliyo kinyume cha Mungu na kujiamuria wenyewe (Lk.22:3; Yn.13:2,27 Mdo 5:4; Lk.11:24-26).

Katika kifungu cha 3 Paulo aliingiza Wayahudi na watu wote. Si WaMataifa tu walio wafu katika dhambi. Pia alitaja hali nyingine ya “wafu katika dhambi” nayo ni kuzitimiza tamaa za mwili na nia, yaani kiburi na kujiona, watu hubuni mawazo yasiyolingana na kweli za Mungu.

Nyuma ya hali hizo zote ni Shetani. Hata hivyo, haiwezekani kumlaumu Shetani moja kwa moja, kwa sababu wanadamu hukubali kwa hiari kushawishiwa naye. Paulo alitumia lugha ya ajabu katika kueleza wanadamu kuwa “wana wa uasi” na “kwa tabia yetu watoto wa hasira”. Maana yake nini? Kwanza tujue kwamba “hasira” ya Mungu haifanani na hasira yetu. Haina chuki wala kijicho wala kisasa. Hasa ni itikio lake la daima kwa uovu nayo inatokana na ukamilifu wa haki yake. Haibadili au kuupunguza upendo wake. Tazama k.4 kinachotaja upendo chafuata k.3. Hasira hiyo inayohukumu ina hali ya kibinafsi sawa na neema yake inayookoa kuwa ya kibinafsi. Maneno “kwa tabia” (hali yetu ya nyuma) yalinganishwe na maneno “kwa neema” (hali yetu ya sasa baada ya kuhuishwa na Mungu). Katika Warumi 5:12-14 Paulo alionyesha asili ya hali yetu ni kwamba tulifanya dhambi katika Adamu na pamoja naye. Kwa hiyo tumerithi dhambi na hatia na hukumu ya mauti katika Adamu na pamoja naye. Ila si wazi kwamba ndiyo maana yake hapo.

k.4 Katika vifungu vilivyotangulia Paulo ameonyesha hali mbaya kabisa na shida kubwa ya wanadamu wote. “tulikuwa wafu katika dhambi” tulikuwa chini ya hukumu ya Mungu kwa sababu ya dhambi zetu. “lakini Mungu” - maneno hayo Paulo ametumia ili atilie mkazo mabadiliko makubwa ambaye yametokea kutokana na Mungu kujiingiza. Katika sehemu hiyo twaona jinsi tulivyo kwa asili na jinsi tulivyo kwa neema. Kwani Mungu alijiingiza? Kwanza kabisa ni kwa sababu ya upendo wake na rehema zake. Alipoangalia hali yetu mbaya na jinsi tusivyoweza kufanya lolote, maana mfu hawezi kufanya lolote, basi, kwa wingi wa rehemu zake na mapenzi yake makuu, Mungu hakuweza kukubali wanadamu wapotee. Ajabu ni kwamba Yeye hakuudhika na hali yetu kiasi cha kusema “basi” “shauri lao” la! Wala hakukata tamaa. Kwa njia ya Yesu Kristo, iwapo tulikuwa “wafu” (Wayahudi kwa WaMataifa) alituhuisha pamoja na Kristo. (Yn.3:16; 1 Yoh.4:9 Rum.5:6,8; 2 Tim.1:10) Lilikuwa tendo la neema, tendo tusilolistahili hata kidogo. Kristo alikufa Msalabani hali akizibeba dhambi zetu kusudi akiondoe kile kiambaza kilicholetwa kati yetu na Mungu kwa sababu ya dhambi zetu. Katika Kufufuka Kwake aliishinda mauti ya kimwili na kiroho. Tokeo lake ni kwamba Uzima mpya hupatikana baada ya dhambi kusamehewa (Kol.2:13). Kwa sababu Kristo alifufuka kutoka kwa wafu, watu hufufuliwa kutoka “ufu” wa dhambi na kupata uzima mpya katika Kristo na pamoja naye (Rum.6:4-8; 8:11; 2 Kor.4:14). Huu ndio wokovu. Paulo amesema “mmeokolewa kwa neema” (k.5, 8) Daima Paulo alikaza neno la “neema”. Mungu kwa hiari yake Mwenyewe alitufanyia kwa hisani kubwa bila sisi kuistahili. “mmeokolewa” ni neno linaloonyesha kwamba hilo limekwisha kufanyika kwa upande wa hukumu ya dhambi, hatumo tena chini ya adhabu yake.

k.6 Ndipo Paulo ametaja mambo mawili yanayofuata “kuhuishwa pamoja na Kristo” (k.5) nayo “ni kupandishwa pamoja na Kristo” (k.6a) na “kuketishwa pamoja naye katika ulimwengu wa roho” (k.6b) (1:20). Kwa hiyo tumeunganika na Kristo katika hatua kubwa za maisha yake. Baada ya Kufa pamoja naye,

tumefufuka pamoja naye; na baada ya Kufufuka pamoja naye tumepaa pamoja naye na kuketishwa mkono wa kuume wa Mungu.

Jambo la kulistaajabia ni kwamba katika vifungu hivyo Paulo hasemi juu ya Kristo, bali juu yetu. Anathibitisha ya kuwa Mungu alituhuisha sisi na kutufufua sisi na kuketisha sisi (1:3) Kama Paulo alivyosema katika Flp.3:10 “uraia wetu ni uko mbinguni”. Hivyo tunayo maisha mapya na ushindi mpya. Kweli tulikuwa “wafu” ila sasa tumekuwa “hai”; tulikuwa “watumwa” sasa “tunatawala” katika “ulimwengu wa roho”. Kwa hiyo waumini wote hushiriki yote sawa na Kristo. Maana Paul hasemi kwamba “watafufuliwa”, kwa sababu kwa kuungana na Kristo wamekwisha kufufuliwa pamoja naye. Bila shaka mbeleni yatakuwepo matimizo ya hayo yote. Tunapofikiri hayo twaona ni mabadiliko ya ajabu, na tukitafuta asili ya mabadiliko hayo twakuta ni “mwingi wa rehema zake” (k4a) ni “makuu ya mapenzi yake” (k.4b) ni “neema yake” (k.5,8) na “ni wema wake” (k.7).

k.7 Katika 1:19-20 Paulo aliposema juu ya Kufufuka na Kupandishwa kwa Kristo alisema kwamba hayo yalionyesha uwezo mkuu na nguvu zake Mungu. Hapo anapotaja kufufuka na kupandishwa kwetu amesema hayo yanaonyesha “wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi”. Wema huo wa Mungu utaendelea na kuzidi kuudhihirishwa kwa njia ya Kanisa (3:10). Twatoa ushuhuda mkali kwa pendo lake na rehema zake tunapoishi maisha mapya.

k.8-10 Katika sehemu hiyo Paulo amerudia neno la k.5 akilipanua na kulieleza. Je! ni kwa njia gani mtu aweza kupata maisha ya mbinguni anapokuwa angali hapo duniani wakati huo. Ni kwa sababu ya neema, “tumeokolewa kwa neema” ni kazi ya Mungu peke yake, kwa sababu ya upendo wake kwetu. Sisi twaipokea “kwa imani” (Rum.3:22,25 Gal.2:16; 1 Pet.1:25). Mtu husikia haja ya msaada, hali ametambua udhaifu na utupu wake, ndipo humgeukia Mungu na kumpokea Kristo na msaada wake (Yn.1:12).

k.8b Paulo aliweka nje wazo lolote la wanadamu kuupata wokovu kwa jitahada zao wenyewe “ambayo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu”. Na mkazo huo unaendelea katika k.9 “wala si kwa matendo”. Wanadamu huzoea kufikiri kwamba wanaweza kuchanga kitu fulani kwa wokovu, ama wema wao, au matendo yao mema, au kufikiri kwamba maisha yao yalivyo yamridhisha Mungu. Ni kiburi kufikiri hivyo. Paulo amekwisha kusema kwamba wanadamu wote ni wenye dhambi, na kwa sababu hiyo wametengwa na Mungu, wala hawana ushirikiano mwema wao kwa wao, wala uhusiano mwema na Mungu, mpaka wamemkubali Kristo. Mungu hakubali kwamba kuna neno lolote au hali yoyote ya upande wetu wala nafasi yoyote ya kujisifu mbele zake. Njia ya wokovu iliyofanywa na Mungu imekomesha kiburi cha kibinadamu.

k.10 “tu kazi yake” “tuliumbwa katika Yesu Kristo”. Kazi ya Mungu ni kutuumba kwa upya. Uumbaji ni kazi yake tu, na huo uumbaji wetu mpya, ambao ni

wokovu, vivyo hivyo ni kazi Yake. (2 Kor.5:17; Efe.4:24; Gal.6:15; Kol.3.10). Mungu amefanya kazi hiyo kwa njia ya Yesu Kristo.

Hata hivyo, lengo la sisi kufanywa viumbe vipya ni kutenda matendo mema, kwa sababu aliyetuumba ni Mungu wa haki na utakatifu (4:24; 1:4). Maneno "tuenende nayo" yaonyesha ya kuwa mazoea yetu yatakuwa kufanya mema, tutaendelea kutenda matendo mema kama kawaida yetu kutokana na uumbaji wetu mpya.

2:11-22 <u>Upatanisho wa Wayahudi na WaMataifa</u>

Makusudi ya kazi ya Kristo katika wokovu yalikuwa zaidi ya wokovu wa mtu mmoja mmoja. Yalikuwa kuwaunganisha waumini wa Kiyahudi na waumini wa KiMataifa ili wawe kitu kimoja katika Yeye. Hali wamepatanishwa na Mungu kwa njia ya Kristo vivyo hivyo wamepatanishwa wao kwa wao kusudi awepo "mtu mmoja" tu (si wawili walioshirikiana vizuri tu). Ubinadamu mpya umeumbwa na Mungu. Neno hilo ni kubwa mno, maana hapo nyuma ukuta mrefu, mpana, uliwatenga Wayahudi na WaMataifa, wala tusiusahau ule mtengano mkubwa kati ya wanadamu na Mungu kwa sababu ya dhambi. WaMataifa ni wote wasio Wayahudi.

k.11-12 Kwa hiyo Paulo alianza kwa kuwaita WaMataifa wakumbuke hali yao kabla ya Kuja kwa Kristo. Walidharauliwa mno na Wayahudi waliowaita "wasiotahariwa" maana yake watu wasio na ile alama ya Agano la Mungu. Lakini hali yao ya kweli ilizidi ile iliyowazwa na Wayahudi. Paulo alisema kwamba wakati ule walikuwa "hamna Kristo". Kabla ya Kuja kwa Kristo Wayahudi walikuwa na ahadi na tumaini la kumpata Masihi, nao wakamtarajia sana. Paulo aliongeza kwa kusema "mmefarakana na jamii ya Israeli" walikuwa wageni waliokuwa nje ya maagano na ahadi za Mungu walizopewa Waisraeli. Waliishi mbali na baraka hizo. Kwa sababu walikosa matumaini maisha yao yalikosa maana na lengo. Maana ya kusema "hamna Mungu duniani" ni kusema kwamba hawakuwa na ujuzi wa kweli juu ya Mungu. Kweli, walikuwa na miungi mingi, nao waliziabudu sanamu za miungu, lakini miungu hiyo haikuwa na uhai, ilikuwa ya majina tu, katika mawazo ya watu. Hawakuwa la kufanya isipokuwa kukabili shida na matatizo ya maisha bila msaada wowote
(1 Kor.8:4ku. Gal.4:8).

k.13 "lakini sasa" ni maneno yanayoonyesha jinsi hali yao ilivyobadilika kabisa Kristo alipokuja. Badiliko kubwa la kwanza lilikuwa "kuwa na Kristo" na kwa sababu walikuwa na Kristo walikuwa "wameletwa karibu" kwa sababu ya Upatanisho uliofanyika katika Kifo Chake. Hayo yalikuwa tofauti sana na hali yao ya nyuma.

k.14 Halafu, baada ya kuletwa karibu waliunganishwa na Wayahudi na hao watu wawili tofauti walifanywa kuwa "mtu mmoja" (si wawili walioshirikiana vizuri) katika Kristo. Hivyo uadui na ukuta uliowatenga ulibomolewa, na tangu

hapo hakuna wa kumtangulia mwenzake au kuhesabiwa bora kuliko mwenzake, la. Iliwapasa wote wampokee Kristo na wokovu wake hata na wale waliokuwa na ahadi na maagano. Wote walikuwa wenye dhambi, na wote walihuishwa katika Kristo. Kristo ni “amani” ya wote, maana ndiye Yeye aliyefanya amani.

k.15-16 Paulo alitaja sheria kuwa “adui” kwa sababu kwa njia ya sheria dhambi ilipata nafasi, kwa kuwa hakuna mtu yeyote awezaye kuyatimiza maagizo ya sheria na kupata ile Haki kamili ya Mungu. Ni Yesu tu, kwa njia mbili, amefaulu kutupatia hiyo haki. Kwanza, alistahili kwa sababu ya maisha yake makamilifu, na pili, kwa Kifo chake cha kuifidia dhambi alipozibeba dhambi, hukumu, na laana za watu. Katika kufanya hivyo ameiondoa Torati kuwa njia ya kuipata haki. Mambo hayo Paulo alizungumza kwa kirefu katika Waraka kwa Warumi (sura ya 7) na katika Waraka kwa Wagalatia (Gal.3:13; Kol.2:14).

k.17-18 Kwa hiyo Myahudi ataokolewa kwa neema sawa na Mmataifa. Njia ya kumkaribia Mungu ni mmoja tu (Yn.10: 7, 9, 14:6) Mpatanishi ni mmoja tu. Amani ni kwa wale waliokuwa mbali na kwa wale waliokuwa karibu.

k.19 Paulo alitumia mfano wa nyumba kuonyesha kwamba wageni wamekuwa wenyeji, wote wa familia moja, wote wa jamii mpya. Mungu kwa njia ya Kristo ameunda Jamii Mpya ya wanadamu.

k.20 Pia Paulo alitumia mfano wa jengo. Kristo ni jiwe kuu kwa kuwa katika Yeye wote hushikana. Jengo linaendelea kukua kwa sababu umoja bado haujakamilika, bado tunahitaji msaada wa Roho kutusaidia kuwa na umoja wa kweli. Roho anaishi ndani ya Mkristo mmoja mmoja, pia anaishi ndani ya Jamii ya Wakristo, ndani ya Hekalu, maana kazi yetu ni kumwabudu Mungu. (1 Kor.3:16; 6:19; 2 Kor.6:16) Roho ni Mmoja afanyaye kazi maishani mwa Myahudi na maishani mwa Mmataifa (Rum.8:15ku. Gal.4:6).

3:1-13 Heshima ya kuwa watangazaji wa upatanisho huo

Katika sura ya kwanza Paulo aliwaza sana utajiri wa baraka nyingi zipatikanazo katika Kristo. Alizistaajabia, na mwishowe hakuwa la kufanya isipokuwa kumshukuru Mungu kwa ajili ya waumini wa Efeso, na kuomba kwamba hao wajaliwe kuzitambua baraka walizo nazo katika Kristo. Pia wajue utajiri wa urithi wao, na kuuonja maishani mwao uwezo mkubwa wa Mungu, uleule ambao Mungu alioutumia alipomfufua Kristo kutoka kwa wafu. Wajue hakika kwamba Kristo amepandishwa juu kabisa na kupewa mamlaka kuu juu ya enzi zote, na amewekwa hivyo kwa ajili ya Kanisa, ili awakamilishe waumini kama Yeye naye alivyokamilishwa. (Ebr.5:7-9).

Ndipo katika sura ya pili Paulo alipanua zaidi maelezo juu ya makusudi makuu ya Mungu ya kuvijumlisha vitu vyote katika Kristo (1:10). Alisema juu ya

neema ya ajabu ya Mungu katika kuwahuisha “wafu katika dhambi” akionyesha kwamba njia ya kuokolewa ni moja kwa Wayahudi na kwa WaMataifa. Ni njia ya neema, potelea mbali mtu awe Myahudi au Mmataifa akimwamini Kristo ataokolewa. Halafu alionyesha kwamba hilo ni tukio kubwa na hatua kubwa katika Mungu kuyatekeleza makusudi yake ya kuvijumlisha yote katika Kristo. Amewafanya Wayahudi na WaMataifa kuwa “mtu mmoja” kwa sababu ya upatanisho alioufanya Kristo Msalabani alipokufa kwa dhambi za wote. Labda kwa sisi siku hizo jambo hilo halionekani ni kubwa, kama lilivyokuwa wakati ule. Siku zile wanadamu waligawiwa Wayahudi na Wasio Wayahudi na ukuta mkubwa uliwatenga wasishirikiane. Kwa kubomelewa kwa ukuta ule mkubwa kuta nyingine zote pia hazina nguvu za kuwatenga wanadamu kwa njia yoyote. Katika Kristo tofauti zote zimeondolewa (Gal.3:28) Iliyopo ni kwa tofauti hizo kuzidi kutoweka ili tusitawaliwe wala kuongozwa nazo. Hatuna budi kufanya kazi ili neno hilo litumie.

3:1ku Katika mwanga wa hayo yote Paulo alianza sura ya tatu kwa maneno “kwa sababu hiyo”. Aliona ya kuwa amefungwa kwa sababu ya huduma yake kati ya WaMataifa. Alikamatwa alipokuwa Yerusalemu, akafungwa pale, halafu akapelekwa Kaisaria na kufungwa tena kwa miaka miwili, kisha akapelekwa mpaka Rumi ili ahukumiwe na Kaisari. Hayo yalitokea kwa sababu ya upinzani mkubwa wa Wayahudi (Mdo.21:17ku. 22: 21ku). Alisisitiza jinsi alivyopewa huduma yake na Mungu Mwenyewe hali alikuwa amefunuliwa na Mungu “siri” hiyo ya WaMataifa kuokolewa kwa neema na kupokelewa katika Kristo sawa na Wayahudi.

k.2 na k.7 Alikaza ya kuwa ni “neema ya Mungu” iliyomjalia huduma yake kwa WaMataifa. Kwanza “kwa neema” alifunuliwa siri kuhusu WaMataifa, hakuigundua mwenyewe wala kuifahamu kwa akili zake mwenyewe. Na katika k.7 alirudia kusema juu ya “neema ya Mungu” katika kumwita, kumweka na kumwezesha kufanya huduma ya kuwatangazia WaMataifa Injili ya Kristo.

Alitumia neno “siri” mara tatu katika sehemu hiyo, k.3, 4, 9 Neno hilo, maana yake nini? Ni kweli fulani ambayo wanadamu hawakuijua wala kuifahamu mpaka Mungu amewafunua. Tusiwaze kwamba katika Ukristo ziko “siri” yaani kweli fulani ambazo ni kwa wachache tu. La! “siri” za Mungu ni kwa waumini wote.

Alisema ni “siri” maana hapo nyuma wanadamu hawakujua kwamba WaMataifa watakubalika na Mungu na kuwa “watu wa Mungu” sawa na “watu wa Mungu” wa zamani, yaani Wayahudi. Neno hilo limewezekana kwa sababu ya Kuja kwa Kristo na kwa Kifo chake cha Upatanisho. Kristo katika Kufa Kwake alifanya fidia ya dhambi za WaMataifa na za Wayahudi, hivyo aliwakomboa wote.

k.5 Siri hiyo si yeye peke yake aliyefunuliwa, mitume pia walifunuliwa, ndipo kwa njia yao waumini wote. Twakumbuka jinsi Mungu alivyomsaidia Petro kuielewa alipomtuma kwa Kornelio (Mdo.10:1ku).

k.6 Katika kifungu hicho ameweka wazi kabisa siri kuwa nini hasa. Lakini, Je! neno hilo halikujulikana wakati wa Agano la Kale? Kwa sehemu ilionekana. Mungu alisema kwa Ibrahamu “katika wewe jamii zote za dunia zitabarikiwa” (Mwa.12:1-3) Katika Zaburi ya 2:8 alisema Masihi atayapokea Wamataifa kuwa urithi wake; na katika Isa.42:6 alisema Israeli litakuwa mwanga kwa WaMataifa. Yesu alipokuja alionyesha nia ya kuwapokea WaMataifa. Neno ambalo lilikuwa jipya ni katika Wayahudi kutohesabiwa tena “Taifa la Mungu” na Kanisa “taifa jiypa, jamii mpya, Watu wa Mungu” kuwekwa mahali pake. Kanisa ni wazi kwa mtu yeyote, wa mahali popote, wa rika lolote, wa hali yoyote, wa ustaarabu wowote. Wa kuingia ni wale wote wampokeao Kristo na upatanisho wake kwa dhambi zao.

k.7 Kama ambavyo tumeona mara nyingi katika Nyaraka zake Paulo alikaza ya kuwa aliitwa na kuwekwa na Mungu, tena si kwa kustahili kwake, wala kwa uzuri wake, bali kwa sababu ya neema ya Mungu; Mungu alitaka awe Mtume, basi akawa Mtume. Mungu alikuwa amefanya kazi kubwa sana maishani mwake, alimbadili kutoka kuwa Farasayo mwenye kujaa kiburi kingi cha kuwa Myahudi, mpaka alivua “Uyahudi” wake na kumvaa Kristo na kuwa mtumishi mnyenyekevu kwa ajili ya WaMataifa. Aliona amewajibika, tena ilimlazimu awaendee na kuwahubiri WaMataifa mahali popote atakapowakuta. Alitaka watajirike kiroho na kimaisha kwa baraka za Kristo, wawe naye kama Bwana na Mwokozi wao. Kufanya hivyo kulisababisha agongane sana na Wayahudi, hata na baadhi ya Wayahudi walioamini, ambao walitaka WaMataifa walioamini watahiriwe. Wengine hawakutaka Kanisa lifungue milango yake wazi ili WaMataifa waingie bila tohara na bila desturi zozote za Kiyahudi, wengine walikwazwa.

k:7-8 Paulo alihesabu kwamba huduma aliyopewa ilikuwa ya heshima kubwa mno. Yeye mwenyewe alijiona kuwa “mdogo kuliko yeye aliye mdogo” katika waumini wote kwa sababu hapo nyuma alijitahidi kabisa kulifuta Kanisa na kuumaliza Ukristo. Alijua ni neema tu iliyomwokoa na neema ilizidi katika kumchagua na kumweka kuwa mtumishi. Alinyenyekezwa sana na neema hiyo. Unyenyekevu huo uliandamana na mwito wake, wala hakusita kuukuza mwito wake na kutumia mamlaka aliyopewa kwa kutimiza huduma yake.

k.8 Aliona imemlazimu kuwahubiri WaMataifa Injili na kuwajulisha habari za “utajiri wa Kristo usiopimika”. Utajiri ni zile baraka alizozitaja katika sura ya kwanza na ya pili. Kwa yeyote Injili ni Habari Njema ila kwa Wamataifa wakati ule Habari ilizidi kuwa Njema kwa kuwa walizoea kuhesbiwa mbali na Mungu na nje ya ahadi zake. Tena Habari Njema si kwa mtu mmoja mmoja tu kuokolewa bali ni kwa watu wengi kuingizwa katika Mpango Mzima wa Mungu

wa kuvijumlisha vitu vyote katika Kristo (1:10). Wao wamo ndani ya Mpango huo. Utajiri usiopimika ni lugha inayoeleza kwamba hamna mwisho katika baraka za Kristo, ni kama bahari inayokwenda chini, na chini, na chini, na kuendelea kwenda chini. Maneno hayo yanatupiga deni la kuwaambia wengine yale ambayo wenyewe tunayafahamu juu ya Mungu na Kristo. Tu mawakili wa kweli hizo. Budi tufahamu kwamba ujumbe wa Kristo ni ujumbe bora ambao utakuwa msaada na baraka kwa wengine.

k.9 Paulo aliona kazi yake ina hali ya kuwaangaza watu. Nje ya Kristo watu wamo gizani, hawana nuru ya ufahamu juu ya Mungu na makusudi yake. Haja yao ya kwanza ni kuufahamu wokovu wa neema, na haja ya pili ni kujua kwamba wokovu huo ni sawa kwa Wayahudi na kwa WaMataifa. na haja ya tatu ni kutambua kwamba Yeye aliyeviumba vitu vyote sasa anauumba “uumbaji mpya” na kwa uumbaji huo vitu vyote vitaletwa pamoja katika Kristo (1:10).

k.10 Tukio la kwanza ni katika kutokea kwa Kanisa na kukua kwake. Ndani yake watu wa aina zote hukutana hali wameokolewa na kuhuishwa na Kristo ili waishi maisha mapya. Kanisa linadhihirisha uwezo, neema, na hekima ya Mungu. Hamna mfano wake hapo duniani. Ni shirika la watu wa makabila na rangi mbalimbali, wa rika na elimu mbalimbali, wa ustaarabu mbalimbali, shirika la watu wenye nia na shabaha moja ya kumpenda na kumtumikia Kristo na kuishi bila ubaguzi. Ndani yake Mungu anazidi kufanya kazi ya kuwakamilisha walio wake ili wazidi kupendana na kufanya mapenzi yake. Watazamaji wa Kanisa ni malaika na enzi za “ulimwengu wa roho” ambazo hawakufunuliwa kikamilifu makusudi hayo ya Mungu, kwa hiyo wanazidi kujifunza kwa hayo wanayoona katika Kanisa (1 Pet.1:10-12). Twaona Mungu ametumia njia tatu za kujulisha watu Makusudi yake. Kwa Paulo na Mitume aliwafunua moja kwa moja (Mdo:10: Iku) Halafu watu walipata kuyafahamu kwa njia ya kuambiwa kwa midomo ya Paulo na wenzake na waumini wengine. Halafu malaika na enzi za juu wanajulishwa kwa kuona kielelezo cha utendaji wa Kanisa kutekeleza Makusudi ya Mungu katika maisha ya kila siku ya waumini. Ni kama duara, toka Mungu kwa Paulo na Mitume, toka Paulo na wenzake kwa watu; halafu kutoka watu yaani Kanisa kwa mamlaka na enzi zilizo juu.

k.11-12 Kanisa ni la maana sana katika utekelezaji wa Mpango Mzima wa Mungu, kwa sababu kwa njia yake Mungu anazidi kuunda jamii mpya katika Kristo. Kanisa ni jumuiya ya watu wanaoishi kwa kanuni za Kristo, kwa amani na upendo, bila kujali cheo wala hali ya mtu kimwili, na hasa ndani yake watu wanajifunza kuishi bila ubaguzi wa aina yoyote.

k.13 Paulo aliomba kwamba wasikate tamaa kwa ajili ya dhiki zake za kufungwa kwake. Tukitaka kuutekeleza Mpango wa Mungu kwa vyovyote tutakuta vipingamizi vingi na katika vita hiyo baadhi watateswa, kwa sababu ulimwengu ni kinyume cha shabaha ya Mungu ya kukusanya vitu vyote chini yake.

3:14-21 <u>Maombi</u>

Paulo alianza sura ya tatu na maneno “kwa sababu hiyo” pengine alikuwa tayari kurudia maombi yake ya 1:15ku. Lakini kabla ya kufanya hivi alisisitiza neno kubwa la WaMataifa kukubalika na Mungu sawa na Wayahudi. Tena aliikuza neema ya Mungu katika kumteua yeye na kumweka kuwa mtumishi wa Injili kwa ajili ya WaMataifa, na hali amefungwa wakati wa kuandika aliisifu neema ya Mungu iliyomwezesha kuitimiza huduma aliyopewa, iwapo alikuta vipingamizi vingi hasa kutoka Wayahudi wenzake.

Kwa sababu aliyafahamu mapenzi ya Mungu alikuwa na haki ya kuomba kufuatana na mapenzi hayo. Alianza maombi yake kwa maneno “nampigia Baba magoti”. Kwa kawaida Wayahudi walizoea kuomba hali wamesimama (Mt.6:5; Lk.18:11, 13). Kupiga magoti ilikuwa dalili ya shauku na bidii, unyenyekevu na utii. Sulemani alipiga magoti wakati wa hekalu kuwekwa wakfu (1 Waf.8:54) Stefano wakati wa kuuawa kwake (Mdo:7:60) Petro kwenye kitanda cha Dorkasi (Mdo.9:40) Paulo alipoaagana na Wakristo (Mdo.20:36; 21:5) na Bwana Yesu Mwenyewe alipoomba Gethsemani wakati wa dhiki kubwa ya kukaribia Kuuawa Kwake (Lk.22:41).

Paulo alikuwa amekwisha kumtaja Mungu kuwa “Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo” (1:2-3) na amekwisha kusema juu ya waumini wa Kiyahudi na KiMataifa kuwa katika familia moja ya Baba (2:18-19). Kwa hiyo Mungu ni Baba wa familia nzima ya waumini wote, walio hai na waliokufa.

k.16 Katika maombi twamkaribia Mungu kama Baba, na neno hilo linatutia moyo wa kusogea karibu naye kwa imani. Paulo alizidi kuwatumainisha kwa kuwaambia kwamba Mungu ni “Tajiri wa Utukufu” (1:7), Mungu ni mzuri sana anayetaka kutoa “kwa kadiri ya” Utajiri Wake, yaani kwa kulingana na (si kutoka kwa) Utajiri Wake, kwa sababu hamna mwisho wa Utajiri Wake. (Flp.4: 19). Hamna mpaka katika Kutoa Kwake.

Paulo aliwaombea mambo gani? Kwanza aliomba wapewe “nguvu” ili wafanywe imara, kusudi wawe na nguvu ya kusimama imara (1:19) ili waishi na kufanya kazi kwa ajili yake (1 Kor.16: 13; Flp.4:13). Agano Jipya linafundisha kwamba nguvu ya kuishi maisha ya Kikristo yatoka kwa Roho Mtakatifu akaaye ndani yetu (2 Kor.4:16) Roho hututia nguvu “ndani” katika moyo, na nia, na roho zetu, twabadilishwa kwa ndani ndipo mabadiliko hutokea na kuonekana katika maisha ya kila siku.

Halafu Paulo aliendelea kwa kuomba kwamba “Kristo akae mioyoni mwenu kwa imani” Kristo kukaa ndani na Roho kukaa ndani ni mamoja, Kristo anakaa ndani kwa njia ya Roho na Paulo hakuweka tofauti kati ya mambo hayo mawili (Rum.8:9ku. Yn.14:16-18). Neno “akae” laonyesha kwamba ukaaji wao ni wa kudumu, hawawi wageni wa kufika na kuondoka, bali huwa “wenyeji”. Kwa upande wa waumini imani inatakiwa, mtu ataka na amkaribie Kristo (Ufu.3:20).

Pamoja na nguvu ya kusimama twahitaji hekima na ufahamu wa namna ya kuishi.

k.18 Ndipo Paulo alitaja jambo la upendo. Upendo ndio kiini cha kumfahamu Mungu. Paulo hakutaka waumini wazitegemee akili zao katika kumfahamu Mungu bali wamfahamu kwa njia ya kuwa na shina na msingi katika upendo. Wakitia mizizi chini katika "udongo mzuri" wa upendo na wakijenga maisha juu ya msingi imara wa upendo, basi watazidi kukua katika kumjua Mungu. Ujuzi wa kweli wa Mungu haupatikani nje ya upendo. Bila upendo Roho hayupo. (1Kor.1:21-22; 8:1-3; Kol.2:18,23; 1 Tim.1:4; 6:4; Yn.7:17; 15:9. Waraka wa kwanza wa Yohana wasema sana juu ya neno hilo 1 (1 Yoh.2:9; 3:11-19; 4:8; 13-21).

Tena hali hiyo si kwa mtu mmoja mmoja binafsi tu, bali Paulo aliandika "mpate kufahamu pamoja na watakatifu wote". Tukumbuke jinsi ilivyokuwa wakati ule, waumini wa Kiyahudi na waumini wa KiMataifa walijitahidi kuwa na umoja na upendano tofauti na wakati wa nyuma walipokuwa adui, watu ambao hawakushirikiana hata kidogo.

Tena upendo huo hauna mpaka, tukienda juu sana au chini sana, tukienda mbele kiasi gani au nyuma kiasi gani, huo upendo bado ungalipo. Twaitwa kuishi maisha yote katika upendo.

k.19 Zaidi Paulo aliomba waujue upendo wa Kristo ulio mwingi sana, kiasi cha kuupita uwezo wao wa kuufahamu. Hapo nyuma alisema vivyo hivyo juu ya nguvu ya Mungu (1:19) na juu ya neema ya Mungu (2:7). Hawataufikia mwisho wa kujifunza upendo huo wa Kristo, wataendelea kuugundua milele na milele.

Paulo alifikia upeo wa maombi yake kwa kuomba kwamba waumini watimilike katika utimilifu wote wa Mungu. Ina maana kwamba iwapo wamejazwa Roho, hata hivyo, bado nafasi ipo kwa kukua. Ni kujazwa na Mungu Mwenyewe, si upendo wake au hekima yake tu, bali Mungu Mwenyewe awajaze, akae ndani yao kwa utimilifu (1:23; 4:13; 5:18; Yn.1:16; 1 Kor.8:1-3; 13:1-3).

k.20-21 Lakini, Je! maombi kwa mambo hayo, kweli yaweza kujibiwa kiasi cha waumini kutimilika na utimilifu wote wa Mungu? Jibu ni ndiyo, kwa sababu Paulo aliendelea kusema "atukuzwe Yeye awezaye" Awezaye nini? Mungu aweza kufanya kwa sababu Mungu ni Mungu wa kutenda sio wa kusema tu. Aweza kufanya nini? Aweza kufanya mambo ya ajabu mno kuliko..... Kwa nini aweza? Kwa sababu ya nguvu isiyo na mpaka, Mungu aweza kufanya yale yote anayokusudia kwa watu wake. Anafanya kazi ndani ya mtu binafsi na katika jumuiya ya watu wake. Mawazo yetu na maneno yetu yana mpaka ila nguvu ya Mungu haina mpaka.

Paulo alimaliza sehemu hiyo kwa wimbo wa sifa kwa Mungu. Twapaswa kumtukuza Mungu kwa sababu uwezo wote watoka Kwake, kwa hiyo ni haki sifa zote zirudi Kwake. Wala si jambo la mara moja, vizazi kwa vizazi huwajibika kumtukuza. Katika Kanisa atukuzwe kwa sababu nguvu Zake zadhihirika katika maisha ya Kanisa, ni chombo chake cha kuyatekeleza makusudi yake. “Katika Yesu Kristo” kwa sababu makusudi yake yote hutimizwa kwa njia ya Kristo.

4:1-6 <u>Kuudumisha Umoja</u>

Sura 3 za kwanza zilitoa mafundisho na sura 3 zinazofuata zinatoa maelezo jinsi mafundisho hayo yatakavyotekelezwa katika maisha ya kila siku, ili Mungu apate kutukuzwa katika Kanisa lake (3:21). (Ila tusifikiri kwamba hamna mafundisho katika sura hizo, yapo, lakini hasa maadili yamezidi).

k.1 Alianza kwa kuwaomba waishi maisha “yaliyoustahili wito wao” kama wafuasi wa Bwana Yesu. Alitia uzito kwa kujitaja kuwa “mfungwa katika Bwana”. Iwapo alifungwa minyororo, hata hivyo, maisha yake yalitawaliwa na Bwana - alikuwa “mfungwa katika Bwana”. Ni mfungwa kwa sababu ya upendo wake kwa Bwana na kwa uaminifu wake kwa Injili yake.

Hapo nyuma ameweka wazi mbele yao makusudi makuu ya Mungu kwa Watu Wake, kwa Kanisa, yaliyopata uwezekano wake katika Kristo. Ameomba wayajue na kuyatambua makusudi hayo kuwa ya ajabu sana, na pia, wajue kwa ujuzi wao wa kibinafsi upendo na uwezo wake na baraka zote walizo nazo katika Kristo.

Kwa hiyo aliendelea kwa kusema juu ya kuishi kwao mtu mmoja mmoja na katika sharika zao, kwa kuwa kusudi la Mungu ni kuunda jumuiya mpya ya wanadamu. Hayo si mafundisho tu, la, ni zaidi. Shabaha yake ni “kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo Yesu (Kol.1:28; Mdo.20:27, 31). Kwa hiyo maadili ya Kikristo hujengwa juu ya mafundisho ya Kikristo. Ni itikio la Mkristo kwa yote ambayo Kristo amefanya kwa ajili yake na kwa yote anayomfanyia ndani ya maisha yake. Tena ni njia ambayo kwayo hayo makusudi makubwa ya ajabu ya Mungu yatatimizwa. Mkristo huwajibika “kuenenda kama inavyoustahili wito wake”.

Neno “kuenenda” ni kuonyesha kwamba yanayozungumzwa ni maisha ya kila siku. “Wito” ni neno linalotumika sana katika Maandiko. Mungu amewachagua kuwa watoto wake (1:4, 5) kwa hiyo wapaswa waishi kama “watoto wa Baba yao wa mbinguni”. Mtu mmoja aishi kama “mtoto wa Baba” na Wakristo kwa pamoja waishi kama “watoto wa familia moja ya Mungu”. Wakati ule neno hilo liliwahusu waumini wa Kiyahudi na waumini wa KiMataifa. Wito ni kuwa na umoja na kuwa watakatifu, watu waliotofautiana na watu wa dunia, watu wa kuishi maisha safi.

k.2 Paulo ametaja tabia nne zitakazosaidia kuudumisha umoja wao. Kwanza ni unyenyekevu, na aliongeza kwa kusema unyenyekevu wote. Wakati ule Wayunani hawakuona unyenyekevu kuwa tabia ya sifa, waliuwaza kuwa hali ya kitumwa, hali ya unyonge, si vizuri mtu ajidhili, ni kama kuishi maisha ya upungufu. Lakini Kristo alipokuja, alikuwa mnyenyekevu sana, alikubali kutumika badala ya kutumikiwa, naye alijitoa hata kufa bila kujijali (Flp.2:5ku). Alitoa mfano wa “mtoto” kuwa kielelezo kwa wafuasi wake. Wafuasi wake wameitwa kuzifuata nyayo zake. Tangu hapo unyenyekevu umekuwa tabia ya sifa pia tabia impasayo kila Mkristo. Mkristo hunyenyekezwa anapokumbuka ukuu na utukufu na utakatifu wa Mungu wake. Kwa njia hiyo autambue udhaifu na unyonge wake na jinsi asivyozistahili baraka za Mungu. Unyenyekevu ni kinyume cha kiburi ambacho chaharibu uhusiano wa watu.

Tabia ya pili inayotajwa ni upole. Upole ni hali njema inayowasaidia watu kuishi pamoja vizuri. Ni kama mafuta katika mashini. Mtu mpole hajioni, wala hajiinui. Mpole aweza kujitawala, kwa sababu amekubali kutawaliwa na Kristo na kuongozwa naye. Yesu alisema “Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo....jitwike nira yangu, jifunze kwangu (Mt.11:28).

Tabia ya tatu ni uvumilivu. Mtu mvumilivu hawi mwepesi wa kukasirika, yu tayari kuvumilia mabaya. Yu tayari kusubiri, hafanyi haraka ya kujitafutia haki yake.

Tabia ya nne ni kuchukuliana katika upendo. Ni kuchukuliana na dhaifu za watu, ni kuendelea kumpenda jirani au rafiki iwapo amekosewa, au ikiwa hali yake haimpendezi. Bado angali akimfanyia kwa wema “katika upendo”. Mara nyingi katika Waraka Paulo ameutaja upendo, maana upendo ndio utakaowasaidia kuishi kwa sifa hizo nne. Tabia hizo ni lazima tukitaka kuudumisha umoja.

k.3-6 Neno “moja” limetumika mara 7 katika vifungu hivi. Lengo la kuishi kwa tabia hizo ni “kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani”. “Umoja wa Roho” ni maneno yanayoonyesha kwamba Umoja ni kipawa cha Mungu. Kwa Kifo chake msalabani Kristo alifanya amani (2:14) na Roho Mtakatifu hufanya kazi ndani ya waumini, mtu mmoja mmoja, na waumini kwa pamoja, na kuwafanya kuwa “Mwili wa Kristo”. Si umoja unaoundwa na wanadamu, ni umoja wa Roho, ni kipawa cha Mungu, ila ni wajibu wa waumini kuuhifadhi umoja huo, kuulinda katika mashambulio yote ya nje na ya ndani.

Paulo alitumia neno “kujitahidi” kuonyesha kwamba ni kazi muhimu kuuhifadhi umoja, ni kazi inayotaka uangalifu na bidii. Wakiishi kwa upendo, wataishi katika amani ya Kristo (Yn.16:33) na wakiishi katika amani ya Kristo watauhifadhi umoja wa Roho.

k.4 Paulo alifahamu kwamba ziko tofauti nyingi katika hao waumini. Wametoka mataifa na makabili mbalimbali, wametoka katika hali mbalimbali za maisha, ni wa marika mbalimbali, wa elimu mbalimbali, na wa ustaarabu mbalimbali. Sasa wamekutana katika Kanisa, Mwili wa Kristo, wameunganishwa na Kristo na kuunganishwa wao kwa wao. Mambo ya kiroho yaliwaleta pamoja na mambo hayo yana nguvu inayozidi na kuzishinda tofauti zao. Wameshirikishwa baraka za ajabu (1:13-14) na ukuta mkubwa uliowatenganisha umebomolewa katika Kristo. Hivyo wote hushiriki kwa usawa neema ya Kristo na kuzirithi pamoja ahadi zote za Kristo.

Paulo amejumlisha kwa kusema wao ni wa Mwili Mmoja, Mwili wa Kristo, viungo vya Mwili wake. Ni wa Roho mmoja (Rum.8:9) kwa sababu Roho ni mmoja anayekaa ndani yao na kuwapa uzima wa kiroho. Wote walikuwa na tumaini moja. Iwapo wametoka katika mazingara mbalimbali lengo lao ni moja, wote hutazamia Kurudi kwa Bwana wao Yesu Kristo na wote hutarajia kufika kwenye uzima wa milele (1:18; Rum.5:2; Kol.1:27).

k.5 Wanaye Bwana mmoja Yesu Kristo. Yeye ni kiongozi wa maisha, nao wamempa utiifu wao. Wakiwa waaminifu Kwake watashikana vizuri sana, wakimtumikia na kumheshimu.

Imani moja yaweza kumaanishwa kwamba kila mmoja amemwamini na kumtegemea Kristo, kila mmoja amemkaribia Mungu kwa njia moja ya Kristo, na kuishi kwa neema yake. Maana nyingine yaweza kuwa mafundisho ya Kikristo, yaani kweli za msingi kumhusu Mungu, Kristo, na Roho Mtakatifu, ukombozi wa Kristo na makusudi makuu ya Mungu.

Ubatizo mmoja. Tendo la nje la kumwingiza mtu katika Kanisa ni ubatizo. Kristo Mwenyewe aliuweka ubatizo kuwa mlango wa kuingia Kanisa, na Mitume waliagizwa kwenda kuihubiri Injili na kuwabatiza wale wote waliouitika wito wa kuamini. Kwa hiyo kila muumini amepita mlango mmoja wa ubatizo (Gal.3:27; 1 Kor.1:13) Si kitu walibatizwa na nani, si kitu walibatizwa katika kanisa au shirika au dhehebu gani, wote walibatizwa katika Jina la Yesu au Jina la Utatu, si katika jina la mtu au dhehebu fulani. Ni sakramenti au ibada ya umoja.

k.6 Mwishowe umoja ni wa Mungu mmoja, aliye Baba wa wote, juu ya yote, katika yote na ndani ya yote. Wote wameumbwa na Mungu, wote waichukua sura yake, na wote wamekombolewa na kurudishiwa “uana” wao katika Kristo. Wakristo ni wa familia moja ya Baba. Mungu ni mmoja, hamna miungu isipokuwa katika mawazo ya watu. Twaishi katika ulimwengu ulioumbwa na kuhifadhiwa na Mungu. Yeye yumo ndani ya Watu wake akifanya kazi kwa njia ya Roho Mtakatifu akituelekeza kufanya yale yote yatakayoyatekeleza makusudi yake makuu.

Ni wapi ambapo wanadamu waweza kuungana kwa namna hiyo isipokuwa katika Kanisa? Ni wapi ambapo wanadamu waweza kupata shabaha moja ya kuishi kwayo isipokuwa kutoka Mungu, Aliye Baba, Mwana, Roho ambaye tumewekwa katika Mwili wake.

Kama ni hivyo ni ujinga kwa Wakristo kugombana na kuachana kwa mambo madogomadogo. Ni vibaya kwa watu kuyafuata mapenzi yao bila kutafuta kuyafanya mapenzi ya Mungu kwa pamoja na kwa nia moja. Twaweza kusema ni dhambi kubwa kuyasababisha mafarakano katika Kanisa, Mwili wa Kristo (1 Kor.3:16-17).

4:7-16 <u>Utofauti katika Umoja</u>

Iwapo Wakristo wote hushiriki huo Umoja uliotajwa katika vifungo vilivyotangulia, hata hivyo, wao wenyewe huwa na tofauti katika vipawa na kazi zao katika Mwili wa Kristo.

k.7 Mungu katika hekima yake amekusudia ziwepo tofauti nyingi za vipawa na huduma. Hakupenda wote wafanane; neno la wote katika k.6 limebadilika kuwa “kila mtu” katika k.7. Tofauti zetu zinatufanya kutegemeana na kusaidiana na kujengana, maana hakuna aliye mkamilifu kiasi cha kutokuuhitaji msaada wa wenzake.

“kila mmoja wetu alipewa neema kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo”. Paulo ametumia neno la “neema” kueleza vipawa (3:2, 7, 8), ni neno linalomzuia mtu asijione na kuwa na kiburi. Tena “kila mtu amepewa” (1 Kor.4:7) mtu hastahili kuitwa kumtumikia Mungu wala hastahili kupewa uwezo wa kufanya kazi aliyoitiwa. Hakuna aliye na vipawa vyote, na hakuna asiye na kipawa chochote. Neno hilo ni kwa waumini wote si kwa viongozi na wahudumu tu.

Ni Bwana anayempa kila mtu fungu lake kufuatana na hekima yake na makusudi yake (Rum.12:3-8; 1 Kor.12:14).

Ipo neema “inayookoa” na neema hiyo waumini wote walipewa walipompokea Yesu kuwa Mwokozi wao. Pamoja na neema ya kuokoa ipo neema ya utumishi inayowawezesha waumini kutumika “kwa kadiri ya kipimo cha kipawa chake Kristo”.

k.8 Vipawa vyatoka kwa Kristo aliyeshinda na Kupaa juu kabisa, yuleyule aliyeshuka hapo duniani. Yeye aliwaahidi wafuasi wake kwamba watajaliwa uwezo wa kufanya sawa na Yeye hata kumzidi (Yn.14:12-14; 7:39; Mdo.2:33; Zab.68:18).

k.9-10 “mpaka pande za chini” maana yake nini? Huenda ni lugha ya kueleza Kushuka Kwake hapo duniani. Au pengine ni kusema juu ya jinsi alivyonyenyekezwa sana mpaka Kifo chake Msalabani (Flp.2:8).

Shabaha ya Paulo ilikuwa kufundisha kwamba mapenzi ya Kristo ni kujaza kila kitu na Kuwepo Kwake. Cha duniani na cha mbinguni. Yeye ni juu ya enzi zote za mahali popote, anayo mamlaka ya kila kitu, hamna mahali wala utaratibu ulio nje ya uwezekano wake wa kuugusa. Ndiyo sababu alishuka halafu akapaa. Kupaa kwa Kristo kuna maana kwamba licha ya ulimwengu kuwa bila Kristo (kwa Kuondoka Kwake) ulimwengu umemjaa kwa njia ya Roho (Yn.16:7).

Tena ni faraja kwa watu wake kujua kwamba yule wanayemwomba ni yuleyule aliyeshuka na kuishi kati ya wanadamu na kushiriki maisha yao, huzuni zao, majaribu yao na dhiki zao. Kwa sababu hiyo wanapomwomba wanajua kwamba Yeye anawafahamu kabisa kabisa na kujua wanavyojisikia nafsini mwao.

4.11 Paulo aliendelea katika kifungu hicho kutaja vipawa mbalimbali ambavyo Kristo ametoa kwa Kanisa. Vipawa ni wahudumu mbalimbali, hao huwa zawadi kwa Kanisa. Kanisa limepewa hao, si sawa na kuwekwa na Kanisa, maana yawezekana mtu amewekwa ambaye hana vipawa vya Roho kwa kazi yake. Paulo ametaja watu kufuatana na huduma yao na kazi yao, si cheo chao. Tena shabaha ni kwa Kanisa kujengwa si mtu ajifaidi mwenyewe. Ndiyo sababu Paulo ametaja watumishi wa aina tano bila shaka wapo zaidi ya hao ambao hao nao ni “vipawa kwa Kanisa”. Zipo orodha mbalimbali za “vipawa vya Roho” katika Agano Jipya na kila orodha hutofautiana na nyingine. Hii ya hapo inalingana kiasi fulani na 1 Kor.12:28.

Kwanza Paulo alitaja “mitume”. Katika Agano Jipya neno hilo limetumika kwa njia tatu:

i. Katika Flp.2:25 mtume ni mjumbe
ii. Limetumika kwa wale Thenashara, Mitume 12 waliofuatana na Bwana Yesu, hao ni wa kipekee (1 Kor.15:5; Ufu.21:14)
iii. Wachache wengine waliitwa mitume - Paulo na Barnaba (Mdo.14:14) Yakobo, ndugu yake Bwana Yesu (Gal.1:9) Sila (1: The.2:16) Yunia na Andronikо (Rum:1.16:7).

Twafikiri kwamba walikuwapo wengine ambao hatujui majina yao. (1 Kor.15:7). Katika 1 Kor.9:16ku. tumepewa mambo mawili ya sifa zilizotakiwa kwa mtume: (a) kumwona Yesu hai baada ya Kufufuka Kwake; (b) kutumwa naye. Thibitisho la mtu kuwa Mtume ni “ishara na maajabu...” (2 Kor.12:12). Hao walikuwa wale waliowekwa kama msingi wa Kanisa (Efe.2:20).
Halafu “manabii” walitajwa. Twajua katika Agano la Kale hao waliisikia sauti ya Mungu kipekee, walipewa ujumbe moja kwa moja kutoka kwa Mungu, nao waliutoa kwa kusema “Bwana asema hivi...”

Manabii wametajwa pamoja na Mitume kama watumishi waliowekwa kama msingi wa Kanisa (Efe.2:20; 3:5-6) Walitoa Neno kwa uvuvio wa Roho. Walikuwa muhimu katika siku za kwanza za Kanisa wakati Kanisa lilipokuwa changa. Walitoa habari za matukio mbalimbali (Mdo.11:28; 21, 9, 11). Walitoa neno lililogusa kwa nguvu dhamiri za watu (1 Kor.14:24). Walitoa mausia ya kuwatia moyo waumini na kuwaimarisha (Mdo.15:32).

Je! mitume na manabii wako mpaka leo? Kweli hamna mfano wa Mitume 12, wao walikuwa wa kipekee, hakuna waliorithi mahali pao. Hata manabii huenda hawapo kama wale wa zamani zile. Kitu kikubwa kwa upande wetu ni kuwa na Agano Jipya, ambalo ni Maandiko ya KiMitume. Kwa Agano Jipya twaweza kuyapima mambo na kujua yaliyo halali na ya kanuni kwa Kanisa.

Huenda wako watu wenye kipawa cha “unabii” ambao huduma yao ni kulisaidia Kanisa mahali walipo.

Wainjilisti: Filipo aliitwa Mwinjilisti (Mdo.21:8) Timotheo aliambiwa afanye kazi ya uinjilisti (2 Tim.4:5). Pengine ni wale waliosafiri huko na huko na kuihubiri Injili. Ni vema kuwaza kwamba walikuwa na kipawa cha kuhubiri Injili na kuieleza vizuri kiasi cha kuwasaidia wengi waifahamu na kuitika vema. Ni kama walikuwa na kipawa cha “uvutiko” wa kudaka usikivu wa watu na kuieleza Injili kinaganaga kiasi cha kufaulu kuleta wengi kwa Kristo. Siku hizi kuna uinjilisti wa aina nyingi - wa mtu mmoja mmoja - wa umati wa watu - wa kuyatumia maandishi - wa kutumia vyombo kama redio na televishoni na filamu n.k.

Halafu Paulo alitaja wachungaji na waalimu kwa pamoja. Je! alikuwa na maana kwamba hao ni mamoja au vipi? Huenda hao walihusika na shirika la palepale, wakiwa na kazi ya kuwachunga na kuwajenga waumini wa mahali pale. Mchungaji ni yule wa kutunza kundi lake. Ni kuwalisha na kuwalinda ili wasipatwe na madhara ya kiroho. Bwana Yesu alisema Yeye ni Mchungaji Mwema (Yn.10:11; 14) na Yeye Ndiye Mchungaji Mkuu (Ebr.13:20; 1 Pet.2:25; 5:2, 4).

Katika 1 Tim.3:2 na Tito 1:9 twaona ya kwamba kila mchungaji awe na maelekeo ya kufundisha. Huenda baadhi yao walikuwa na kipawa kwa upande wa kufundisha. Waalimu ni zawadi kwa Kanisa (Mdo.13:1; Rum.12:7; 1 Kor.12:28). Yawezekana wachungaji walihusika na maadili na marudi ya waumini, na kutoa sakramenti n.k.

Kanisa lahitaji sana waalimu wa kulifundisha Neno la Mungu. Siku hizi katika maeneo mengi watu wengi wamemwamini Kristo na ipo haja kubwa kwa hao watu kupewa mafundisho ili waimarike na kuthibitika katika imani yao.

k.12 Kwa nini Kanisa limepewa “vipawa” vya hao waliotajwa katika k.11? Paulo ametoa jibu katika kifungu hicho. Kazi yao ni “kuwakamilisha watakatifu”. Maana yake wajibu wao ni kuwaleta waumini wote katika hali njema, hali ifaayo, ili watumike. Watengenezwe vizuri, tayari kumtumikia Bwana, ndipo kwa njia ya hao wote huduma itendeke. Ina maana kwamba kila Mkristo ana kazi yake, kila mmoja ni kiungo cha Mwili wa Kristo, yaani Kanisa, na kila mmoja huwajibika kufanya kazi au jambo kwa ajili ya mwili mzima. Hivyo, huduma ni ya wote, na wale waliotajwa katika k.ll wamepewa huduma ya “utengenezaji” wa waumini ili wote watende huduma, si wachache tu walio na cheo au madaraka kanisani.

“hata Mwili wa Kristo ujengwe” Ndipo, kwa njia ya kila mtu kufanya yampasayo kufuatana na wito na kipawa chake, na kwa msaada wa wale walio na wajibu wa “utengenezaji” basi Mwili Mzima utakuwa na afya, utakua, utajengwa. Kwa hiyo lengo si kwa kila mmoja kukamilika mwenyewe tu, wala si kwa wachache kufanya huduma tu, bali ni kwa wote kushirikiana katika utumishi wa Bwana. Kweli mtu hawezi kuuhesabu mwili wake kuwa mzima kama mkono wake haufanyi kazi, wala hawezi kuhesabu amekua vizuri ikiwa kidole chake kimepungua au kimezidi vidole vingine. Afya yapatikana kwa kila kiungo kufanya kazi yake na kila kiungo kuwa na afya ndipo na mwili mzima utakua. Ndiyo sababu mafundisho ni muhimu, ili watu wapate kuelewa vizuri neno hilo.

4:13 Yale mambo matatu ya k.12 ni mambo yanayoendelea katika maisha ya Kanisa, ila Paulo, wakati wote, hakuweza kuwaza mambo kama hayo bila kutafakari juu ya shabaha au lengo lake. Neno “kufikia” limetumika mara 9 katika Kitabu cha Matendo ya Mitume kuhusu wasafiri kupafikia mahali walipokusudia kufikia. Neno pia limetumika katika Mdo.26:7 na Flp.3:11 kwa maana hiyo ya hapo.

Ni nini “mwisho” wa “safari” ya Kanisa? Kwanza ni “umoja wa Imani” ile iliyohubiriwa na kufundishwa iliwakusanya watu kutoka mazingira na hali mbalimbali, waumini walitoka dini na imani na elimu mbalimbali zisizo kweli, pamoja na wale ambao hawakuwa na dini. Na hao wote walipata kuelewa zaidi na zaidi “tumaini” lililo mbele yao, na kumtegemea “Bwana mmoja” katika maisha ya sasa hali wakizidi kutambua ya kuwa wameunganika katika “Mwili mmoja”. Lengo ni “umoja wa Imani” Pili, ni “kumfahamu sana Mwana wa Mungu”. Hiyo Imani siyo ya akili tu, kama jumla ya masharti fulani au kanuni fulani, la, ni zaidi. Ni neno la moyo na la binafsi. Hatuwezi kumjua mtu kwa akili peke yake, vivyo hivyo na Mwana wa Mungu. Ili tumjue twahitaji kushirikiana naye kibinafsi. Imani yetu ni katika Mwana wa Mungu. Paulo alitumia Jina hilo mara chache tu (Rum.1:4; Gal.2:20; 1 The.1:10) Aliposema juu ya uhusiano wa Bwana na Kanisa lake alitumia Jina la Kristo na aliposema juu ya uhusiano wake na mtu alimwita “Mwana wa Mungu”.

Paulo aliendelea kwa kuonyesha kwamba iliyopo ni kwa waumini kuwa na ujuzi wa kibinafsi, wakiishi maisha yao “katika Kristo” ili wakue mpaka wawe “mtu mkamilifu hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo”. Lugha hiyo yote husema juu ya utimilifu, ukamilifu, ina maana ya kupevuka, kukomaa (1Kor.2:6; 14:20; Ebr.5:14) Mtu mkamilifu ni sawa na mtu mzima (1Kor.13:11). Kukomaa kwaleta “umoja” umoja wa wengi kufanywa kuwa “mtu mmoja” (2:15).

“cheo cha kimo” lasema juu ya kukua na kukomaa. Upeo wa kimo ni “utimilifu wa Kristo” (1:23) yaani ni kila Mkristo kujazwa na baraka na vipawa na neema ya Kristo. Kama tutafaulu kulitimiza lengo hilo katika ulimwengi si kitu, ila neno kubwa ni kwa kila Mkristo na Wakristo wote kwa pamoja kusonga mbele ili waendelee kukua kiroho na katika ufahamu wao wa Kristo na katika umoja wao.

k.14 Kwa sababu hiyo wasiwe “watoto wachanga” wasioweza kusimama imara wakiyumbishwa na mafundisho ya uongo na maisha yasiyopatana na imani na maadili ya Kristo. “kutupwa huko na huko” ni maneno yanayoleta picha ya chombo wakati wa bahari kuchafuka (Lk.8:24; Yak.1:6) “kuchukuliwa na kila upepo” ni picha ya karatasi kuchukuliwa na upepo na kuzungushwazungushwa. Ni rahisi kwa wale wasio na msingi imara kuondoshwa katika njia ya kweli. Wengine hudanganywa bila kutambua ya kuwa wamedanganywa. Pia wengine ni wale wa kudanganya wakitumia hila na bidii (2 Tim.3:13) Paulo alijua kwamba wako watu wa namna hiyo wanaotumia hila na ujanja. Mara nyingi wale ambao wameondoka katika njia ya kweli hujitahidi kuwadanganya wengine ile wajipatie wafuasi. Mafunzo ya uongo husababisha mafarakano na matengano kati ya watu na kwa kawaida waalimu wa uongo hujiwaza na kujiweka mbele badala ya kuuwaza “Mwili wa Kristo” na faida yake.

k.15 Wale wa kweli hawazitumii njia za ujanja na hila (2 Kor.4:2). Watahubiri na kufundisha waumini kwa unyofu na nia safi na kwa moyo, tena watafanya “katika upendo”. Kweli, watapaswa kufundisha “kweli za imani na maadili” ila wafanye kwa upendo; ni lazima upendo na ukweli viandame, maana ukweli bila upendo utapasua “ubao” ni kama kugonga msumari kwa nguvu bila kuujali ubao, na upendo bila ukweli ni kitu hafifu. Kwa kufundisha kweli za Imani katika hali ya upendo, basi waumini watazidi “kumfikia Yeye yaani Kristo”. Sehemu zote za maisha zitaguswa na kuelekezwa kwa Kristo na mapenzi yake. Kristo ni “Mwili Mzima” ila pia ni “Kichwa” (1:22, 5:23). Kichwa chaleta wazo la kuwa Kiongozi. Kila jambo ni chini yake, yaani chini ya Uongozi wake. Kila muumini hupata nguvu na afya kadiri anavyomtii Kristo. Kristo ni asili ya ukuaji wa Kanisa, pia ni lengo la Kukua kwake.

k.16 Iwapo Kristo ni asili ya ukuaji wa Mwili pamoja na kuwa lengo lake pia, hata hivyo kila kiungo ni muhimu hasa katika hali ya kutegemeana na kushirikiana na viungo vingine kama ilivyo katika mwili wa mtu. Jambo muhimu

ni kwa kila kiungo kuwa kimeungana na Kichwa, yaani Kristo, vilevile ni muhimu kwa kila kiungo kuutimiza wajibu wake kwa viungo vingine. Ni kazi inayoendelea, mfano wa jengo linaloendelea kujengwa au mwili wa mtu kuendelea kukua na kupevuka na kukomaa. Siri ni "upendo" yote yatendeke kwa upendo na katika upendo (3:17; 4:2, 15).

4:17-24 Maisha Mapya badala ya Maisha ya Zamani

Katika sehemu iliyopita mkazo ulikuwa umoja wa Watu wa Mungu na katika sehemu hiyo mkazo ni juu ya utakatifu wao. Tukirudi kwa k.1 Paulo alianza sura hii kwa kuwaita "waenende kama inavyoustahili wito wenu" akikaza mamlaka yake kama Mtume wa Kristo. Hapo tena Paulo amejitaja kwa nguvu "nasema neno hilo, tena nashuhudia katika Bwana" (Gal.5:3; Mdo.20:26). Ni neno gani? Ni onyo zito kwa sababu iwapo wameuitika wito wa kumfuata Kristo bado wangali wamezungukwa na umati wa watu wanaofuata desturi na maisha yao bila kumjali Mungu wa kweli. Kwa hiyo ni lazima waachane kabisa na maisha yao ya zamani. Paulo alitaja hali za Wamataifa kama alivyofanya katika 2:1ku. "ubatili wa nia zao" maana yake waliishi bila shabaha, na bila tumaini, kwa hiyo hawakujali jinsi walivyoishi. "akili zao zimetiwa giza" hawakuwa na ufahamu wa kweli; "wamefarikishwa na uzima wa Mungu" hawakuwa na uhai wa kiroho, waliishi bila ushirikiano na Mungu aliye Hai. Iwapo wengi wao walikuwa bado hawajasikia Habari Njema ya Kristo, hata hivyo, nuru waliyo nayo katika uumbaji, dhamiri n.k. hawakuifuata (Rum.1:18ku. 2:12ku) Hivyo mioyo yao ilikuwa migumu. Walikuwa wamekufa ganzi, hawakuweza "kusikia" kitu, kwa upande wa kweli hawakuitambua, kwa upande wa ubaya hawakuona aibu, walifanana na watu ambao ngozi imekufa ganzi, kwa hiyo hawasikii "baridi" wala "joto". Kwa sababu mioyo ni migumu na kwa sababu wamekufa ganzi, basi, walijitia kufanya mabaya aina zote wakitawaliwa na tamaa.

Watu wakiupoteza uwezo wa "kujisikia" mwisho ni kuupoteza uwezo wa kujitawala. Chanzo cha kuteleza ni "ugumu wa moyo" ukifuatwa na giza katika akili, na giza husababisha ujinga na ubatili ndipo kiroho mtu hufarikishwa na uzima wa Mungu na kufa ganzi, halafu mwishowe hujitia katika ubaya. Hatua hizo zaonekana katika Warumi 1:18-32.

k.20 "Bali ninyi" Baada ya kuwaonya kwa kuwakumbusha hali za WaMataifa Paulo aliwageukia waumini akisema nao kwamba wao wamefundishwa kuishi tofauti sana na hao WaMataifa. Katika kumpokea Kristo wametiwa nuru kwa mafundisho waliyoyapata. Bila shaka katika matayarisho ya Ubatizo walipewa mafundisho ya maadili ya Kikristo, na fahamu zao zilitiwa nuru ya Kristo.
Walifundishwa "kuvua" na "kuvaa"; kuvua maisha ya zamani na kuvaa maisha mapya, mfano wa mtu kubadili kabisa nguo zake. Shabaha yao iwe ya kumpendeza Mungu, wakiwa na tumaini la uzima wa milele. Lengo lao la sasa ni kujenga Jamii Mpya wa Wanadamu wanaoishi kwa umoja na upendo na ushirikiano mwema. Budi waachane kabisa na machafu na mabaya yote. Kristo

ni kiini cha mafundisho waliyoyapata, pamoja na kuwa asili ya “uhai” wao wa kiroho.

Twaona jinsi nia, akili, na ufahamu ni wa maana katika maisha ya watu. Jinsi mtu anavyowaza na kuamini na kufahamu ni jambo kubwa kwa upande wa mema au kwa upande wa mabaya (Rum. 12:2). Mtu mpya huumbwa kwa namna ya Mungu, ambayo ni haki na utakatifu wa kweli. Kama hali hizo hazionekani, basi, hamna dalili ya kuzaliwa mara ya pili, hamna ushuhuda wa Mungu kufanya kazi ndani. Twajifunza kwamba watu wanapoishi maisha mabya wamedanganywa, wameletwa kuwaza kwamba kwa njia ya kufanya wanavyotaka, basi watapata furaha na utoshelevu wa maisha, kumbe, sivyo, ni uongo wa Shetani. Wanapoishi maisha mema wamefuata mwanga wa kweli utakaowaletea raha ya kweli na amani, nao wamewajibika kuendelea kufanywa upya katika nia zao kila siku (Rum.12:2).

4:25-5:2 <u>Ukweli na upendo badala ya uongo na uchungu</u>

Paulo aliendelea kwa kueleza ni dhambi na tabia zipi za kuachwa yaani wavue nini, na badala yake wavae tabia zipi.

k.25 “vueni uongo, mkaseme kweli kila mtu na jirani yake” Wamekuwa viungo katika mwili mmoja kwa hiyo lazima wawe wa kweli na waseme kweli wao kwa wao ili Mwili upate kufanya kazi yake vizuri. Kwa hiyo kuuvua uongo ni zaidi ya faida ya mtu mmoja pia ni faida kwa wote. Kwa mfano, kama jicho likiona mdudu mkali Je! litaudanganya mguu kwa kusema huyu si mdudu mkali? Likifanya hivyo litauhatarisha mwili mzima, maana mguu utabakiza mwili palepale bila kukimbia. Vivyo hivyo kila Mkristo hana budi kusema kweli ili Mwili mzima uwe salama. Kuaminiana ni hali ya lazima katika kuujenga ushirikiano mzuri.

k.26-27 Tabia nyingine ya utu wa kale ni hasira isiyo na sababu. Lakini ipo hasira ya haki, ambayo waumini wameruhusiwa kuwa nayo, yaani ni haki wayakasirikie mambo kadha, ila mipaka imewekwa: i. wasifanye dhambi, yaani hasira isiruhusu kiburi, chuki, uchungu n.k. ii. jua lisichwe na uchungu wenu bado haujawatoka - yaani wasiibembeleze, isikae kwa muda. Mwisho wa siku iwe imepoa. iii. “tusimpe Ibilisi nafasi” (Yak.4:7) maana yeye ni adui ambaye hujitahidi kuichochea hasira mpaka imetutawala hata tumeshindwa kuitoa. Tena hasira iliyoanza kwa kuhusu jambo fulani yaweza kugeuzwa kulenga jambo jingine zaidi ya hilo la kwanza. Bwana Yesu alikasirika (Mk.3:5; Yn.2:13- 17) budi wafuasi wake nao wakasirike wanapoona dhambi inasitawi wala haikemewi, au wanapoona watu wamedhulumiwa na kuonewa. Mungu hapendi dhambi kwa hiyo watu wake wasiipende. Paulo amesema “uwe na hasira” halafu ametaja mipaka, Yakobo alisema tusiwe wepesi wa kukasirika (Yak.1:19-20).

k.28 Ndipo Paulo alitaja tabia nyingine mbaya ya maisha ya kale. “Mwibaji asiibe tena....bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi...” Bila shaka waumini wengi kabla ya kumpokea Bwana Yesu walizoea kupata riziki zao kwa njia ya wizi, na wengi waliona kuchukua kitu cha mwingine si kosa. Ila katika maisha mapya sivyo ilivyo. Budi “wavue wizi”, na badala ya kuiba wavae utu mpya wa kuishi kwa njia ya kufanya kazi na kupata riziki zao kwa mapato ya halali. Tena walishauriwa wawe na juhudi katika kufanya kazi, wasiwe wavivu, wasiwalemee wengine. Tena, wajaribu kuwa na ziada ili wawasaidie wahitaji. Ni badiliko kubwa kwa mwizi kugeuzwa kuwa mfadhili, lakini ndivyo watakavyokuwa, kwa neema ya Kristo. Katika hali hiyo njema si wao tu watakaosaidiwa, ni Mwili wa Kristo, yaani Wakristo wenzao. Wataepuka na hali ya kujipenda na kujiwaza. Tangu mwanzo Kanisa limeukaza wajibu wa kuwasaidia maskini na wahitaji (Mt 19:21; Lk.14:13; Yn.13:29; Mdo.2:44; 4:32ku. 6:1-4; Rum.15: 25-29; Gal.2:10; 2Kor.8 na 9)

k.29 Uwezo wa kusema ni kipawa kikubwa kutoka kwa Mungu. Katika uwezo huo tumetofautiana na wanyama wasioweza kusema. Paulo amekwisha kuwaambia wasiutumie uongo, wawe watu wa kusema kweli, kwa sababu kwa njia hiyo watajenga hali ya kuaminiana na uhusiano mwema. Katika kifungu hicho Paulo amerudia jambo la kunena. Zaidi ya kutokusema uongo anataka wasinene neno lo lote baya, kwa sababu mazungumzo na maneno yanasababisha watu kutafakari mambo yasiyofaa, mambo yasiyo ya maana wala lengo, ya upuzi yasiyowafaidi watu. Maneno mabaya ni kama matunda mabovu ambayo huyaozesha matunda mengine (Mt.12:33-37; Yak.3:1-12). Badala yake wanene mambo mazuri yenye faida na msaada kwa wale wanaohitaji mashauri na uongozi, na kuwatia moyo au hata kuwaonya (Mith.12:18; 15:23). Kwa hiyo, iliyopo ni mtu aepukane na makosa katika kunena kwake na zaidi maneno yake yawe njia ya kuwahudumia wengine, yawe ya neema. Twasoma watu waliyastaajabia maneno ya neema yaliyotoka kinywani mwa Yesu (Lk.4:22; Kol.3:16; 4:6).

k.30 Neno juu ya kumhuzunisha Roho limewekwa mara baada ya Paulo kusema juu ya habari za kunena. Twaweza kumhuzunisha Roho kwa sababu tumeitwa kushirikiana naye kibinafsi, Yeye ni Nafsi na sisi ni nafsi. Roho ndiye kifungo cha kuwaunganisha waumini wote pamoja, na tunapomkosea ndugu kwa maneno yasiyofaa au kwa tendo lisilo zuri, basi twamhuzunisha Roho (Ling.5:18-19). Imeonekana kwamba Roho amehusika sana na maneno na usemi wa Wakristo. Tulipoamini tulitiwa muhuri na Roho Mtakatifu (Efe.1:13) na kazi ya Roho ni kutulinda katika imani na utakatifu mpaka siku ya mwisho, yaani mpaka mwisho wa safari yetu, hivyo yatupasa kuangalia sana mwenendo wetu wa kila siku. Ni dhahiri Roho ana hali ya “nafsi” kwa sababu ni wenye nafsi tu walio na uweza wa “kusikia” huzuni, maudhi, furaha n.k. Kwa sababu Roho ni Roho Mtakatifu, daima ataumizwa na yote yasiyo matakatifu; pia kwa sababu Roho ni mmoja hali zote za farakano na utengano zitamhuzunisha. Tena Roho ni Roho wa Kweli na kwa sababu hiyo makosa

yote katika kunena humhuzunisha. Mkristo alenge kumfurahisha kwa kunena vema.

k.31 Ndipo Paulo ameyataja mambo ambayo Mkristo hupaswa kuyaondoa katika maisha yake. Uchungu wote, ghadhabu, hasira, kelele, matukano na kila namna ya ubaya. Uchungu wote ni kama ukali, uhasimu, chuki, kutokuwa tayari kupatanishwa, hali hizo zote ziondoke kabisa. Halafu ghadhabu na hasira (Rum.2:8; Kol.3:8; Ufu.16:19; 19:15) Ni nini tofauti kati ya hasira na ghadhabu? Ghadhabu ni kama kuhamaki, kufoka, na hasira ni kama hali inayokaa ndani. Kelele na matukano vinatumiwa na watu wanapogombana wakipiga kelele na kukasirikiana, Pia, ni kusema vibaya, kusengenya, na kumtusi mtu (1 Kor.10:30; Kol.3:8; Tit.3:2). Halafu Paulo alimaliza orodha na "kila namna ya ubaya" ni kila hali ya mtu ambaye humkabili mwenzake vibaya. Paulo alifundisha kwamba budi Mkristo aachane kabisa na hali hizo zote kusudi uhusiano wake na wengine uwe mzuri.

k.32 Ila haitoshi wayaondoe mambo hayo katika maisha yao. Wapaswa kuyaweka mambo mengine mazuri badala yake ili hayo yasipate nafasi kuzuka tena. Paulo ametaja, fadhili, huruma, msamaha (Kol.3:12). Kumfadhili mtu ni kumpenda kiutendaji, ni kujiweka mahali pa mwingine na kumtendea kama yeye mwenyewe angependa kutendewa. Kuwa na huruma ni kuwa na moyo wa upendo, si kutenda matendo mema tu, bali matendo mema yafanywa kwa moyo na kwa furaha. Halafu kusameheana ni jambo la maana kwa sababu mara nyingi kitu kinachotuzuia tusimfadhili mwingine ni kwa sababu bado tungali na neno juu yake (Kol.3:13). Kristo ametupa kielelezo chema, maana Yeye ametangulia kutusamehe. Ni vigumu kwa mtu asiye tayari kusamehe kuupokea msamaha wa Mungu (Mt.6:12, 14ku.18:21-35). "kama na Mungu.."ni kuonyesha kwamba msamaha wetu hauna budi kufanana na ule wa Mungu, uwe kamili, na uwe bila masharti.

5:1-2 Hapo nyuma Paulo amesema juu ya maadili akipambanisha aina za ubaya wa kuvuliwa na aina za wema wa kuvaa. Kisha katika vifungu hivi viwili amejumlisha kwa kuwaita waumini kumfuata Mungu kama watoto wapendwa. Katika 4:1 aliwaita "waenende kama ilivyoustahili wito wao; na katika 4:17 aliwasihi "wasienende kama WaMataifa" kwa sababu sivyo walivyojifunza Kristo, yaani si jinsi walivyofundishwa. Alianza Waraka kwa kuzitaja baraka kubwa za kuchaguliwa na Mungu katika Kristo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ili wawe watakatifu na kufanywa kuwa wana wake kwa njia ya Kristo. Sasa waitwa "kumfuata Mungu kama watoto wapendwa" Basi, wamfuate kwa namna gani? Jibu ni "mkaenende katika upendo" Basi wameitwa kupendana ili wafanane na Baba yao, tena upendo wao ulingane na upendo wa Kristo, uwe upendo wa kujitoa, uwe upendo wa namna ya kidhabihu - si upendo rahisi, si upendo wa juujuu, wala upendo usiowagharamia hali au kitu. Upendo wa kijitoa ni upendo unaompendeza Mungu. Ni heshima ya hali ya juu kuwa Mtoto wa Mungu, tena ni heshima

kubwa kuwa wapendwa wake (Mt.5:44ku. Lk.6:36; 1 Yoh.4:10; Yn.13:34). Itikio lifaalo kwa upendo wa Mungu ni kufanana naye katika tabia na katika kutenda. Neno “enenda” ambalo limetumika mara nyingi katika sehemu hiyo linaonyesha kwamba ni maisha ya kila siku yanayosemwa. Kristo Mwenyewe hakusema anatupenda tu, bali aliuonyesha upendo wake kwa kutenda tendo kuu sana katika Kufa kwa ajili yetu. Ila ni vema tukumbuke ya kwamba Kifo cha Kristo ni zaidi ya kielelezo. Hakuna mahali popote katika Agano Jipya ambapo Kifo chake kimetajwa kama kielelezo tu, hata hapo maneno “sadaka, dhabihu, na kwa ajili yetu” yauhusu upendo wa ukombozi. Tena, tendo lake la kujitoa mpaka Kufa lilimpendeza Baba yake, lilikuwa kama harufu ya manukato Kwake, lilijaza mbinguni harufu nzuri. Vivyo hivyo tunapoishi maisha ya namna hiyo sisi nasi twatoa harufu nzuri (Flp.4:18; 2 Kor.2:14-16). Ni hapo tu waumini wameitwa kumfuata Mungu.

5:3-14 <u>Nuru badala ya giza</u>

Paulo anaendelea kutoa mashauri yake kuhusu mwenendo wao.

k.3 Alianza sehemu hiyo kwa kusema juu ya upendo uliopotoka hasa katika uhusiano kati ya wanaume na wanawake. Alijua kwamba walizungukwa na umati wa watu ambao waliishi katika uchafu, uasherati, uzinzi n.k. mambo yaliyo hatari kwa waumini. Bila shaka wengi wao walikuwa wamezoea maisha ya namna hiyo kabla ya kuokolewa. Alitaka wajihadhari kabisa na hali zote ambazo zilipinga mapenzi ya Mungu ambayo ni ya mtu mmoja na mke mmoja kuishi pamoja katika ndoa. “kutamani” kumewekwa pamoja na uasherati na uchafu, pengine ina maana ya kupita kiasi au kuzidi mpaka wa uhalali katika matumizi ya mwili, kiasi cha kudhuru watu. “uasherati usitajwe kamwe” yaani hata kuyazungumza mambo hayo ni kosa, kwa sababu wameitwa kuwa “watakatifu” yaani safi. Tena si vizuri hata kusemasema juu ya dhambi za wengine kama ni jambo jepesi, kumbe ni jambo zito. Licha ya kutokufanya hayo hata kuyawaza na kuyazungumza ni vibaya.

k.4 Aibu, maneno ya upuzi, ubishi, ni mambo yasiyotakiwa. Aibu ni yale yote ya kumtia mtu aibu, mambo ambayo mtu mwema atasikia haya juu yake kama mazungumzo machafu n.k. Maneno ya upuzi ni mazungumzo au maneno yasiyo na maana wala faida, ni maneno au mazungumzo ya bure. Ubishi ni kama maneno ya mtu anayejiona ana akili. Tena mbishi huamsha ugomvi na majadiliano yasiyoleta faida kwa maisha ya kiroho, mbishi apenda kusemasema na kuchokoza mambo bila shabaha ya kujenga uhusiano mzuri. Hali hiyo nayo haina faida kwa Mkristo na maisha yake ya kiroho. Badala yake Mkristo aweke “shukrani”, maana shukrani ni kama mafuta yanayolainisha uhusiano kati ya watu. Hasa mzungumzo ya Mkristo yawe ya neema, na katika mazingara ya sehemu hiyo bila shaka maana yake ni aseme juu ya uzuri wa vipaya vya Mungu katika uhusiano mzuri na halali wa mume na mke na baraka ya upendo wa kweli wa kimwili.

k.5-6 Halafu Paulo ameweka neno zito akisema wazi juu ya wale ambao hawatauurithi Ufalme wa Mungu. Tena amesema katika hali ya kuwa wamekwisha kufundishwa uhakika wa neno hilo “mnalijua hakika”. Ni nini walilolijua kwa uhakika? Walijua kwamba hakuna mwasherati, wala mchafu, wale mwenye tamaa ndiyo mwabudu sanamu ambaye ataurithi Ufalme wa Kristo na Mungu. Tena, aliongeza kwa kuwaonya juu ya kudanganywa. Bila shaka walikuwapo watu waliojitahidi kuutikisa ukweli huo kwa kusema sivyo ilivyo. Pengine wengine walikaza jinsi ilivyo vigumu kuishi maisha safi katika ulimwengu huu na kwa sababu hiyo si vizuri Mungu awatazamie kuishi hivyo.

Kisha Paulo alitaja “hasira ya Mungu”. Wale walio “wana wa uasi” tofauti na wale walioitwa watoto wa Mungu (2:2-3) yaani wale wasiokubali neno hilo la usafi wa maisha watapatikana na hasira ya Mungu. Matokeo ni mazito sana kwa wale wote wanaoishi maisha yaliyotajwa wasipotubu. Twaona mwenye tamaa ameitwa “mwabudu sanamu”. Kwa nini? kwa sababu mtu anayetamani kitu au mtu ametanguliza kile kitu au yule mtu kabla ya Mungu, na hii ndiyo kuabudu sanamu maaana amri ni “usiwe na miungu mingine ila Mimi” Waasi wanajua sheria ya Mungu na kuiasi. Ni picha ya watu waliojitoa kwa mabaya.

Je! dhambi za aina hizo ni kubwa kuliko zingine kama kiburi, kujipenda n.k.? la! Ila Neno la Mungu halituruhusu kuwaza kwamba zile dhambi zinazoivunja ndoa na kuharibu familia na kusababisha watoto kuzaliwa nje ya ndoa bila wazazi kuubeba wajibu wao wa kuwatunza na kuwalea, ni dhambi ndogo, la, ni dhambi kubwa.

k.7: Waumini wasishirikiane na watenda mabaya katika kutenda kwao. Haina maana ya kujitenga nao katika mambo ya kawaida ya kuishi (1 Kor.5:9-10; Yn.17:15).

k.8-10 Kwa nini waenende kama ilivyostahili wito wao? Paulo ametoa sababu nyingine. Zamani walikuwa “giza” (yaani maisha yao si mazingira yao tu) bali sasa wamekuwa nuru katika Bwana, kwa hiyo “waenende kama watoto wa nuru”. Maneno giza na nuru huonyesha tofauti kubwa kati ya maisha yao ya zamani na maisha yao sasa kama Wakristo. Kama Paulo alivyosema katika 1:18 wametiwa nuru ya Kristo, nao wamo katika Kristo aliye Nuru (Yn.8:12) Wamehamishwa kutoka giza mpaka nuru. (Mdo.26:18; Rum.13:11; 2 Kor.4:6; Kol.1:13; 1 Pet.2:9). Kwa sababu Mungu ni Nuru (1 Yoh.1:5) amejifunua, yaani Amejiweka wazi kwa wanadamu kwa njia ya Yesu Kristo. Yeye hupenda kuwafunulia wanadamu mapenzi yake. Ulimwengu ulio kinyume chake hukaa katika giza.

Kwa sababu wamekuwa nuru katika Bwana basi waenende vivyo hivyo na waishi maisha ya kila siku kwa nuru hiyo, wamfuate Kristo kweli, ndipo tunda la nuru litaonekana, katika wema wote, yaani katika kila namna ya wema, na katika haki na kweli. Mambo hayo ni tunda la nuru. Wakiishi kwa kanuni hiyo ya

nuru watampendeza Bwana. Mkristo wa kweli hutafuta kujua na kuhakikishia mapenzi ya Bwana kwa maisha yake (Rum.12:2; 2 Kor.5:9; Flp.4:18; Kol.1:10). Hali hizo zitakuwa badala ya chuki na uchungu, matukano na kelele (4:31) uhusiano na watu utakuwa mwema wakiishi nao kwa kuwatendea wenzao kwa haki, na kwa rehema, na kwa kweli badala ya udanganyifu na uongo.

k.11-13 Maisha ya zamani ya giza hayakuzaa matunda mazuri (Rum.6:21) ni kama waliishi bure. Iliyopo wajitenge na matendo ya giza (5:7) wasishirikiane katika matendo yao, kwa kuwa wamehamishwa, hawapo tena katika eneo la giza. Sasa wamo katika eneo la nuru. Pia wapaswa kuyakemea matendo ya giza, hasa kwa njia ya kuishi maisha ya tofauti sana, maana maisha yao ya nuru yatayadhihirisha matendo ya giza hata bila wao kuyasemasema, kwa sababu Paulo amesema “ni aibu hata kuyanena” na k.3 “usitajwe kamwe” ling. Yn.3:20.

k.14 “Hivyo husema” asili ya maneno yanayofuata si wazi ila yafikiriwa yalitumika na Wakristo. Msingi wa maneno ni katika Isaya 9:2; 26:19; 52:1 40:1. Yafikiriwa yalitumika wakati wa Ubatizo au katika matayarisho ya Ubatizo kama Katekisimo, au huenda ni sehemu ya wimbo.

Mambo matatu yahusu wito wa kumgeukia Mungu:
i: wito wa kuamka kutoka usingizi;
ii: wito wa kufufuka kutoka wafu; na
iii: wito wa kutoka gizani na kuingia Nuru ya Kristo (Rum.13:11),
Katika sura ya pili Paulo alifundisha kwamba dhambi ni mauti na wote wamefanya dhambi. Kristo amefufuka na Yeye anawahuisha wote wampokeao. Tena amefundisha kwamba wale walio nje ya Kristo wamo gizani ila wakimjia Yeye anawaangaza. Ni kama wimbo au shairi linalojumlisha mafundisho ya Paulo katika Waraka huo, na kama tulivyosema huenda ni maneno Kanisa lilivyozoea kuyatumia ama katika Ubatizo au katika Ibada.

5:15-21 <u>Hekima badala ya Ujinga</u>

Paulo hakuacha kusema juu ya mwenendo wao. “Basi, angalieni sana jinsi mnavyoenenda” ila badala ya kuutumia mfano wa nuru na giza ameutumia mfano wa hekima na ujinga, akitofautisha watu kwa maneno “wasio na hekima” na “wenye hekima”. Waumini wamepewa hekima na Mungu (1:8,17). Ni hekima ya kiutendaji, si ya mawazo tu. Wenye hekima watakuwa na utambuzi wa wakati. Watajua kwamba nyakati zao ni za uovu, nao watajua kwamba ni wajibu wao “kuukomboa wakati”, maana yake waishi kwa hekima ya kuutumia wakati kwa faida ya kiroho katika kuhakikisha mapenzi ya Mungu kuwa nini, kusudi wayafanye kama Mungu anavyotaka. k.10. Wawe waangalifu sana, wasiishi kwa “mradi tu” au “bila tahadhari”. Wapaswa wapime mambo na kukamata nafasi yoyote inapotokea, hii ndiyo maana ya “kuukomboa wakati” huenda lipo wazo la kuwaelekeza kufikiri kwamba wakati walio nao ni mfupi, na kila nafasi ishikwe kabla haijatoweka (1 Kor.7:29; Gal.6:10).

“Wakati” ni kitu cha thamani na watu wote wamepewa masaa 24 katika siku 1 na siku 7 katika juma, na majuma 52 katika mwaka na kadhalika. Kwa hiyo tuwaze “wakati” kwa uzito na kuutumia kwa uangalifu ili tusipoteze masaa kadha au siku kadha katika mambo yasiyofaa. Wakati haurudi, unaendelea hadi mwisho wake. Hivyo wajitahidi kabisa kujua mapenzi ya Mungu na kuyatekeleza, maombi yatawasaidia.

k.18 Jambo moja la ujinga ni ulevi na mara nyingi ulevi unaandama na ufisadi, watu wakishindwa kutawala matendo yao kuwa sababu wamekuwa chini ya uongozi wa “kileo”. Mambo hayo hayana msaada wowote kwa mtu na maisha yake. Tangu zamani watu wametafuta kushinda au kusahau ugumu na shida za maisha kwa njia ya “kileo” ili warushwe au kupotewa na akili kwa muda, na kuingia hali ya furaha kama ya uvuvio. Watu wa sehemu zote za ulimwengu wamefaulu kubuni “kileo” kutoka vitu vipatikanavyo mahali pao. Inaonekana hata watumishi wa Kanisa walijaribiwa kuzidi mpaka katika kutumia divai (1Tim.3; 3,8; Tito 1:6,7; 2:2; 1 Pet.4:4), Paulo aliagiza “msilewe kwa mvinyo”.

Halafu aliendelea kwa kuagiza “mjazwe Roho”. Hapo nyuma alisema wametiwa muhuri na Roho (1:13) na “wasimhuzunishe Roho (4:30). Paulo hakutaka kuwanyima furaha katika maisha yao. Ila ipo njia bora ya kushinda ugumu na shida za maisha, njia ambayo kwayo watasikia furaha ya kweli na bubujiko safi na la halali. Wajazwe Roho si divai. Waruhusu Roho kuwajaza. Katika Waraka Paulo amesema wamo “katika Roho” (2:18;22; 3:5; 6:18). Maana ya “kujazwa” ni kila sehemu ya maisha kuwa chini ya uongozi wa Roho, na hali hiyo si jambo litokealo mara moja tu, bali ni jambo la kurudiwarudiwa kila wakati (Mdo.2:4; 4:31; 9:17; 11:24; 13:52) Chini ya uongozi wa Roho hawataupoteza uwezo wa kujitawala tofauti na kuwa chini ya uongozi wa kileo, maana tunda la Roho ni kiasi (Gal.5:23) Matokeo ya kujazwa na Roho ni nini? Paulo ametaja tokeo moja ni la Wakristo kushirikiana pamoja kwa njia ya kuimba na kumsifu Mungu wakitumia vyombo vya muziki, na zaburi, na nyimbo ainaaina. Kwa njia hiyo watiane moyo huku wakimsifu Mungu. Muziki na nyimbo zimekuwepo katika Kanisa tangu mwanzo na bila shaka ni kwa sababu waliyarithi mambo hayo kutoka dini ya Kiyahudi, kwa kuwa waumini wote wa kwanza walikuwa Wayahudi na ibada zao zilifuata mfano wa ibada za sinagogi. Moyo ni kitu kikubwa kuliko sauti nzuri, waimbe kwa ukweli wa moyo. Kila mara uamsho katika Kanisa umeleta uamsho katika uimbaji.

Tokeo lingine la kujazwa Roho ni shukrani kwa Mungu Baba (1:16) Iwe tabia yao daima katika mambo yote kumshukuru Mungu. “katika Jina la Bwana Yesu Kristo” ni ukumbusho kwamba mema yote ambayo wametendewa ni kwa njia ya Kristo na ukombozi wake. Kumshukuru kwa mambo yote si kumshukuru kwa maovu au kwa matokeo ya dhambi. Mambo yote ni yale yote yanayopatana na Ubaba wa Mungu na upendo wake ulioonyeshwa katika kumtoa Kristo.

Tokeo lingine ni kunyenyekeana. Kila mmoja ajitie chini ya wenzake, asiwepo anayejiinua juu ya mwenzake. Neno hilo linatukumbusha hoja kubwa ya Waraka juu ya umoja kama mfano wa Mwili na viungo vyake. Mjazwe Roho ni agizo kwa wote si kwa wachache. Mtu aliyejaa Roho asijitenge na wenzake, bali azidi kushirikiana nao. Katika shirika za Kikristo waumini waishi kwa utaratibu na kwa kuachiana nafasi si kama Wakristo wa Korintho (1 Kor.14:26- 33) Wamekwisha kuambiwa wajitahidi kuuhifadhi Umoja wa Roho (3:2-3). Paulo aliongeza maneno “katika kicho cha Kristo” (2 Kor.7:1; 1 Pet.2:17) maana Yeye ni Kichwa cha Mwili na Yeye hushikamanisha Mwili Mzima. Haina maana kwamba wakubali kufanya matakwa ya wengine haidhuru ni nini, La! ila wawe tayari kujitia chini ya wengine kwa shabaha ya kujengana katika Kristo.

Katika sehemu yote kuanzia 5:22 - 6:9 Paulo amesema juu ya uhusiano wa mke na mume, watoto na wazazi, mabwana na watumwa na kila mara amefuata mtindo mmoja. Amekaza wajibu zao si haki zao.

5:22-23 <u>Uhusiano mwema wa mume na mke</u>

Kwanza alianza na maisha ya nyumbani hasa kwa upande wa mume na mkewe. Kwa upande wa mke wajibu wake ni kumnyenyekea mumewe (1 Kor.11:3; 1Kol.3:18; Tito 2:5; 1 Pet.3:1ku.) (huenda kwetu neno “utii” lina nguvu kuliko alivyowaza Paulo)

Agano Jipya lafundisha kwamba waume kwa wake ni sawa kabisa kiroho (Gal.3:28) Hata katika uhusiano wa kimwili katika ndoa Paulo alitoa idhini yake kwamba katika kukaribiana hakuna aliye juu ya mwenzake, kwa hiyo, wawe wamepatana kwa kuwa hakuna aliye na amri zaidi kuihusu miili yao.(1 Kor.7:4) Ila kwa ajili ya utaratibu na umoja katika familia uongozi umo mikononi mwa mume na baba.

k.22-24 Kwanza Paulo alisema na wake. Wajibu wao ni kuwatii waume zao “kama kumtii Bwana wetu”. Maneno hayo hayana maana kwamba uhusiano wa mke na mume ni sawa na uhusiano wao na Bwana Yesu, ila ina maana kwamba mke anapoutimiza wajibu wake wa kumtii mumewe vilevile anautimiza wajibu wake kwa Kristo. Katika Kol.3:18 maana hii imewekwa wazi “ninyi wake watiini waume zenu kama impendezavyo katika Bwana”. Nyuma ya mume, wamtambua Bwana Mwenyewe ambaye amewapa madaraka hayo. Wakipenda kumtii Yeye watawatii wale kwa kuwa ni kwa mamlaka Yake wamepewa madaraka yao (k.21).

Kwani utii umewekwa kuwa wajibu wa mke? Ni sababu katika mpango wa uumbaji Mungu amemtanguliza mume. Mume ni kichwa, (1 Kor.11:3-12; 1Tim.2:11-13 ling. Mwanzo 2:18-25). Ila siyo kusema mamlaka ya mume haina mpaka, utii wa mke ni katika mambo ya halali, lakini mume akizidi mpaka kwa kutokuutumia uongozi wake vizuri, basi mke hafungwi na wajibu wa kumtii. Tutaangalia neno hilo katika kufikiri juu ya wajibu wa mumewe. Neno la utii

limejengwa juu ya uumbaji uliomweka mume kuwa kichwa cha mkewe. Pia limewekwa juu ya neno la ukombozi, maana katika ukombozi mume amewajibika kumtunza mkewe na mke aupokee huo utunzaji kwa shukrani.

k.23-24 Wajibu wa mume. Tumeona ni juu yake kuongoza familia yake vizuri, maana amepewa mamlaka na Mungu kufanya hivyo. Ila mamlaka hiyo imesimama katika kumdai upendo wa hali ya juu. Tena wote wawili budi wauwaze uhusiano wao kama mfano wa Kristo na Kanisa lake. Mume ni kichwa cha mkewe kama Kristo ni kichwa cha Kanisa, kwa hiyo mke amtii mumewe kama Kanisa limtiivyo Kristo. Kwa hiyo Paulo ameutumia uhusiano wa mume na mke kuwa mfano wa Kristo na Kanisa, akionyesha jinsi katika ndoa upendo na kutegemeana, mamlaka na utii vilivyo. Mfano wa Kanisa na Kristo ni bora kuliko mfano wa Hekalu na Jiwe la msingi, na hata mfano wa Kichwa na Mwili kwa sababu katika mfano wa mume na mke hali ya "nafsi" ni bora kuliko vitu kama jiwe na mwili. Mambo mawili yamo katika mfano wa Kristo kuwa Kichwa cha Kanisa, moja ni wajibu wa Kristo kwa Kanisa na la pili ni wajibu wa Kanisa kwa Kristo.

Pamoja na kuwa Kichwa cha Kanisa Kristo ni "Mwokozi wa mwili" Je! Mume ni Mwokozi wa mkewe? La! maana jambo la Kristo kuwaokoa watu ni la pekee wala hamna mfano wake. Ila Paulo ameingiza wazo hilo ili aonyeshe ni wajibu wa mume kumtunza sana mkewe na katika upendo wa kujitoa afanye juu chini kufanya hivyo k.25; k.28ku.

k.24 Inaposema "wake watiini waume katika kila jambo" ni katika mazingira ya mume kumpenda mkewe na kujitoa kwa ajili yake. Kama mume atampenda mke kama Kristo alivyolipenda Kanisa basi, haiwaziki kwamba mke atasikia shida yoyote katika kumtii mumewe. Hatafanya lolote la kumwumiza au kumhuzunisha au kumshusha. Wala haiwaziki kwamba mke atanyimwa nafasi za kupumua vizuri na kuvitumia vipawa na uwezo wake.

k.25 Hapo Paulo amesema kwa waume: "wapendeni wake zenu kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake". Tena Paulo alitumia neno la Kigriki kwa upendo "agape" neno ambalo limetumika kueleza upendo wa Kristo. Yapo maneno mawili mengine ya upendo, ashiki, na upendo wa kindugu. Kwa hiyo upendo unaotajwa si upendo unaouitikia upendo wa mwenzake tu. Zaidi ni upendo unaojitoa kuwaza na kumtunza mwenzake.

k.26 Kristo alilipenda Kanisa na kujitoa kwa ajili yake kwa kusudi la kulitakasa na kulisafisha. Kristo anayo mapenzi makuu juu ya Kanisa. Apenda watu wake kuwa "safi kabisa" bila mawaa. Kweli mume hawezi kumtakasa mkewe kwa namna hiyo ila liko wazo la mume kutafuta sana ubora wa mkewe, ili aufikie upeo wa uwezo wake. Mume ampendaye mkewe atajitahidi kumsaidia akue kiroho, awe na tabia njema, awe na uzuri wa ndani.

k.29 “hakuna mtu anayeuchukia mwili wake bali huulisha na kuutunza kama Kristo naye anavyolitendea Kanisa” Katika Mwanzo 2:21-24 twaona jinsi mke ni sehemu ya mwili wa mumewe kwa hiyo katika kumtunza mkewe mtu hujitunza mwenyewe.

Katika sehemu hiyo yote Paulo anazungumza mambo mwili, Kristo na Kanisa lake na mume na mke wake. Mara asema juu ya Kristo na Kanisa lake, mara asema juu ya mume na mke wake. Siyo kusema mambo yote mawili ni sawa, kwa sababu uhusiano wa Kristo na Kanisa huwa bora zaidi ya uhusiano wa mume na mke hata hivyo ameuinua uhusiano wa mume na mkewe kuwa wa maana sasa, uhusiano upasao kufanana na ule wa Kristo na Kanisa iwapo hautafikia kuwa sawa lakini ni mfano wa kufuatwa.

k.30 Hapo tena Paulo amesema juu ya Kristo na Kanisa lake. Mkazo ni juu ya urafiki wa ukaribu sana kati ya Wakristo na Kristo. Kama mke amekuwa sehemu ya karibu sana na mume na maisha yake hali mume anampenda na kumtunza sana, vivyo hivyo hata Bwana Yesu atendavyo kwa watu wake akiwahesabu kuwa wa karibu sana hali ameungana nao kama tawi na mti, mfano wa mzabibu (Yn.15).

k.31 Ndipo Paulo ametaja kitu ambacho kimetawala mawazo yake yote. Msingi wa mawazo hayo ni katika Mwanzo 2:24, mahali ambapo tumepewa kwa wazi kusudi kuu la Mungu katika kuiamuru ndoa. Kusudi hilo ni mwamba imara wa Kanisa na sababu ya Kanisa kuzikataa sababu zote ambazo zimeletwa na watu kuipinga ndoa ya mume mmoja na mke mmoja kuishi pamoja kwa maisha yao yote kama watu wawili waliojiunga katika ndoa kuwa kama mwili mmoja. Neno hilo lapinga wale wote wanaotaka kuishi bila kuujali mpango huo, au wanaopenda kuishi maisha ya kuutumia miili yao isiyo halali katika uchafu na ufisadi. Hata Bwana Yesu alipoulizwa juu ya talaka alirudisha watu kufikiri juu ya ndoa kuwa mapenzi ya Mungu akisema talaka imeruhusiwa tu kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya wanadamu walioshindwa, lakini si jambo limpendezalo Mungu (Mt.19:4ku) Hata wajibu wa kwanza kwa wale wanaooana ni kuwaacha wazazi wao na kuangalia maisha yao ya pamoja.

k.32 Paulo aliona jambo hilo ni kweli ya ajabu sana. Ndipo alirudi kusema tena juu ya Kristo na Kanisa hali akishangaa kwamba Kristo na watu wake wako pamoja katika uhusiano wa ukaribu sana. Ndipo alimaliza sehemu hiyo

akishauri mume ampende mkewe kama nafsi yake, na mke amstahi mumewe (k.21).

6:1-4 <u>Uhusiano mwema wa wazazi na watoto</u>

Paulo aliendelea kwa kusema juu ya uhusiano wa wazazi na watoto. Kwanza alifundisha wajibu wa watoto kwa wazazi wao. Wajibu wao ni utii, akiweka

maneno “katika Bwana” kama ambavyo aliweka kwa wake na waume zao (Kol.3:20). Siyo kusema wazazi wataagiza mambo yasiyo halali kwa watoto ila Paulo alikuwa akiwaza mahali pa watoto katika nyumba za Kikristo. Pia alisema “hii ndiyo haki” maana yake katika utaratibu wa uumbaji ni sawa. Tena katika Amri walizopewa Wayahudi hii ndiyo amri iliyowekwa kwa watoto (Kut.20:12). Pamoja na hayo Bwana Yesu alitoa kielelezo chema wakati wa utoto wake (Lk.2:51). Amri ya 5 ilikuwa na ahadi “ukae siku nyingi katika dunia” pengine maana yake ni kwamba familia zinazoishi kwa umoja na utaratibu zasaidia jamii ya watu kuwa imara na kudumu kuliko zile jamii ambazo maisha ya familia kwa ujumla ni hafifu. Ni vigumu kufikiri kwamba maana yake ni kwamba watoto wanaowatii wazazi wao wataishi maisha marefu.

“Amri hii ndiyo ya kwanza” ni vigumu kukubali kwamba amri hii ya tano ilikuwa ya kwanza yenye ahadi, maana hata amri ya pili ilikuwa na ahadi. Huenda ni kusema ni muhimu kwa watoto kuishika.

k.4 Lakini si watoto tu walio na wajibu, hata wazazi wanao wajibu. Paulo alisema “nanyi, akina baba” Je! ni kwa baba tu? huenda ni kwa baba na mama. Wajibu wao ni nini? “msiwachokoze watoto wenu”. Kwa njia gani wataweza kuwachokoza? Labda kwa kuwakandamiza wakiwadai mambo mengi madogomadogo; labda kwa kuwahukumuhukumu; labda kwa kuwanyima nafasi za kujieleza na kutumia uwezo na vipawa vyao. Wawe na hekima, ili wasiwakatishe tamaa (Kol.3:21).

Pia, wazazi wajibika kuwalea watoto wao katika adabu na maonyo ya Bwana. Ni juu yao kuangalia maisha yao ya kiroho ili watoto wafundishwe maadili, waongozwe kumtanguliza Bwana Yesu katika maisha yao, kumpenda na kumcha. Wawe na afya rohoni, na ikitakiwa warekibishwe makosa yao. Kwa hiyo ni juu ya Wakristo walio wazazi kutia maanani hali ya kiroho ya watoto wao hata kabla ya elimu na afya zao, na maendeleo yao ya kimwili. Neno zuri ni kwamba watoto walishirikishwa maisha ya Kanisa, hata wamepewa sehemu yao katika mashauri ya Paulo.

6:5-9 <u>Uhusiano mwema wa mabwana na watumwa</u>

Zamani zile watumwa walikuwa wengi, na watu walizoea kuwa na watumwa waliowatumikia katika shughuli za nyumbani. Watumwa wengi walivutwa na Injili nao wakamkubali Bwana Yesu. Walipokelewa katika Kanisa kwa njia ya ubatizo sawa na wengine wote, wakiruhusiwa kushirikiana na Wakristo wenzao katika ibada na mikutano ya Kikristo, mradi walipata ruksa ya mabwana wao ikiwa mabwana wao hawakuamini.

Iwapo mafundisho ya Paulo yalihusu watumwa na mabwana wao, vilevile yawahusu wafanyi kazi wote na wakubwa wao. Mafundisho ya Paulo yasema juu ya jinsi iwapasavyo wafanyi kazi kufanya kazi zao, na jinsi iwapasavyo mabwana kuwafanyia.

Kwanza Paulo aliwaambia watumwa ni wajibu wao kuwatii mabwana wao. Maneno “walio bwana zenu kwa jinsi ya mwili” ni ukumbusho kwamba wote wanaye Bwana aliye juu mbinguni ambaye ni bwana juu ya uhusiano wao. Halafu Paulo aliendelea kusema kwamba imewapasa kuwatii kwa hofu na kwa kutetemeka, na kwa unyofu wa moyo. Kwa hiyo, iwapo wanamtumikia bwana wa hapa duniani, hata hivyo utumishi wao pia ni kwa Bwana Yesu. Hivyo kazi za hapo duniani zawekwa sawa na utumishi wa kiroho katika kumtumikia Kristo. Tena wasifanye kazi katika hali ya kujali wanadamu na kutafuta kibali cha watu. Budi wafanye kazi kwa kumtazama Bwana Yesu kwa nia ya kumpendeza. Ni kama kila kazi iwe na uzuri wa kutosha kumwonyesha Bwana Yesu na kumridhisha. Halafu Paulo alitaja jambo la thawabu iliyopo kwa kazi za namna hiyo, thawabu kutoka kwa Bwana itakayolingana na ile kazi.(Kol.3: 23- 24; 1 Pet.1:17; 2 Kor.5:10; Ufu.22:12) Jambo la thawabu lahusu si watumwa tu bali wafanyi kazi wengine.

Ni nini, wajibu wa mabwana? Ni kuwatendea watumwa wao vizuri, hasa wasiwatishe, wasiwe wakali n.k. Itawapasa kukumbuka ya kuwa iwapo wao ni mabwana hata hivyo wanaye Bwana aliye mbinguni, Bwana asiye na upendeleo. Wanapowaongoza watumwa wao kwa upande wa kazi na maisha yao kwa jumla wafanye “katika Bwana” wakiangalia manufaa ya watumwa wao. Kwa hiyo wote wawili, mtumwa na bwana, wako sawa katika kuwa na Bwana mmoja asiye na upendeleo.

6:10-20 <u>Vita ya Kikristo</u>

Paulo ameufikia mwisho wa Waraka. Limebaki neno moja la maana. Lazima waumini waonywe kwamba wamo vitani. Wakitaka kuwa upande wa Mungu anapotekeleza makusudi yake makuu ya “kujumlisha vitu vyote katika Kristo” (1:10) watahitaji kuwa hodari na kusimama imara. Kwa nini? kwa sababu kuna adui mkuu wa makusudi makuu ambayo hujitahidi pamoja na rafiki zake kuharibu kabisa na kuzuia kabisa shughuli zote za Mungu katika utekelezaji wa mapenzi yake. Wale wote ambao wamejitoa kwa Mungu na Bwana Yesu wameingizwa katika mapenzi ya Mungu, na katika kuingizwa wameingizwa pia katika vita iliyopo kati ya Kristo na Shetani. Paulo alitoboa wazi kwamba kushindana kwao si juu ya wanadamu bali ni juu ya Shetani, na falme na mamlaka za giza, na mapepo mabaya katika ulimwengu wa roho. Yaani ni juu ya enzi zile zisizoonekana. Enzi hizo zina nguvu, enzi hizo zi ovu, enzi hizo ni za giza, hazipendi nuru wala haziji kwenye nuru. Zinaongozwa na Shetani. Yeye na enzi zake zimedai madaraka na utawala juu ya ulimwengu (Yn.12:31; 14: 30: 16:11; 2 Kor.4:14; 1 Yoh.5:19; Lu.22:53; Rum.13:12; Kol. 1:13; Mt.4:8- 9). Kweli Kristo amezishinda ila bado hazijakubali ushindi wake, hivyo bado zinajikaza kisabuni. Paulo amesema “mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani” enzi hizo ni za hila, Shetani anapanga mipango yake kwa werevu sana ili awadanganye watu. Hasa amefaulu kabisa kama akimshawishi mtu aamini kwamba hakuna yeye. Hata Yesu alituonya juu ya mbwa-mwita kujiingiza kwenye kundi kama ni mwana-kondoo.

Askari wa Kirumi

Kwa hiyo jambo la kwanza ni kuwa hodari na kusimama kwa kuzitegemea nguvu za Bwana. Katika 1:19 Paulo amekwisha kusema kwamba waumini wameshirikishwa nguvu ileile iliyomfufua Bwana Yesu kutoka kwa wafu. Halafu ni kuukaza msimamo wetu, kuwa thabiti. Ndipo ni kuzivaa silaha ambazo Mungu ameziweka kwa ajili yetu, silaha zitoshazo kwa vita hiyo. Kwa vyovyote wasijitegemee katika vita hiyo. Mtu atathubutu kujitegemea ikiwa atakosa kuhesabu nguvu za adui zake. Silaha zina Mungu ila ni juu yetu kuzivaa.

Bila shaka Paulo hali amefungwa minyororo na askari alizoea kuona jinsi walivyovaa na kwa mfano wao alifundisha jinsi impasavyo Mkristo, askari wa Kristo, kuvaa. Kwanza alisema “simameni, hali mmejifunga kweli viunoni”. Siku zile mtu alivaa kanzu ndefu, na kufunga nguo kwa mshipi ili nguo zisimzuie katika shughuli zake. Pia alifungia upanga wake kwa mshipi. Askari aliweza kutembea bila shida. Ukweli wa namna gani? Je! ni ukweli wa Injili? Ndiyo Kwa sababu kwa ukweli wa Injili mtu atalindwa na mafundisho ya uongo na uongo za Shetani, atasimama thabiti katika mashambulio yote ya dini na filosofia na mawazo yaliyopotoka. Pamoja na hayo ukweli waweza kuwa hali ya unyofu na uaminifu. Hivyo mtu hatatikiswa na mashtaka ya uongo.

Silaha nyingine ni dirii ya haki kifuani. Hapo tena twaweza kumaanisha kwa njia mbili. Kwanza, haki kama kipawa cha kuhesabiwa haki. Mtu kusamehewa dhambi zake na kuvikwa haki ya Kristo, na kwa mtu huyo hamna tena hukumu ya adhabu, hamna mashtaka yawezayo kusimama mbele za Mungu (Rum 8:1; 33-34) Pia yaweza kuwa tabia ya mtu, uaminifu, unyofu. Mtu wa tabia hizo hatasikia shida anaposhtakiwa makosa yasiyo kweli, atakuwa na nguvu ya dhamiri safi ambayo ni msaada mkubwa anaposhambuliwa na adui zake.

Silaha nyingine ni “kufungiwa miguu utayari tupatao kwa Injili ya amani”. Maneno hayo yana maana gani? Huenda ni utayari wa kutoa Habari Njema. Au ni mtu kusimama imara kwa kuiweka miguu yake katika msingi imara wa Injili, ili asiteleze, awe salaam. Picha ni ya kuvikwa viatu vya nguvu viwezavyo kusaidia mtu kusimama na kutembea bila shida. Injili ni mfano wa miguu iliyovikwa hivyo. Shetani huichukia Injili sana.

Ndipo silaha nyingine ni ngao ya imani. Maneno “zaidi ya yote” yanaonyesha umuhimu wa silaha hiyo. Siyo kusema twaweza kuvaa silaha kadha tu, ila kwa ngao mtu huulinda mwili mzima. Maana ngao iliyotajwa ni ile kubwa, ndefu. Kwa imani mtu aweza kuzima mishali yote ya adui, mishale hiyo Paulo ameeleza ni “yenye moto” mikali, mishale ya kuumiza na kujeruhi. Imani ni msaada mkubwa katika mashambulio yote ya adui, maana Shetani hufanya juu chini kuwafanya waumini wakate tamaa, kuona mashaka na kuacha kumtumaini Mungu na kumfuata Bwana Yesu kwa uaminifu.

“ipokeeni chapeo ya wokovu” Wokovu ni kipawa cha Mungu, mtu aliyeokolewa na Bwana amesamehewa na kuhesabiwa haki. Kwa ujuzi wa binafsi amejitoa kwa Yule ambaye alitoa maisha yake mpaka Kufa kwa ajili yake. Kwa kawaida chapeo ilitengenezwa na chuma au shaba, nayo ililinda kichwa cha mtu, sehemu ile ya thamani sana.

Upanga wa Roho ni kama silaha ya kujilinda, pia ni silaha ya kushambulia. Upanga wa Mkristo ni Neno la Mungu, ni “wa Roho” kwa sababu kwa Roho Mtakatifu mtu huchomwa moyoni kwa Neno la Mungu. Roho na Neno huandama pamoja, kwa hiyo mtu anapolitumia Neno la Mungu kwa halali,

hakika Mungu Roho huwa pamoja naye (Ebr.4:12) Twakumbushwa jinsi Bwana Yesu alivyoyashinda majaribu yake kwa kulitumia Neno la Mungu akisema mara tatu “imeandikwa” (Mt.4:1-10).

Iwapo lugha ni ya vita silaha zenyewe, kweli, haki, amani, imani, Neno la Mungu huwa tofauti sana na silaha za kawaida. Ni silaha zisizoonekana, hazimtishi mtu wala kumwogofya, wala hazimtengi avaazo na wenzake. Ila tunapozivaa, hakika, ni silaha za ajabu, zina nguvu, nguvu ya Mungu.

Kisha watazivaa silaha zote hali wamedumu katika maombi. Katika kushirikiana kwa ukaribu sana na Mungu na katika hali ya kumtegemea kwa kila hali na kumwendea kwa mahitaji yao yote, basi watashinda katika vita juu ya enzi zote za giza. Haitoshi kuvaa silaha tu, wala haitoshi kuomba tu, inayotakiwa ni kuvaa silaha na kuomba daima. Mkristo hana budi kudumu katika maombi, kuomba kila wakati, tena “katika Roho” kwa kuongozwa na Roho, ili maombi anayoyaomba yawe yamepatana na mapenzi ya Mungu. Hasa kwa sababu waumini ni familia moja, wapaswa kuwaombea wenzao wa kila mahali. Hoja kubwa ya Waraka ni umoja wao, na umoja huo hutiwa nguvu kwa wote kuwa na mzigo wa kuombeana. Wakeshe na wadumu katika maombi. Halafu Paulo aliwaomba wamkumbuke yeye katika maombi yao, alisikia haja ya msaada wa maombi yao, na katika kila Waraka aliouandika alikaza jambo la kuombeana. Alitaka waombe nini kwa ajili yake? hakusema waombe ili afunguliwe, la! Hasa alitaka aombewe kupewa ujasiri wa kunena habari za Kristo. Pengine alijaribiwa anyamaze ili asiwachokoze wale waliokuwa wamemfunga, maana kesi yake ilikuwa bado haijasikiwa. Tena aseme habari za Kristo kwa hekima. Kwa hiyo Paulo hakuona kwamba yeye ni nje ya vita ya Injili, alitaka uhuru wa kuihubiri Injili si uhuru wa kufunguliwa. Hapo twajifunza unyenyekevu wa Paulo. Kweli alikuwa kiongozi hodari, hata hivyo, alisikia haja ya maombi ya Wakristo wenzake, wala hakuona aibu ya kuikiri haja hiyo.

6:21-24 Ujumbe wa mwisho na salaam za kuagana

Paulo aliufunga Waraka na salaam za kibinafsi. Katika sehemu kubwa ya Waraka Paulo hakutaja mambo ya kibinafsi ama ya kwake au ya wasomaji wake. Mambo makuu yaliyozungumzwa yaliwahusu waumini wote zaidi ya wale wa Efeso tu.

k.21-23 “basi, ninyi nanyi mpate kuzijua habari zangu ni hali gani, Tikiko atawajulisha mambo yote”. Paulo alitaka wajue habari za kweli juu yake. Alikuwa kifungoni, na wengi walikuwa na wasiwasi juu yake (3:13) hasa kujua kesi yake imekuwaje. Kwa hiyo Paulo alimtuma na Waraka huo pamoja na Waraka kwa Wakolosai na kwa Filemoni (Kol.4:7-9) Tikiko alikuwa mtu wa Asia, pengine wa Efeso (Mdo.20:4: Tit. 3:12 ; 2 Tim.4:12). Paulo alimtaja kwa lugha ya mapenzi akimwita “ndugu mpendwa” na “mhudumu mwaminifu katika Bwana” Inaonekana Paulo alimtegemea sana na kumtuma mahali mahali kama alivyomtuma Timotheo.

k.23 Salaam hizo ni kama maombi pia (1:2) Paulo alitaja baraka kubwa tatu za maisha ya Kikristo, mambo ambayo alitajataja katika Waraka mzima. Amani na iwe kwa ndugu, hoja yake kubwa imehusu umoja wa waumini katika familia moja ya Mungu, walioitwa kuuhifadhi umoja wao katika amani (4:3). Ndipo Paulo ameweka upendo pamoja na imani. Bila imani mtu hashirikiani na Mungu na bila kushirikiana na Mungu kibinafsi hamna upendo. Upendo unatoka kwa imani katika Kristo. Asili ya mambo ni Mungu Baba na Bwana Yesu Kristo.

k.24 Ombi la mwisho ni kwa neema, ambayo Paulo amerudia kutaja mara nyingi katika Waraka (1:6, 7: 2:5, 7, 8; 3:2, 7, 8: 4:7) “kwa wote wampendao Bwana wetu Yesu Kristo” si kana kwamba Paulo alitaka kuweka nje wengine ila bila itikio la upendo mtu hawezi kuonja neema na upendo wa Mungu. Ni neema inayoendeleaendelea muda wote, ni ya thamani sana na ni ya kutunzwa sana.

MASWALI
Maswali kuhusu ujumbe wa Waraka mzima:

1. *Ni nini Makusudi Makuu ya Mungu?*

2. *Mungu amefanya matendo gani ili Makusudi yake yatekelezwe?*

3. *Kwa upande wetu sisi twapaswa kufanya nini katika kuendeleza makusudi hayo?*
   (a) Eleza kwa kusema juu ya jinsi ya kuishi?
   (b) Eleza kwa kusema juu ya tabia zinazotakikana?
   (c) Eleza kwa kusema juu ya maisha ya nyumbani, kazini nk

4. *Kwa kutazama Kanisa na hali yake unaona nini ambayo unafikiri ni kinyume cha makusudi ya Mungu?*

5. *Katika Kanisa na mahali ulipo kuna farakano au shida au ubaguzi unaohitaji matengenezo? Wewe mwenyewe unatoa mashauri gani kwa Kutibu shida hizo?*

WARAKA KWA WAFILIPI

YALIYOMO

UTANGULIZI

(a) Mji wa Filipi
(b) Kanisa la Filipi
(c) Mwandishi
(d) Mahali na tarehe ya kuandikwa
(e) Sababu na Shabaha za Waraka
(f) Hali ya Waraka

UFAFANUZI

1: 1- 2 Salaam
3- 8 Shukrani na Tumaini
9-11 Ombi kwa ajili ya wasomaji wake
12-18 Matokeo ya Paulo kufungwa
19-26 Mbele yake - Kuishi au kufa
27-30 Wito wa kuishi kama istahilivyo Injili

2: 1- 4 Wito wa kuwa na umoja na unyenyekevu
5-11 Kristo na kielelezo chake
12-18 Wokovu uwe na matokeo kiutendaji
19-30 Mipango ya kuwahusu Timotheo na Epafrodito

3: 1 Furaha
2- 3 Onyo juu ya Wayahudishaji
4- 6 Historia ya Paulo katika dini ya Kiyahudi
7-17 Paulo aliukaza mwendo ili amjue Kristo
18-21 Onyo juu ya “adui za msalaba wa Kristo”

4: 1- 3 Umoja, na ombi kwa Euodia na Sintike
4- 7 Furaha, Upole, Maombi, Shukrani, Amani ya Mungu
8- 9 Kuwaza mambo mema
10-20 Shukrani za Paulo kwa vipawa walivyomletea
21-23 Salaam za kuagana

UTANGULIZI

(a) Mji wa Filipi

Mji ulianzishwa KK.360 na Filipo wa Makedoni, baba wa Iskanda Mkuu. Kabla ya kujengwa na Filipo palikuwepo na mji wa zamani sana ulioitwa Krenides. Filipo aliutambua uzuri wa mahali pake kijiografia maana ulikuwa kwenye njia ya kutoka Ulaya mpaka Asia, hivyo ulitawala usafiri wa kutoka magharibi mpaka mashariki. Baadaye Mji wa Filipi ulianguka mikononi mwa Warumi KK.168 halafu uliwekwa katika Jimbo lao la Makedonia. Katika KK.42 maaskari wa Kirumi waliotumika muda mrefu katika jeshi walipewa nafasi ya kuishi pale kama wakoloni. Walipewa mapendeleo ya kuishi kama Warumi walivyoishi Rumi penyewe, wakitumia lugha ya KiLatini na kuvaa mavazi ya Kirumi na kufuata sheria na mipango na kuyatumia majina ya vyeo vya Kirumi. Baadaye Warumi waliweka vikundi vya namna hiyo katika miji ya maana kusudi wailinde amani ya sehemu ile na kutunza usalama wa njia za usafiri na biashara. Katika Matendo l6:l2 Luka alieleza mji kuwa "mkuu katika jimbo lile na mahali walipohamia Warumi". Hasa Thesalonike ulikuwa mji mkuu wa Jimbo la Makedonia, ila kwa hali ya uzuri wake Filipi ulipata sifa ya kuwa mkuu.

(b) Kanisa la Filipi

Paulo, Sila na Timotheo walifika Filipi kwa mara ya kwanza baada ya Paulo kutokewa na maono usiku alipokuwa Troa (Mdo.l6:9ku) Luka alikuwa pamoja nao, tazama neno "tu..." (16:10,11,12,13). Kuna mapokeo yasemayo kwamba Luka alikuwa mwenyeji wa Filipi. Ila hatuna uhakika, maana mapokeo mengine husema alikuwa mzaliwa wa Antiokia wa Shamu (Mdo.11:27). Walikuwa katika Safari kubwa ya pili ya Injili iliyofanywa na Paulo na wenzake kati ya BK.49-52 (Mdo 15:40-18;22).

Kawaida ya Paulo ilikuwa kuanzia penye sinagogi, ila inaonekana hawakuikuta sinagogi pale Filipi ila siku ya sabato, kando ya mto, walikutana na wanawake kadha. Basi Paulo na wenzake waliwahubiri habari za Kristo, na mmoja wa wale waliosikiliza, jina lake Lidia, akaujali sana ujumbe wa Paulo, akampokea Bwana Yesu moyoni. Kwa asili alitoka mji wa Thiatira, katika Jimbo la Asia, yawezekana alikuwa amekuja Filipi kwa ajili ya biashara yake ya kuuza rangi ya zambarau. Alikuwa "mcha Mungu" mwongofu wa dini ya Kiyahudi. Mwanamke mwingine alitolewa pepo wa uaguzi na Paulo, huenda yeye naye alimwamini Kristo. Twajua mkuu wa gereza na nyumba yake waliokolewa. Ni hao, pamoja na wengine waliokuwa washiriki katika Kanisa la Filipi, walioandikiwa barua hiyo.

(c) Mwandishi

Ni Mtume Paulo. Zipo dalili nyingi katika Waraka kwamba yeye ndiye mwandishi. Kuanzia kwa salaam mpaka kutaja habari za kufungwa kwake, tumaini lake la kufunguliwa, na uhusiano wa ukaribu na wale walioandikiwa, ushuhuda wote unaonyesha kwamba ni Paulo aliyeuandika Waraka huo.

(d) Mahali na Tarehe ya Kuandikwa
Wakati wa kuandika Paulo alikuwa mfungwa. Lakini wapi? na wakati gani? Wataalamu wamejadili neno hilo kwa kirefu. Baadhi wameona Waraka uliandikwa wakati Paulo alipofungwa Kaisaria kama BK.58 (Mdo.23:33). Shida katika kulipokea wazo hilo ni kwamba inaonekana mashtaka juu yake hayakuwa na uzito kiasi cha Paulo kusema kwamba mbele yake ni kufa au kuishi. Pale Kaisaria Paulo aliweza kuipeleka kesi yake mbele, tofauti na picha tuliyo nayo katika Waraka. Baadhi huwaza Efeso, ila hatuambiwi katika Kitabu cha Matendo au mahali pengine kwamba Paulo alifungwa pale, na ikiwa alifungwa ni vigumu kufikiri alifungwa kwa muda mrefu. Kwa kweli wazo ambalo lina nguvu zaidi ni kwamba ni wakati alipofungwa Rumi kwa miaka miwili baada ya kumaliza Safari kubwa ya tatu ya Injili na kukamatwa Yerusalemu, halafu kupelekwa Rumi. Kwa hiyo tarehe ya kuandikwa ni kama BK.60-62 (Mdo.28:16,30,31). Alitaja "askari" (Flp.1:13) na "nyumbani mwa Kaisari" (Flp.4:22) yote hayo yatuelekeza kuwaza alikuwa Rumi.

(e) Sababu na Shabaha za Waraka
Alitaka kuwafahamisha hali yake na kuwatia moyo kwamba kufungwa kwake hakuizuia Injili (1:12-16). Pamoja na hayo alitaka kuwajulisha mpango wa kumtuma Timotheo kwao na tumaini lake la kuja mwenyewe baadaye (2:19- 24).

Aliona aliwajibika kuwaeleza juu ya kumrudisha Epafrodito kwao. Epafrodito alitumwa na Wafilipi kwa Paulo akimletea msaada kutoka kwao. Inaonekana wao walifikiri ataendelea kukaa na Paulo na kumhudumia. Lakini aliugua vibaya sana, akataka kurudi kwao, maana alipata kufahamu kwamba wao wamejua habari za kuugua kwake, aliona watakuwa na wasiwasi juu yake. Basi Paulo alimrudisha, ila hakutaka wamwaze vibaya eti! amemwacha; alitaka wampokee vizuri (2:25).

Kutokana na habari zilizomfikia Paulo alipata kujua kwamba ugomvi umeanza kati ya baadhi ya waumini na Paulo alitaka kuitibu shida hiyo mapema, ndiyo sababu aliwaomba waishi na kutenda katika Umoja wa Roho (1:27; 2:2ku. 4:2ku.)

Pia aliwaonya juu ya watu waliokaza Tohara na Torati na kutegemea sana mambo ya nje. Huenda walikuwepo na kuwasumbua Wafilipi au Paulo aliona hatari ya namna hiyo itatokea kwao. Alitoa ushuhuda mkali jinsi Torati na Tohara visivyoweza kumwokoa mtu (3:3-11).

Aliona ipo hatari ya mafundisho mengine ya kuitikisa imani yao. Huenda baadhi ya waumini walifikiri kwamba inawezekana kuifikia hali ya "ukamilifu" wangali hapa duniani, yaani waifikie hali ya kutokutenda dhambi. Iwapo kila wakati Paulo aliwasihi waumini wa kila mahali waulenge ukamilifu, na "wakamilike" lakini hakufundisha kwamba inawezekana watu wakamilike

kabisa katika maisha ya hapo duniani (3:13-16). Paulo alitaka kuwatia moyo wayakabili mateso na magumu, wawe na nia na moyo wa kumfuata Kristo na kumtegemea katika yote (1:17-30; 2:12-18; 3:17-21; 4:4-9). Alitoa shukrani kwa vipawa walivyomletea (4:10, 14-18) Huenda vipawa hivyo vilimfikia zamani na ya kuwa alikwisha kutoa shukrani ila aliona vema ashukuru tena jinsi walivyomfadhili.

(f) Hali ya Waraka

Waraka una hali ya kibinafsi kuliko nyaraka zote zingine. Paulo alitaja hali zake na mawazo na matumaini yake, akifunua yaliyomo moyonoi mwake. Pia aliuonyesha na kuukaza uhusiano wa ukaribu sana uliopo kati yake na wao. Aliwataja watu mbalimbali kwa majina. Waraka umejaa shukrani na kuyakaza mambo kama furaha, (imetajwa mara 16) ushirikiano (1:5-7; 2:1-4); unyenyekevu (2:3,5-11). Katika Waraka twajifunza jinsi Paulo alivyokuwa amejitoa kabisa kwa Yesu Kristo na nia yake ya kumjua Kristo zaidi na zaidi, pamoja na kumtangaza Kristo kwa wengine (3:7-14 1:20) Pia twaona jinsi alivyoridhika na hali zote, hakusita wakati wa kupatwa na upungufu wa mahitaji na magumu mradi Kristo amtie nguvu. Alikuwa tayari kuyastahimili yote ili Kristo atukuzwe (4:11-13).

UFAFANUZI

1: 1-2 Salaam

Salaam za Paulo zafuata kawaida yake katika Nyaraka zake na ya siku zile. Kwanza alijitaja pamoja na Timotheo. Timotheo alikuwa naye alipoihubiri Injili kwa mara ya kwanza pale, na Paulo alimtuma kwao baadaye (Mdo.19:22) na alitazamia kumtuma tena (2:19ku). Alimweleza Timotheo na yeye kuwa "watumwa wa Yesu Kristo" watu waliojitoa kufanya mapenzi ya Bwana wao Yesu Kristo, kiasi cha kuweka kando hiari yao na matakwa yao wenyewe na kujihesabu kuwa mali ya Kristo. Walikuwa watu wenye heshima ya hali ya juu, maana walichaguliwa na Mungu na kupewa mamlaka ya kumtumikia. Paulo hakuona haja ya kuikaza mamlaka yake ya KiMitume alipowaandikia Wafilipi kwa sababu wao walimpokea hivyo bila shida. Uhusiano wake na wao ulikuwa mzuri sana, tazama lugha ya 4:1 "ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu na taji yangu." maneno hayo yaonyesha uhusiano wa upendo mwingi. "kwa watakatifu wote katika Kristo Yesu walioko Filipi" Maneno hayo yawahusu waumini wote, si wachache walio bora zaidi. Jina hilo latumika katika Agano Jipya lote kuwaeleza Wakristo. Halitumiki kwa mtu mmoja tu. Maana ya neno ni "waliotengwa" waumini ni watu waliojitenga na maovu ili wawe na maisha tofauti na wengine. Kwa upande wa pili wametengwa kwa ajili ya Mungu na utumishi wake. Maisha yao ni katika Yesu Kristo, wameungana na Kristo katika Kufa na Kufufuka Kwake na kwa sababu hiyo waweza kuitwa "watakatifu" (1 Kor. 1:3). Paulo alizoea sana kusema

“katika Kristo” kwake kuwa “katika Kristo” ni kiini cha imani ya Kikristo. “pamoja na maaskofu na mashemasi” Tusiwawaze maaskofu kama walivyo siku hizi. Wakati ule Kanisa halikuwa na mpango halisi wa vyeo. Katika kila shirika watu wa palepale walipewa uongozi, nao waliitwa “wazee” au “maaskofu” au “waangalizi”. Walikuwa kundi, hatuoni kama mmoja aliwekwa juu ya wenzake. Hali hiyo ilitokea baadaye. (Mdo.20:17,28). Mashemasi walikuwa watu waliohusika na mipango kama tunavyoona katika Matendo 6. Kwa nini awataje? maana hakuwataja tena katika Waraka. Yawezekana hao waliongoza mkusanyo wa msaada ulioletwa na Epafrodito (2:25; 4:18).

k.2 “Neema” ni kibali cha Mungu kisichotegemea uzuri wa mtu na asili yake ni upatanisho uliofanyika na Yesu Msalabani. Mtu hupokelewa na Mungu kwa mikono miwili bila masharti. Kwa neema Mungu humkubali mtu awe mtumishi wake. "Amani" ni zaidi ya kutokuwapo kwa vita au shida. Ni tokeo la upatanisho nayo inaandama na neema kama tunda lake. Maana ya amani ya namna hiyo ni "uzima" mtu huwa na mema yote. Neema na amani vyatoka kwa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo. Ni baraka kubwa kwa Wakristo. Twaona Yesu Kristo amewekwa sawa na Mungu Baba kuwa asili ya baraka hizo.

1:3-8 Shukrani na Tumaini
Paulo alijaa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya waumini wote wa Filipi. Aliwakumbuka daima katika sala zake, tena kwa furaha. Twaona mkazo juu ya “wote” na juu ya “furaha”. Iwapo alikuwa mfungwa alisikia furaha sana kwa mambo yaliyohusu maendeleo ya Injili. Ni nini hasa iliyompa kufurahi na kumshukuru Mungu?

k.5 Ni kwa sababu ya ushirika wao, si katika Kristo tu, bali pia katika kuieneza Injili. Inaonekana kwamba tangu walipoipokea Injili waliunga mkono kazi za kuieneza, wakiwa na mzigo wa kuona Injili iendelee kuhubiriwa na kuaminiwa. Wakati wa shida walimletea Paulo msaada. Dalili moja ya upendo kwa Injili ni utayari wetu wa kutoa mali yetu kwa ajili yake na kwa kujitoa ili Kristo atangazwe.

k.6 Paulo alikumbuka sana siku zile za kwanza alipofika Filipi na kuihubiri Injili, na itikio la watu mbalimbali waliompokea Bwana Yesu. Alijua hakika ni Mungu aliyefanya kazi miongoni mwao (Mdo.16:14 Bwana alifungua moyo wa Lidia) Paulo hakudai kuwa mwanzilizi wa Kanisa lile.

Wala Mungu hakuacha kufanya kazi baada ya wao kuondoka, walizidi kukua kiroho, na Paulo aliamini kabisa kwamba Mungu ataendelea kufanya kazi mioyoni mwao. Twaona hekima ya Paulo kikazi, alijua haitoshi kupanda mbegu tu, mimea huhitaji kutunzwa hadi siku ya mavuno. Shabaha ya Paulo ilikuwa kuleta Wakristo wenzake pamoja na yeye mwenyewe mbele za Kristo katika hali ya ukamilifu, wasiwe na lawama, wala wasiwe na haya katika siku ile (Kol.1:28).

k.7-8 Paulo aliendelea kuwakumbuka wakati alipofungwa, nao vilevile walimkumbuka yeye na kumletea msaada. Mzigo wa Paulo na mzigo wao ulikuwa mmoja, Injili na maendeleo yake. Katika hilo waliendelea kushirikiana. Ndiyo sababu Paulo aliwapenda sana, walikuwa “moyoni mwake”. Aliona amewajibika kuwaombea iwapo kimwili yu mbali nao, lakini katika neema ya Kristo wako karibu kiasi cha kuwa “moyoni”.

k.8 Alisema Mungu ni shahidi wa shauku iliyomo moyoni mwake, shauku yenye asili katika moyo wa Kristo. Maana yake alijisikia sawa na Kristo anavyojisikia kwa watu wake. Alisukumwa na upendo wa Kristo (2 Kor.5:14). Bila shaka hakupenda kutengwa nao lakini hakuwa la kufanya. Iliyobaki ni kuwakumbuka, kuwaombea, kuandika barua, na kutuma watu.

1:9-11 Ombi kwa ajili ya wasomaji wake

Aliomba upendo wao uzidi sana, na katika upendo huo wawe na hekima, waishi kwa busara ili waamue lifaalo na lisilofaa. Pia ufahamu wao wa Mungu uwaongoze ili watambue na kuzifuata njia bora za kuishi kwa ushirikiano mwema. Yaani upendo wao usiwe kitu cha juujuu, usio na kina. Huenda Paulo alikuwa akiwaza maelekeo yao ya kugombana na kutokunia mamoja (2:2-4; 4:2-3).

k.10 Upendo wa namna hiyo ulioombwa na Paulo utatokeza watu wa kukubali yaliyo mema, watu wa kweli, watu safi, na watu wasio na lawama. Kwa jumla, watu walio tayari kwa Kuja Kwake Bwana Yesu. Watu ambao maisha yao yote yamejaa mema na matendo ya haki, hali wamewezeshwa na Bwana Yesu, kusudi Mungu atukuzwe. Paulo alijua kwamba maisha ya namna hiyo hayawezekani nje ya neema ya Kristo.

1:12-18 Matokeo ya Paulo kufungwa

k.12. “nataka mjue...” Wakristo wengi walioishi mbali na Rumi walikuwa na wasiwasi walipofahamu ya kuwa Paulo amefungwa. Bila shaka mawazo yao ya kwanza yalikuwa kwa ajili ya Paulo mwenyewe, hali yake ya kimwili, afya yake, utunzaji kwa upande wa nguo na chakula, na dhiki zake. Pia haikosi waliwaza jinsi alivyojisikia kwa kutokuruhusiwa kwenda hapa na pale kwa ajili ya Injili. Pamoja na hayo ya kumhusu Paulo binafsi bila shaka mawazo ya wengi yaliihusu Injili na maendeleo yake, maana wote walitambua ya kuwa Paulo ndiye hasa nguzo katika kuitangaza na kuitetea, alikuwa mwendeshaji hodari katika kuipeleka kila mahali, pamoja na kuwa kama “baba” wa waumini katika makanisa yaliyopandwa kutokana na safari zake. Paulo alitaka wajue hali yake binafsi, pamoja na maendeleo ya Injili. Paulo hakutaka watu wamsikitikie kupita kiasi kwa hiyo alisema machache tu juu ya mateso yake, alificha shida zake katika maneno “mambo yote yaliyonipata”.

k.12 Aliwaambia neno jema la kuwatia moyo. Licha ya Injili kuzuiliwa, kifungo chake kimekuwa sababu ya Injili kupata nafasi ambayo bila kufungwa kwake isingaliipata.

k.13 Imewafikia askari wa Kirumi na wengine. Imekuwaje askari wameisikia Injili? Paulo alifungwa na mnyororo na kulindwa na askari (Mdo.28:30; Efe.6:20). Alipofika Rumi alipewa nafasi kukaa katika nyumba na kuwapokea watu. Bila shaka kila askari aliyemlinda alipata kuyadaka mazungumzo ya Paulo na wenzake, mazungumzo kumhusu Kristo. Pia Paulo angalitumia nafasi yoyote ya kuzungumza na kila askari aliyemlinda na kumshuhudia. Pamoja na hayo watu wote walifahamu kwamba Paulo amefungwa kwa ajili ya kumfuata Kristo. Kwa njia hizo habari za Kristo zilienea na baadhi waliuitika wito wa kuamini. Tokeo lingine lilikuwa Wakristo wa sehemu zile kutiwa nguvu na kupata ujasiri wa kumshuhudia Kristo kuliko hapo nyuma. Kwa hiyo kufungwa kwake kumeleta faida si hasara kwa upande wa Injili na maendeleo yake.

k.15-18 Neno kubwa na la maana lilikuwa Kristo kuhubiriwa. Hata hivyo wengine hawakufanya kwa nia safi. Inaonekana walimwonea Paulo wivu, walitaka kuongeza shida zake. Lakini Paulo hakukubali kuudhika kwa ajili hiyo, alifurahi sana kwamba kwa nia njema na kwa nia mbaya Kristo alihubiriwa, na kwa sababu hiyo hana budi kufurahi. Hatuambiwi hao watu wasiokuwa na nia safi walikuwa watu gani? huenda ni Wakristo wa sehemu zile, watu walioamini kabla ya Paulo kufika, nao hawakufurahi kuona Paulo aliye mfungwa amekuwa mbele na macho yote yamemwelekea, hivyo nafasi yao ya kutangulia na kuwa na sauti ilipungua. Ila hatuna hakika ilikuwa hivyo. Liko wazo lingine la kufikiri kwamba hao watu walitumia jambo la Paulo kufungwa kuwa sababu ya kuwalaumu sana Wayahudi waliosababisha kukamatwa kwake Yerusalemu, na ya watawala waliokubali kusukumwa na Wayahudi. Lakini Paulo hakuona kwamba kufanya hivyo kutamsaidia, huenda kutazidisha shida zake. Si wote waliompenda Paulo.

Kwa upande wa pili walikuwepo wengine waliothubutu kuwa hodari zaidi wakiunga mkono nia ya Paulo kuihubiri Injili. k.18 Paulo hakutaka kuingia majadiliano, aliamua neno moja la kufurahi kwa sababu Injili ilihubiriwa.

1:19-26 Mbele yake – Kuishi au kufa

Paulo alitegemea sana msaada wa kibinadamu, maombi ya rafiki zake pamoja na msaada utokao kwa Mungu, kuruzukiwa Roho Mtakatifu. “kuruzukiwa” kwaleta maana ya ukarimu wa msaada wa Mungu, msaada ufaao, msaada utoshao. Potelea mbali matokeo ya kufungwa kwake yatakuwa nini alitawaliwa na “tamaa” ya Kristo kutukuzwa, kwa njia ya yeye kusimama imara, kama ni kuuawa, apokee hukumu hiyo kwa ujasiri na tumaini; kama ni kuishi aishi kwa kujitoa kabisa, asiwe na sababu nyingine ya kuishi isipokuwa ile ya kumtumikia Kristo.

Paulo hakujua kesi yake itakavyokuwa. Katika sehemu hiyo ameweka wazi mawazo yake kuhusu kufa na kuhusu kuishi. Kwa ndani aliamini mambo yatatokea vizuri.

Kwa upande mmoja hakusita kufa, kwa kweli angalikaribisha kufa, maana taabu zake zote zingalikwisha, angalikwenda kwa Kristo, jambo bora zaidi. Alipoiwaza Injili na mahitaji ya Wakristo na ya Kanisa aliona amewajibika kuishi na kuendelea katika utumishi wake. Alipotazama haja za Kanisa aliona ni vema asiondolewe na kuwaacha waumini wakati ule.

k.23 Alishuhudia jinsi alivyosongwa kati ya hayo mawili, ila twaona pia yu tayari kuishi. Alitawaliwa na mzigo wa kiuchungaji si kwa kujipenda mwenyewe na mwishowe alielekea kuonyesha nia ya kuishi, na kuwaona tena.

1:27-30 Wito wa kuishi kama istahilivyo Injili
Baada ya kusema juu ya mambo yake mwenyewe Paulo aliendelea kusema juu ya mambo yaliyowahusu Wafilipi. Kwanza, wapaswa kuishi maisha yaliyodaiwa na Injili. Jambo kubwa si kuishi au kufa kwa Paulo, wala kama atakuwa mbali nao au karibu nao, ila jambo kubwa ni jinsi iwapasavyo daima kuishi maisha mema yapatanayo na Injili, wasingojee mpaka amekuja na kuwaona na kutengeneza shida ya fitina na ugomvi kati yao.

Inaonekana walikuwa wakiteswa kwa ajili ya imani yao, adui fulani waliwashambulia. Paulo aliwaita wasimame imara, tena wawe na umoja katika kuishindania Injili. Umoja ndio nguvu. Aliwaambia “wamepewa kuteswa” neno la ajabu, lakini si neno geni katika mafundisho yake; taz. Mdo.14:22; 1 The.3:3; 2 Tim. 3:12; kwa sababu ni ishara thabiti ya kuwa watoto wa kweli wa Mungu. Alisema kwamba mashindano waliyo nayo yafanane na yale aliyoyapata na anayoendelea kuyapata. Wamo pamoja naye katika vita ya Injili. Wahesabu ni heshima kubwa kuteswa kwa ajili ya Kristo.

M A S W A L I

1. *Kutokana na sura hii ya kwanza mmejifunza nini kuhusu hali zinazotakiwa katika watumishi wa Mungu?*

2. *1:21-26 Ni nini hasa inayoonesha kwamba Paulo alikuwa amejitoa kwa Kristo, pia kwa Wafilipi?*
   Je! Mtu aweza kujitoa kwa Kristo bila kujitoa kwa watu? Eleza.

2: 1-4 Wito wa kuwa na umoja na unyenyekevu
Sura hii inaanza na neno “basi”. Wito wa Paulo umefuata habari za mateso yaliyotajwa katika 1:27. Paulo aliwaita Wakristo wa Filipi kuzidi katika umoja kwa njia ya kunyenyekeana, kila mmoja asiyawaze wala asiyeangalie mambo yake mwenyewe tu.

k.1 Maneno “ikiwako”.. “yakiwako”.. “ukiwako” si maneno ya mashaka bali maana hasa ni “kwa kuwa iko..uko...yako...” Msingi wa wito wa Paulo ni katika mambo ya kiroho si katika hali za kibinadamu. Kwanza ametaja “faraja katika Kristo” ama aliwaza kielelezo cha Kristo au nia na wito wa Kristo kwa watu wake kuwa na umoja (Yn.17:22). Ni nia ya Kristo watu wake wawe na umoja, ni kitu anachotaka. Ndipo jambo la pili la msingi ni “mapenzi”. Kristo amewapenda nao wapaswa kuuonyesha upendo huo kwa wengine. Halafu jambo la tatu ni kwamba wote wanaye Roho, wameshirikishwa Roho, kwa hiyo budi waishi katika ushirikiano. Kisha Paulo aliwakumbusha kwamba wote wamehurumiwa na Mungu, wote wamezionja rehema zake, kwa hiyo wapaswa kuwahurumia wengine kama walivyohurumiwa.

Hivyo furaha ya Paulo itazidi hasa akisikia kwamba wamesimama pamoja, bega kwa bega, hali wakipendana na kushirikiana vizuri.

k.2 Twaona mkazo wa umoja jinsi Paulo alivyotaja neno hilo mara nne katika kifungu hicho. “nia moja” “mapenzi mamoja” “roho mmoja” halafu “kunia mamoja”. Maana yake wawe na lengo moja katika maisha yao kama shirika la Kikristo katika kuishi kwa kanuni za Injili, pamoja na kuisimamia, pamoja na kuieneza. Wajiunge katika shughuli za Kikristo kwa upendo bila kila mtu kuvuta kamba upande wa matakwa yake tu. Wasiwaruhusu wachache kutawala na kuamua mambo yote, wala isiwe kwamba ni baadhi tu wanaoendelea kiroho. Kanisa la pale lahitaji kusonga mbele kama kitu kimoja.

k.3-4 Kiutendaji itawezekanaje waishi hivyo? Jambo moja, waache kushindana na kugombana. Tena waache kujivuna. Kwa kujivuna mtu huwa kama “kuvimba” na katika kuvimba ni rahisi asukume au agongane na mwingine. Kwa hiyo kila waliamualo na kila walifanyalo wafanye kwa kupatana.

Siri ni katika kila muumini kumhesabu mwenzake kuwa bora kuliko yeye mwenyewe. Mtu amwangalie mwingine ili apate kutambua vipawa na nguvu yake na uzuri wake, pamoja na kuutambua udhaifu na hitilafu zake mwenyewe (Rum.12:16). Mtu asiwazewaze ya kwake tu, awe tayari kujali na kusikia ya mwenzake (Rum.15:2; 1 Kor.10:24; Gal.6:2). Kujipenda na kujiona ni adui za ushirikiano na kizuizi cha umoja.

Mtu hawezi kutembea na Kristo katika ushirikiano mwema huko ametengana na kutokupatana na wenzake. Paulo hakutoa mashauri mema tu, bali mashauri yaliyojengwa katika Kristo.

2: 5-11 Kristo na Kielelezo chake

k.5 Paulo aliona kwamba jambo lenye nguvu litakalowavuta Wafilipi ni kielelezo cha Bwana Yesu. Aliwatazamisha kwa Kristo, alichora picha ya ajabu sana, picha iliyoonyesha hatua za kutelemka kwa Kristo alipotoka juu na kuja hapa duniani, alipoweka kando utukufu wake wa kuwa Mungu na kufanyika

mwili akawa mwanadamu, kisha telemko kali sana alipouawa msalabani kama mhalifu mbaya.

Paulo aliona ya kuwa imewapasa Wafilipi wajivike nia iyohiyo ya Kristo, si mtu kibinafsi tu, hata shirika lote, nia hiyo iwe katikati yao, wote waishi kwa kunyenyekeana na kwa kutokujipenda na kutokujiona. Waikolee kabisa nia ya Kristo ili itawale kuwaza kwao, na kuishi kwao, na kutenda kwao. Wakianza kwa kurekebisha kuwaza kwao na kunia kwao shida ya kugombana na kutokunia mamoja itatibiwa.

k.6 Kwanza aliwatazamisha wamzingatie Kristo katika hali ya asili yake, katika umilele uliotangulia alipokuwa kwa Mungu, na alipokuwa Mungu (Yn.1:1ku.). Paulo aliandika “alikuwa yuna namna ya Mungu” Maana yake nini? Kristo alikuwa na hali ileile na tabia zilezile za Mungu. Kwa asili alikuwa Mungu. Alikuwa pamoja na Baba na Roho Mtakatifu, usawa wa Nafsi Tatu kuwa Mungu Mmoja. Kristo asingaliweza kuwa na hali bora na ya juu kuliko hiyo ya kuwa Mungu Mwana.

Ndipo Paulo alionyesha nia ya Kristo ya kutokujiona na kutokujipenda. Hakuona vema aushikilie huo usawa wake na Baba. Alikuwa tayari kuachana na utukufu wake na kujifanya kuwa hana utukufu. Kweli maneno hayo yaliwalenga Wafilipi na hali yao ya kugombana na mtu kujiinua juu ya mwenzake.

Pia mawazo yaenda kwa Adamu na Hawa jinsi walivyojiweka juu ya Mungu na kumwasi, Shetani aliwashawishi na kuwadanganya na ahadi ya uongo “mtakuwa kama Mungu” (Mwa.3:5). Tofauti na Kristo aliyekuwa sawa na Mungu, akaamua asiushikilie usawa huo, maana yake asiutumie kwa faida yake mwenyewe, bali ajinyenyekee kwa mapenzi ya Babake, amtii, hata mpaka kufa, ili apewe heshima ipitayo heshima zote, awekwe na Baba kuwa Bwana, na kulipata jina lile lipitalo kila jina.

k.7 Tokeo la kutokuushikilia usawa wake na Mungu lilikuwa kuishi hali utukufu wake wa asili wa kuwa Mungu usionekane. Alifanyika mwili, alishiriki hali yetu ya kibinadamu, alifanana nasi, akivuta pumzi, akibanwa na haja ya kula na kunywa, kupumzika na kupiga usingizi. Alikuwa radhi kuwa mahali pamoja kwa wakati mmoja. nk.

Hata zaidi, alishuka katika ubinadamu wake, hakutafuta kutumikiwa bali kutumika. Angaliweza kuhudumiwa na malaika maelfuelfu, lakini aliishi kwa shughuli nyingi za kufundisha, za kuwaponya wagonjwa, na kutoa pepo waliolemewa nao. Alikwenda hapa na pale bila kujihurumia. Wakati mwingine alikosa chakula na malazi, alichoka sana kimwili. Hayo yote akiwa kwa asili Mungu asiyetawaliwa na hali hizo. Wala haikutosha iwe hivyo, alishuka tena, akakubali kuwa Mtumishi Ateswaye, Dhabihu ya dhambi, Mwana Kondoo halisi

wa Mungu. Utii wa Baba ulimgharimia maisha yake hadi Kufa, aliuawa kwa kutundikwa kwenye mti, kifo kibaya mno, kifo chenye maumivu makali, kifo cha aibu sana, na kifo chini ya laana ya Mungu (Kum.21:33; Gal.3:13). Alitelemka mpaka pande za chini kabisa. Katika hatua hiyo hamna dalili yoyote ya usawa wake na Mungu, Msalabani aliachana kabisa kuushikilia usawa wake na Mungu.

Kila mara katika vifungu hivi Paulo aliwakumbusha kielelezo cha Kristo ili awavute kunyenyekea kama Bwana wao alivyofanya. Kristo alimnyenyekea Baba kwa sababu alimpenda sana sana, hakumwogopa. Pia alimnyenyekea Baba ili atukomboe sisi. Aliudhihirisha upendo wake wa ndani katika matendo hayo ya nje. Ya ndani na ya nje yalilingana.

2:9-11 Baada ya kumtafakari Kristo na kujitoa kwake Paulo aliyaelekeza mawazo ya Wafilipi kuyawaza alivyofanya Mungu. Maneno “kwa hiyo” yana maana kubwa kwa sababu yanaonyesha uhusiano mkubwa kati ya yaliyotangulia na hayo yanayofuata. Yesu aliadhimishwa mno kwa sababu alijidhili mno, ni matokeo ya kudhiliwa kwake.

Ni Mungu aliyemwadhimisha, hatua ya kwanza ilikuwa kumfufua kutoka kwa wafu, ndipo kumpandisha juu, kisha kumketisha kwenye kiti cha enzi na kumweka mkono wake wa kuume. Kwa hiyo ni wazi kwamba ilikuwa mapenzi ya Baba ajidhili hata kiasi cha kuuawa kwa ukatili mkubwa na kufa katika aibu nyingi na kwa maumivu mengi. Ni dhahiri Mungu alipendezwa na Mwana wake alipojitwisha wito wa kuwa Mtumishi Ateswaye na Mwana Kondoo halisi wa Pasaka.

Yesu alikuwa sawa na Mungu, wala hakuona aishikilie heshima hiyo, alikuwa radhi kuuacha utukufu wa asili, kujinyima uwezo wa KiMungu na kujibana katika mipaka ya uwezo wa kibinadamu. Kwa sababu hiyo, Mungu alimrudishia maradufu utukufu wake wa asili. Alimkirimia Jina lipitalo kila jina. Jina si jina la cheo bali ni heshima ya mamlaka ya hali ya juu kabisa. Akipenda asipende, kila mtu atampigia magoti na kwa ulimi wake kumkiri kuwa Bwana. Hata malaika juu, na mashetani chini lazima wawe chini yake. Wote na vyote wataukiri na kuutangaza ushindi wa Kristo. Katika Isa.45:23 nabii alisema juu ya goti kupigwa na ulimi kumkiri Mungu wa Israeli na ukuu wake. Hivyo, Kristo amerithi kiti cha enzi na kutawala pamoja na Baba yake. Hata hivyo, itakuwa kwa ajili ya utukufu wa Mungu Baba. Hakuna shida kati ya Baba na Mwana (Ufu.3:21; 1 Kor.15:28; Efe.1:10,20,22; 4:8-10; Ufu. 5:1-14 ina mafundisho hayo kwa lugha ya kipicha).

2:12-18 Wokovu uwe na matokeo kiutendaji
Iwapo Paulo katika sehemu iliyotangulia alisema makuu juu ya Kristo shabaha yake iliwahusu Wafilipi na maisha yao ya kila siku, hasa maisha ya shirika lao. Kwa kielelezo cha Kristo wauone umuhimu wa kuwa na unyenyekevu kati yao.

Alikuwa ameuonyesha utii wa Kristo kwa Baba yake (k.8) sasa aliukaza utii wa Wafilipi kwa maagizo yake. Ila hakuwaagiza kwa hali ya kiaskari bali kwa upendo wa “baba” wa imani yao akitumia maneno “wapendwa wangu". Kwa utii waliipokea Injili na kwa utii waendelee kuishi kwa kanuni za Injili. Wawe na bidii, wawe na hali ya kujali, wamche Mungu, waone wajibu wa kuishi jinsi ilivyowapasa. Mungu atatenda kazi maishani mwao, atazielekeza nia zao, ili watake kuishi iwapasavyo, pia atawatia nguvu ya kuishi hivyo. Hawatakuwa peke yao. Wamtegemee Mungu na msaada wake.

Wokovu uliozungumzwa ni wokovu wa shirika zima la Filipi si wokovu wa mtu mmoja mmoja. Sehemu yote imesema juu ya maisha yao ya pamoja (1:28; 2:4)

k.14-16 Walikuwa na heshima kubwa ya kuwa wana wa Mungu (Yn.1:12) na kwa sababu hiyo walikuwa na wajibu mkubwa (Efe. 5:1) Wamo katika ulimwengu wa giza, waliishi kati ya watu wakaidi waliomwasi Mungu, budi wasifanane nao (Yn.17:15-16) Kazi yao ni kuwa mianga, maisha yao yatoe nuru ili wengine wapate kumtambua Kristo. Hayo ndiyo mapenzi ya Mungu (Mt.5:14-16; 1 Pet.2:19).

Hivyo waache kunung'unika na kushindana, watende mambo yao kwa furaha na kwa kupendana na kwa kukubaliana. Wasiitumie hila wala udanganyifu. Wasiwe na malawama, wajitahidi kuwa na hali njema. Hasa walishike neno la uzima, yaani Injili. na kuwa waaminifu kwake. Wazitengeneza shida zao. Paulo hakutaka warudi nyuma na kupoa. Ikitokea hivyo atakuwa amejitaabisha bure. Kila mara aliogopa kufanya kazi bure (Gal.4:11; 1 The.2:19; 3:5; Gal.2:2; 1 Kor.15:58) Alitazama mbele kwa “siku ya Kristo” siku ya mwisho. Katika siku ile alitamani sana waumini wa Filipi wafike mbele za Kristo katika hali njema, hali ya kuhitimu, ndipo na yeye ataona fahari juu yao. Neno “kujitaabisha” ni kuonyesha jinsi Paulo alivyotoa maisha yake kwa ajili ya makanisa, wao walikuwa matunda ya shughuli zake za kuieneza Injili. Walifanana na mimea iliyohitaji utunzaji wa uangalifu sana ili wakue na kuimarika.

k.17-18 Paulo alikumbuka kwamba mbeleni aweza kuuawa, hakuwa na uhakika jinsi kesi yake itakavyokwenda. Alitumaini kuachiliwa. Akiuawa itakuwa kwa ajili ya Kristo, maisha yake yatahesabiwa kuwa dhabihu aliyotoa kama mfia dini (2 Tim.4:6). Ila kwake alihesabu dhabihu ni Wafilipi na kuamini kwao, hasa wakiishi maisha safi ya Kikristo (Rum.12:1, Lu.1:23; 2 Kor.9:12; Ebr.8:6; 9:21). Neno hilo lilimfanya Paulo afurahi sana, na alitaka na wao pia wafurahi sana. Wasimsikitikie yeye na kufungwa kwake, wala wasiyasikitikie mateso yao na dhiki zao. Wayakabili hayo yote katika hali ya furaha, wakipokea kwa hiari na kwa kutaka yote yaliyo mbele yao. Mkazo wa furaha ni neno la ajabu tunapokumbuka ya kuwa Paulo alifungwa mnyororo kwa muda mrefu, wala hakuwa na uhakika kwamba ataachiliwa.

2:19-30 Mipango ya kuwahusu Timotheo na Epafrodito

k.l9-24 Paulo aliwajulisha mipango yake. Kwanza alikuwa akikusudia kumtuma Timotheo kwao karibuni, ila hatamtuma mpaka ameyasikia matokeo ya kesi yake. Ikiwa atahukumiwa kufa basi Timotheo atawaletea habari kamili, kama ataruhisiwa Timotheo atawajulisha habari hiyo, na yeye mwenyewe atamfuata. “katika Bwana Yesu” mipango yake ilitegemea mapenzi ya Mungu, jinsi alivyoyatambua. Hasa shabaha ya kumtuma Timotheo ni kuwapa habari zake kamili, hilo litamfariji. Kama atakuwa hai, atakaporudi Timotheo atamletea habari zao kamili. Inaonekana amekaribia kumaliza miaka miwili ya kifungo chake.

Wafilipi walimfahamu Timotheo kwa sababu alikuwa pamoja na Paulo mara ya kwanza ya kuihubiri Injili pale, na Paulo alimtuma mara nyingine katikati ya Safari ya tatu.

k.20 Paulo alimwamini Timotheo kabisa, alifahamu ya kuwa alikuwa na mzigo uleule aliokuwa nao. Hatayapima mambo kwa juujuu, ila atachunguza na kuona hali zao halisi. Timotheo alipewa sifa ya hali ya juu “sina mtu mwingine.."(k.20) na “ametumika pamoja nami kwa ajili ya Injili kama mwana na baba yake” (k.22). Alikuwa amekolea hali ya Paulo, na Wafilipi waliufahamu uzuri wake na upendo wake kwao. Maneno “sina mwingine” ni maneno ya huzuni, inaonekana Paulo hakumwona mwingine wa kufaa kwenda Filipi. Kweli mtu wa kwenda atayakuta mambo yasiyo mazuri, lakini wapi mwenye vipawa na hali vya kuyakabili, inaonekana ni Timotheo tu.

2:25-30 Epafrodito alikuwa mtu wa Kanisa la Filipi. Alitumwa na wenzake kwenda mpaka Paulo akiuchukua msaada wao. Pia walitaka abaki na Paulo na kumhudumia. Paulo alimwita “ndugu yangu” “mtenda kazi pamoja nami” “askari mmoja nami” “mtume wenu” “mhudumu wa mahitaji yangu” Huenda maneno hayo yalihusu ushirikiano wao alipokuwa Filipi na wakati wa kuwa Rumi.

Epafrodito aliugua sana hata alikaribia kufa. Inaonekana alikuwa amejishughilisha sana kupita kiasi, kwa ajili ya kumtumikia Kristo kwa njia ya kumhudumia Paulo. Alipona na Paulo aliona ya kuwa katika jambo hilo Mungu amemhurumia Epafrodito, lakini si Epafrodito tu, ila na yeye pia. Kama angalikufa Paulo angalilemewa, angalibaki gerezani hali amefiwa na mtu mpendwa na mtu wa kumhudumia. Iwapo Paulo alikuwa mshupavu hata hivyo alisikia huzuni sawa na wanadamu wengine. Wafilipi walipata habari za Epafrodito kuugua nao walikuwa na wasiwasi juu yake. Yeye naye alisikia huzuni nyingi na shauku ya kurudi kwao ili watulizwe mawazo. Alipowaza hali hizo zote Paulo aliamua ni vema amrudishe kwao na alifanya bidii kumrudisha. Alitaka wampokee kwa furaha na kumheshimu sana kama mtumishi mwaminifu wa Kristo. Wasifikiri kwamba Paulo hakupendezwa naye eti! amemrudisha, la! wala wasimlaumu kwa kutaka kurudi. Kwa jumla, wasimwaze vibaya wala wasifikiri ni mtu aliyekosa kuutimiza utume wake.

Alitaka wafurahi sana kwa kupona kwake na kwa kurudi kwake. Wampokee "katika Bwana" yaani kama wangalimpokea na Bwana na kama ndivyo Bwana anavyowapokea watu wake wote.

M A S W A L I

1. *Kwa nini Paulo alitilia mkazo jambo la unyenyekevu?*

2. *Tunapoangalia hali ya makanisa yetu ya leo, Je! ipo haja ya kukaza jambo la unyenyekevu? Ukijibu "ndiyo" eleza ni mambo gani yanayohitaji kutibiwa na "unyenyekevu".*

3. *Ni nini hasa ambayo ni mvutiko mkubwa kwa Mkristo kuwa mnyenyekevu? Je! ni lazima Mkristo awe mnyenyekevu?*

3:1 Furaha

3:1 "hatimaye" Inaonekana Paulo alitaka kuufunga Waraka ndipo aliipata habari ya hatari ya Wayahudishaji (waumini wa Kiyahudi waliotaka waumini wa KiMataifa kutahiriwa). Kwa hiyo Paulo aliona kwamba amewajibika kutoa onyo kali kwa Wafilipi ili wajihadhari na hao watu na mafundisho yao. Alitumia neno "hatimaye" tena (4:8) alipokuwa tayari kuufunga Waraka.

Kabla ya kutoa onyo aliwaita Wafilipi kufurahi katika Bwana (4:4). Tumekwisha kuona kwamba neno "furaha" ni neno kuu mojawapo la Waraka. Ina maana gani "kufurahi katika Bwana"? Wafurahi kwa sababu wamekuwa mali ya Bwana, au kwa sababu ya mema yote waliyotendewa na Bwana. Haidhuru ni nini hasa, asili ya furaha yao iwe Bwana Yesu Mwenyewe.

Si wazi "mambo yaleyale" ni mambo gani? Yawezekana ni furaha kwa kuwa amesema nao mara kwa mara juu yake (1:18; 2:2, 18, 29). Aliona ni kwa faida yao akaze jambo la kufurahi, huenda alifikiri kwamba wako katika hatari ya kukata tamaa kwa ajili ya mateso (1:28-29).

Yawezekana mambo yaleyale ni kuhusu mkazo wa umoja kwa sababu ya hali ya wengine kugombana na kutokunia mamoja. Wazo lingine ni kuhusu onyo linaloanzia k.2. hasa ikiwa Paulo alikuwa amekwisha kuwaonya juu ya Wayahudishaji. Kama ni hivyo maneno "kutawafaa ninyi" ni maneno mazuri, ni faida yao kuonywa tena, kwa sababu wakitegwa na hao watu watakosa furaha na uhuru wao katika Kristo.

3:2-3 Onyo juu ya Wayahudishaji

Mara tatu Paulo alitumia neno "jihadharini". Wajihadhari na nini au nani". Alitaja "mbwa" ndipo "watendao mabaya" ndipo "wajikatao". Huenda si aina tatu za watu bali aina moja tu, akilieleza kundi moja kwa maneno hayo matatu. Ni dhahiri kwamba onyo lake ni zito akiwaonya kwa bidii.

Basi, Paulo alikuwa akiwawaza akina nani? Ama ni Wayahudi au baadhi ya Wakristo wa Kiyahudi. Kama ni Wakristo wa Kiyahudi ni wale waliotaka kuwalazamisha Wakristo wa KiMataifa watahiriwe (tumezoea kuwaita Wayahudishaji). Hao walimfuatafuata Paulo kila alipokwenda, wakifika kwenye shirika za Kikristo baada ya yeye kuondoka, wakiitikisa imani ya waumini wapya kwa kusema kwamba imani yao si kamili mpaka wametahiriwa, imani peke yake katika Kristo haikutosha. Paulo aliwachukia sana, alipiga vita kali nao (Gal.1:7; 5:2; 2 Kor.11:13-15) Neno hilo lilizuka mapema sana katika maisha ya Kanisa, mara baada ya kupatikana waongofu wa KiMataifa. Kanisa liliwahi kukutana na kuamua jambo hilo na kusema tohara si lazima kwa waumini walio WaMataifa (Mdo.15). Ajabu ni kwamba hao watu hawakuacha kulilisumbua Kanisa. Iwapo wenyewe walimwamini Kristo walitaka kuendelea na tohara na kuilazamisha kwa wale ambao hawakuijua.

Paulo aliwaita “mbwa”. Wayahudi waliwadharau sana WaMataifa na walizoea kuwaita “mbwa” (Mt.15:26; Uf.22:15) lakini Paulo aligeuza mambo kabisa kwa kulitumia neno lilelile kwa Wayahudi. Tena aliwaita “watendao mabaya” (2 Kor.11:13) hasa kwa sababu shughuli zao za kuipotosha imani ya waumini wa KiMataifa ilikuwa shughuli mbaya. Kwa kufanya hivyo walikuza “matendo ya nje” kuwa njia ya wokovu ili watu watumaini mambo ya mwili badala ya kumtumaini Kristo peke yake na kazi yake kwa ajili yao. Kisha Paulo alilitumia neno “wajikatao” bila shaka aliwaza tohara ila hakuwa tayari kusema tohara akimaanisha ni kukata tu, akinyima neno lisiwe na maana ya Tohara ya kweli. Paulo alisema vizuri juu ya tohara, iliyofanyika na Wayahudi kufuatana na agizo la Mungu kwa Abramu. Ila aliona kuwalazimisha waumini wa KiMataifa watahiriwe ni kuipotosha imani ya Kikristo, maana mtu huhesabiwa haki kwa imani bila nyongezo lolote.

k.3 Paulo alidai kwamba ni Wakristo walio nayo tohara ya kweli. Tohara ya kweli ni kumwabudu Mungu kwa Roho na kuona fahari juu ya Yesu Kristo bila kuutumaini mwili. (Ling. na Rum.2:25-29; Kol.2:11) Alifundisha kwamba Kanisa limezirithi ahadi za Mungu kwa watu wake Israeli (Rum.9:24-26; 1 Pet.2: 9-10). Hivyo, tohara imepata maana mpya, haiwi tena alama ya nje katika mwili, bali ni hali ya Kanisa kutambua ni Israeli Mpya, Watu wapya wa Mungu, ambao wamechukua nafasi ya Watu wake wa kale. Ni msaada kutazama vifungu vifuatavyo kuihusu tohara katika mafundisho ya Paulo. (Gal.3:26-29; 5:2-4,6; 6:15; Kol.3:11). Ni hatari sana kwa waumini wa KiMataifa kutahiriwa, badala ya kuwaletea faida itawaletea hasara. Wayahudi walidhani kwamba kwa tendo la nje katika mwili mtu hupata haki. Tohara ya kweli ni jambo la kiroho, ni itikio la imani ya kibinafsi, ambalo ishara yake ni ubatizo.

Twaona umuhimu wa kumwabudu Mungu katika Roho na kweli (Yn. 4:23-24; Zab.51:17). Alama nyingine ni kumfurahia Yesu Kristo, kumtukuza na kumsifu kwa ajili ya wokovu alioutupatia. Twamtegemea Yeye, hatujitegemei wala kujiona (1:26; 2:16; Rum.5:2; 1 Kor.1:3; 2 Kor.10:17).

“kutokuutumaini mwili” Kwa kawaida wanadamu hupenda kuleta uzuri wake na jitahada zake mbele za Mungu ili wavute kibali chake. Wayahudi walitumaini matendo ya nje ya ibada nk. Mtu akitumaini kitu chochote nje ya Kristo ni kuutumaini mwili na ni kuipotosha Injili. Hata Agano la Kale lilikuwa na mafundisho hayo likiwaonya watu wasiliweke tumaini lao kwa tohara nk. (Law.26:41; Kum.10:16; 30:6; Yer.4:4; Eze 44:7) Hivyo ni upuzi kuwalazimisha waumini wa KiMataifa watahiriwe. Iliyotakiwa na Mungu ni imani na utii kwa Kristo.

3:4-6 Historia ya Paulo katika dini ya Kiyahudi

Katika vifungu hivi Paulo aliandika habari za maisha yake kabla ya kumwamini Kristo, wakati alipoishi kwa kanuni za dini ya Kiyahudi. Wayahudi wakitaka kujadiliana naye juu ya dini yao, basi yeye yu tayari, tena hakika atawashinda, kwa sababu katika mambo yote aliwazidi. Zamani zile aliutumaini mwili, na aliweza kuthibitisha kwa ujuzi wa maisha. Katika habari hiyo hakuna aliyeweza kuamua vizuri kuliko Paulo “mimi zaidi” (k.4b).

Alitaja mambo saba

(i) “alitahiriwa siku ya nane” kama ilivyoandikwa katika Lawi 12:3 na kwa mfano wa Abramu Mwa.l7:l2. Neno hilo lashuhudia kwamba wazazi wake walikuwa Wayahudi kwelikweli walioishikilia Torati kama Wayahudi safi.

(ii) “ni mtu wa taifa la Israeli” Alizaliwa katika taifa teule la Mungu.

(iii) “wa kabila la Benyamini” sawa na Mfalme wa kwanza wa taifa la Israeli.

(iv) “Mwebrania wa Waebrania” alikuwa mwana wa wazazi walioitumia lugha ya asili (Mdo.6:1; 22:2; 2 Kor.11:22) alama ya yeye na wao kuwa Wayahudi halisi.

(v) “kwa habari ya kuishika Torati ni Farisayo” Utiifu wake na bidii yake kwa Torati ilionekana katika kujiunga na dhehebu la Mafarisayo, watu waliojulikana kwa bidii zao.

(vi) “kwa habari ya juhudi, mwenye kuliudhi Kanisa” katika kujitoa kwa ajili ya imani yake ya Kiyahudi alijitia kabisa katika shughuli za kuwakamata na kuwatesa Wakristo akinia kulifuta Kanisa (Mdo.7:58; 8:3).

(vii) “kwa haki ipatikanayo kwa sheria sikuwa na hatia” alijitahidi kabisa kuishika Torati na kuzitii amri zote za Mungu ili apate kuwa na haki na kibali cha Mungu. Aliishi bila lawama na bila hatia, hivyo alikuwa amehitimu kupita wenzake zote.

3:7- 17 Paulo aliukaza mwendo ili amjue Kristo

Kama ambavyo tumeona alikuwa na faida nyingi katika dini ya Kiyahudi, ila alipoamua kuwa Mkristo aliziweka kando faida hizo zote, na zaidi ya kuziweka kando, alizihesabu ni hasara tupu kusudi aipate ile faida ambayo ni faida hasa, ampate Kristo. Faida zile hazikuwa na msaada wowote katika kumpatia kibali cha Mungu na kumleta kwenye uhusiano mwema naye ambako ni kuhesabiwa haki kwa imani na kuvikwa haki ya Kristo.

Ni kama aliziweka pamoja na kutia katika ferushi na kuandika juu ya ferushi “hasara tupu”. Alifanya hivyo kwa ajili ya Kristo. Alizikataa kabisa na kuzichukia, pengine alikumbuka maneno ya Bwana Yesu (Mt.16:26; Mk.8:35). “Naliyahesabu” alipokutana na Yesu njiani kwenda Dameski alikata shauri la kumpokea Kristo na kuacha nyuma maisha yote yaliyotangulia hata maisha yake mazuri katika dini ya Kiyahudi.

k.8-14 Pamoja na kuzihesabu kuwa hasara faida alizokuwa nazo katika dini ya Kiyahudi aliamua kwamba hata faida nyingine za dunia si kitu. Aliikaza nia yake ya kumjua Kristo tu, yule aliyemwita na kumpa utume wa kuhubiri Injili. Mengine yote aliyahesabu kuwa kama mavi. Alipoyapima mengine yote na Kristo alimwona Kristo anao uzuri wa ajabu. Kwa kadiri alivyoendelea kuishi ndivyo alivyouona uzuri wa Kristo kuzidi. Kwake dini si kanuni, wala masharti, wala desturi na mila, bali ni Kristo, ni kumjua Kristo kibinafsi na kushirikiana naye. Kufanya hivyo kulimgharimia mahali pake kati ya Wayahudi wenzake, pengine hata katika familia yake. Kiburi chake chote na kujiona kwake kote kulikwisha. Kwake kuwa na Kristo ni utajiri mkuu, Kristo alitosha.

k.9 Nia yake ilikuwa kuonekana katika Kristo ili awe na haki ile itokayo kwa Mungu, haki kamili, haki ya kweli, haki ipitayo ile ya sheria. Haki nyingine haikutosha, wala haikukubalika na Mungu. Kwa kuvikwa haki ya Mungu hofu ya kukataliwa ilifukuzwa. Katika hukumu ya Mungu atakuwa salama salimini (Rum.8.1). Kwa imani mtu huipokea haki, ni kipawa cha Mungu (Gal.2:15-3:29; Efe.2:4-9; Rum.3:21-4:25).

k.10 “ili nimjue Yeye” Shabaha ya Paulo ilikuwa kushirikiana na Kristo zaidi na zaidi, kusudi amfahamu, amwelewe, awe na uhusiano naye kwa ukaribu sana, wawe kama marafiki wapendwa. “na uweza wa Kufufuka Kwake” Paulo alitaka kuishi maisha mapya, maisha ya kuzitegemea nguvu za Kristo, awezeshwe na nguvu zilezile zilizomfufua Kristo kutoka kwa wafu ili ashinde dhambi na majaribu yote, pamoja na kushinda shida na dhiki atakazozipata katika kumtumikia Kristo.

k.10b “na ushirika wa mateso yake.” alijua kwamba ameamua kumfuata Kristo aliyeteswa, Kristo aliyeishi maisha magumu si ya raha. Kristo aliyewaita watu kuuchukua msabala na kumfuata. Kristo aliyeahadi dhiki (Yn.16:33). Kwa hiyo alikuwa amejiweka tayari kuandamana na Kristo na kushiriki mateso pamoja naye (Rum.8:36; 2 Kor.4:10; Gal.6:17;Kol.1:24) Alipookolewa Anania alitumwa kwa Paulo na Bwana alimwambia kwamba Paulo atateswa mengi kwa ajili ya Kristo (Mdo.9:16). “nikifananishwa na Kufa kwake” Katika Rumi 6 Paulo alifundisha kwamba waumini hushiriki Kufa na Kufufuka Kwake Kristo. Alipokufa Kristo wao walikufa pamoja naye, maana yake waliifia dhambi, waliamua kuikataa dhambi (Rum.6:11) na Kristo alipofufuka wao nao walifufuka ili wamwishie Mungu (Gal.5:24; 6:14) Paulo alitumia lugha ya “kusulibiwa” yaani kuiua nafsi ili Kristo apate kuwa Bwana wa maisha.

k.11 Ndipo mambo yote yatatimia na kukamilika mbeleni wakati wa kiyama ya wafu. Wakati ule vita ya kiroho itakwisha. Paulo alitamani sana jambo hilo. Alikuwa na uhakika wa uzima wa milele ila hakujua yatakayompata karibuni hivi, kama atakufa au ataachiliwa.

k.12 Paulo hakudhani kwamba tayari amekamilika, la, hata kidogo. Ila alikuwa na shabaha hiyo akifanya juu chini ili azidi kukamilika, huku alijua kwamba kwa vyovyote mtu hawezi kukamilika kabisa akiwa angali hapa duniani. Alitambua ya kuwa Kristo alipomwita na kumwokoa alikuwa na lengo hilo, kwa hiyo ilimpasa akaze mwendo ili aitimize shabaha hiyo. Asitazame nyuma na kufikiri juu ya kushinda kwake na kushindwa kwake, mambo hayo yamepita. Iliyopo ni kutazama mbele na kusonga mbele. Atawaliwe na yale tu ambayo yatamsaidia kuutimiza mwenendo wake vizuri. Ni neno zuri kusahau kwa kusudi mambo ambayo yamepita, yaana tukiendelea kuyawaza tutacheleweshwa katika safari yetu. Tukiwaza mabaya yaliyo nyuma twaweza kulemewa na tukiwaza mema twaweza kushikwa na kiburi na kujiona.

Pengine walikuwepo watu waliosema kwamba inawezekana waumini wakamilike maadamu wako duniani. Paulo hakukubali. Ila alikubali kabisa kwamba ni juu ya waumini wote kuwa na nia ya kukamilika na kujitahidi kukamilika na kuwa na maendeleo katika kukamilika. Tena tukitazama mafundisho yake twaona kwamba alihesabu ni sehemu ya huduma yake kuwaita watu na kuwavuta waishi maisha yalengayo ukamilifu.

Ukamilifu aliousema Paulo ulikuwa nini hasa? Inaonekana ni kumjua Kristo kwa ukamilifu. Ni baraka ya uzima wa milele, uzima tunaoanza kuonja tungali hapa duniani. Na uzima huo Yohana ameueleza kuwa “kumjua Kristo” (Yn.17:3; 1 Yoh.5:12). Kutokana na sehemu hiyo twajifunza kwamba Paulo hakuridhika na hali yake kiasi cha kuacha kufanya bidii wala hakukata tamaa kwa sababu alikuwa bado hajakamilika. Neema ya Kristo ilimsukumu aendelee kuifuata shabaha yake ya kumjua Kristo na kushirikiana naye. Mbeleni liko tuzo kwa wale wote wenye kuukaza mwendo, tuzo ni kushirikiana na Kristo kwa ukamilifu katika ulimwengu ujao. Ila tuzo ni zawadi isifikiriwe kuwa thawabu kwa bidii zao. Asili ni katika mwito mkuu wa Mungu na katika neema ya Kristo.

k.15-17 Paulo aliwaita Wafilipi wawe na umoja “mkiwaza mengine” maneno hayo ni dalili ya wengine kuwepo ambao hawakupatana na mawazo hayo ya Paulo. Waliwaza tofauti na kwa sababu hiyo waliishi kwa lengo tofauti.

“sisi tulio wakamilifu” maneno hayo yahusu ukamilifu wa wale wenye kulenga ukamilifu, sio ukamilifu wa mwisho ambao Paulo amekwisha kuukataa uwezekano wake mpaka kinyama ya wafu (1 Kor.14:20; Ebr.5:14; 1 Kor.2:6; 3:1). Paulo alijua hakika kwamba mafundisho yake ni kweli hata aliwaambia wale waliowaza mengine kwamba Mungu atawafunulia neno hilo. Mpaka wamefunuliwa neno hilo waendelee katika hali ya kuwa tayari kulipokea.

k.17 Aliweka mbele yao kielelezo cha maisha yake ili waufuate mfano wake. Tusifikiri kwamba Paulo alijaa “umimi” la! Aliweza kusema hivi kwa sababu yeye mwenyewe alikuwa akikifuata kielelezo cha Bwana Yesu (1 Kor.11:1) Tena alipowaandikia Wathesalonike neno hilo aliweka pamoja naye wajoli wenzake kama akina Timotheo, Sila, nk. (1 The.1:6; 2 The.3:7-9). Ni vema tukumbuke kwamba siku zile Wakristo hawakuwa na Maandiko ya Agano Jipya ya kuwasaidia kujua jinsi ilivyowapasa kuishi. Watapata msaada katika kutazama maisha ya akina Paulo na wenzake.

3:18-21 Onyo juu ya “adui za Msalaba”

Paulo alifunga sehemu hiyo kwa kuwaonya juu ya Wakristo ambao aliwawaza kuwa adui za msalaba, watu walioishi kwa kuwaza na kuyafuata mambo ya dunia hii. Kwa jinsi alivyoandika ni dhahiri kwamba amewahi kuwaonya mara nyingi juu yao, na wakati huo wa kuandika alishuhudia kwamba alikuwa akiandika kwa machozi. Kwa hiyo aliwahesabu kuwa wa hatari sana, lazima wajihadhari nao sana sana. Je! walikuwa akina nani hasa? Baadhi ya wataalamu hufikiri ni wale Wayahudishaji waliotajwa mwanzoni mwa sura ya tatu. Au pengine ni Wakristo wa KiMataifa ambao waliwaza kwamba kwa sababu wameokolewa kwa neema si neno jinsi waiishivyo. Mwili si kitu, jambo kubwa ni roho zao. Lakini iwapo hawakuokolewa kwa matendo mema hata hivyo wameokolewa kusudi watende matendo mema (Efe.2:8-10). Au pengine ni Wakristo walioishi maisha ya kujipendekeza tu, hawakuwa tayari kujitoa, hawakuwa na mzigo wa mambo ya kiroho, mradhi tu wamemwamini Kristo hawakuona haja ya kukua kiroho (2:21).
k.20 Katika kifungu hicho Paulo ametoa sababu kubwa ya kuishi kiroho na kukaza mwendo. “wenyeji wetu uko mbinguni” Mkristo ni mtu ambaye kwa mawazo yake na kwa nia na shabaha za kuishi, amehama dunia hii, haishi kwa kanuni zake, iwapo bado angali katika mwili. Neno “wenyeji” linaonyesha kwamba Mkristo ameweka tumaini lake kwa Kristo mbinguni, ni kama anaishi pale, anajisikia kuwa kama mgeni hapa duniani. Bila shaka Wafilipi walikuwa na mfano mzuri katika wale Warumi waliokuja kuishi Filipi. Waliishi kama Warumi iwapo hawakuwa Rumi, utiifu wao ulikuwa kwa Kaisari aliyeishi mbali nao huko Rumi. Ni vivyo hivyo kwa Mkristo, anaishi kama yuko mbinguni iwapo angali duniani.

Ndipo Paulo aliwatazamisha mambo mawili makubwa ya baadaye. Kwanza Kristo Mwenyewe atatoka mbinguni na kuja kuwachukua Kwake ili waishi naye huko mbinguni milele na milele. Pili jambo hilo litatimia katika miili yao kubadilishwa, iwe miili kama mwili wa ufufuo na utukufu wa Bwana Yesu, mwili wa kufaa maisha ya mbinguni. Mwili wetu wa sasa si mbaya, ni mzuri, umeumbwa na Mungu (1 Kor.6:13ku) ila ni mnyonge, dhaifu, ni rahisi kwa dhambi kuunasa na kuvitumia viungo vyake (Rum.6:12ku. 7:14ku) (1 Kor.15:42ku).

Pengine hao watu walikuwa bado hawajatokea katika shirika la pale Filipi ila Paulo aliona vema awaonye mapema juu ya uwezekano wa watu hao kuzuka kati yao au kuja kutoka nje na kuwashambulia.

M A S W A L I

1. *Siku zile walikuwepo watu Wayahudishaji waliotegemea tohara na mambo ya Kiyahudi. Je! siku hizi Mkristo anategemea mambo gani ambayo hayana faida kwa upande wa kumwamini Kristo na kuokolewa kwa neema?*

2. *3:17 na 4:9 Kuhusu jambo la Paulo kuwaambia Wafilipi kuufuata mfano aliowapa. Je! alikuwa amejaa kiburi?*
   Je! katika mazingira ya wakati ule kwa nini aseme hivi?
   Waonaje? wahudumu wa siku hizi waseme hivyo kwa watu wao?
   Ikiwa si vizuri, Je! kimaisha wamewajibika kuwa vielelezo vema kwa watu wao? Eleza.

4:1-3 Umoja, na ombi kwa Euodia na Sintike

Maneno ya k.1 yaonyesha jinsi Paulo alivyowapenda sana Wakristo wa Filipi, akiwaita “ndugu zangu, wapendwa wangu, ninaowaonea shauku, furaha yangu, taji yangu”. Alitamani sana kuwaona (1:8). Kusema “taji yangu” huenda Paulo aliwawaza Wafilipi kuwa muhuri ya utume wake, na thibitisho la kazi yake kuwa si bure, wao ni kama thawabu (1 Kor.9:2; 15:58; Flp.2:16; Ebr.13:17) Aliwasihi wasimame imara katika Bwana kwa sababu ya hatari ya Wayahudishaji na wengine waliopenda mambo ya dunia kuliko mambo ya Kristo.

k.2-3 Euodia na Sintike walikuwa wanawake wawili katika shirika la Filipi. Inaonekana walikuwa baadhi ya waumini wa zamani. Ila walikuwa wamegombana. Paulo alishuhudia kwamba hapo nyuma walikuwa msaada kwake katika kuishindania Injili, ila hakusema walitoa msaada gani. Twakumbuka Lidia alitoa msaada mkubwa siku za kwanza kabisa alipowakaribisha Paulo na wenzake nyumbani mwake (Mdo.16:15,40). Wanawake hao walijulikana sana na bila shaka habari zao zilienea. Paulo alisikitika kwamba wamegombana na aliwaomba wawe na nia moja, wawaze faida ya Kanisa si faida yao ya binafsi na wakifuate kielelezo cha Bwana Yesu (2:3,5).

Paulo alimtaja Mkristo mwingine wa pale ambaye alifikiri ataweza kuwasaidia ila hakusema jina lake, alimwita “mjoli wa kweli”. Pia alimtaja Klementi na wengine akiwajumlisha pamoja kwa maneno “watenda kazi pamoja nami”. Iwapo sisi hatuwajui, Mungu huwajua, nao wameandikwa katika Kitabu cha Uzima (1 Kor.4:5; Kut.32:32. Dan.12:1; Zab.69:28; Lu.10:20; Ufu.3:5; 20:13). Mungu huwakumbuka pamoja na matendo yao. Iwapo Paulo alikuwa

amewahukumu hao wanawake kwa sababu ya ugomvi wao hata hivyo alitumaini wataitengeneza shida iliyo kati yao, na alitaka kuwatia moyo kwa kutaja habari zao za nyuma wakati alipokuwa pamoja nao.

4:4-7 Furaha, Upole, Maombi, Shukrani, Amani ya Mungu

Kama ambavyo tumekwisha kuona katika Waraka huo jambo la furaha limekuwa muhimu. “Furahini katika Bwana sikuzote”. Ni vema tukumbuke Paulo na mazingara yake na Wafilipi na mazingara yao. Paulo aliandika maneno hayo hali amefungwa minyororo akiungoja uamuzi wa kesi yake, wala hakuwa na uhakika wa matokeo yake. Mbele yake, ama ni kuuawa ama ni kuruhusiwa. Hata hivyo neno “furahini” ni midomoni mwake na nafsini mwake. Halafu kwa upande wa Wafilipi, walikuwa wakiyakabili mateso na dhiki kwa ajili ya kumwamini Kristo (1:28-30) pia waliishi kati ya dunia ya giza (2:15) hata hivyo neno la Paulo kwao ni “furahini katika Bwana sikuzote”. Ni wazi kwamba furaha yao haiwi katika mambo ya nje kama ni mema au mabaya bali ni “katika Bwana” kwa sababu Bwana amewapokea na kuwasamehe, Bwana amewapa kipawa cha uzima. Pia baraka ya daima ni kushirikiana kibinafsi na Bwana aliye hai, Bwana aliye juu, Bwana aliyeshinda. Kwa hiyo, furahini, tena furahini. Neno “sikuzote” laonyesha kwamba furaha ya namna hiyo haiguswi na mambo ya kila siku.

k.5 Tena hali nyingine waliyodaiwa ni upole. Wawe na subira na uvumilivu, wachukulieni na watu wa hali zote. Wakimfurahia Bwana mioyoni mwao watavutwa kuwahurumia wengine. “Bwana yu karibu” Maana yake nini? Yawezekana maana yake ni kuhusu ukaribu wa Bwana kwa waumini, kila muumini aweza kushirikiana naye kibinafsi wakati wote. Maana nyingine ni kwamba Bwana Yesu yu karibu kurudi, kwa sababu siku zile wakristo walitazamia Bwana atarudi bila kukawia. Wao kwa wao walitumia usemi “Maran atha” (Bwana wetu anakuja) (1 Kor.16:22; Ufu.22:20). Huenda maana zote mbili ni sawa.

k.6 Halafu Paulo alitoa mwongozo juu ya kuomba. Neno la kwanza ni “msijisumbue kwa neno lolote”. Iwapo mateso na dhiki zipo, iwapo wamezungukwa na dunia iliyojaa giza, dawa ni kuomba. Wajikabidhi kwa Bwana na kumwekea kila jambo, hivyo hawataona nafasi ya kusumbuka. Wamtumaini Bwana na wawe na uhakika wa wema na utunzaji wake (Mt.6:25- 34; Lk.12:22). Wafanye nini? waombe, wamletee Bwana kila neno; wamjulishe haja zao, na hayo yote katika hali ya kumshukuru. Kwa Paulo masumbufu na maombi ni mawili yasiyopatana. Kama mwandishi mmoja alivyoandika “Kwani kuomba ukiweza kujisumbua? kwani kujisumbua ukiweza kuomba?”. Inayotakiwa ni moja tu, na kwa Mkristo ni kuomba.

k.7 Tokeo jema la kuomba kwa imani ya kumkabidhi Mungu neno lolote ni amani ya Mungu. Ahadi ya amani yake ilitolewa kwa watu wake wa zamani (Isa.26..). Amani ya Mungu ni amani yenye asili katika Mungu (4:9b) ni amani

ambayo ni kipawa cha Mungu, yatoka Kwake. Twajua amani hiyo baada ya kupatanishwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo, baada ya kuwa na amani kwa Mungu (Rum.5:1) kwa sababu ni Kristo aliyefanya amani kwa damu ya Msalaba wake (Kol.1:20; Efe.2:14ku). "ipitayo akili zote" ni amani ya kipekee, isiyoweza kulinganishwa na kitu kingine, ni zaidi ya kuwaza kwetu hata ya kuota kwetu.

Amani hiyo hufanya kazi gani? hufanya kazi ya ulinzi mfano wa askari mlinzi alindaye kitu fulani au mahali fulani. Wakati wa kushambuliwa na hofu, mashaka, majaribu nk. amani ya Mungu huwa askari mlinzi ili tusilemewe. "itawahifadhi mioyo yenu na nia zenu katika Yesu Kristo" ulinzi huo upo maadamu tunamtii Kristo kama Bwana wa maisha yetu. Katika Kol.3:15 amani ya Kristo ni mwamuzi, mfano wa mwamuzi wa michezo apigaye filimbi yake, amani itatulia kwa kuamua vizuri na itaondoka kwa kuamua kinyume cha mapenzi ya Mungu. Ni msaada mkubwa wakati wa kutokujua la kufanya.

4:8-9 Kuwaza mambo mema

Ndipo Paulo aligusa jambo la Mkristo na mawazo yake. Ili Mkristo aendelee kujua amani ya Mungu na kusikia hali ya Kuwepo kwa Mungu katika maisha yake budi aangalie sana ni mambo gani anayoyazingatia na kutia maanani, mambo ambayo yatamwongoza katika utendaji wake. Neno la Mungu lakaza "utendaji" na kufundisha kwamba utendaji wa mtu umejengwa juu ya kuwaza kwake (Rum.12:2). Kujua mapenzi ya Mungu hakutoshi, inayotakiwa ni kuyajua na kuyatenda. Halafu Paulo aliorodhesha mambo mbalimbali ya kuyatafakari: "ya kweli, ya staha, ya haki, yaliyo safi, ya kupendeza; yenye sifa njema, ya wema wowote, ya sifa nzuri yoyote" – Wafilipi wayatafakarini sana mambo hayo ili yakolee maishani mwao.

k.9 Paulo mwenyewe alikuwa ameruhusu maisha yake kuguswa na kutawaliwa na mambo kama hayo, hata aliweza kusema "mambo mliyojifunza kwangu, na kuyapokea, na kuyasikia, na kuyaona kwangu, yatendeni hayo" Kumbe! kwake wamejifunza, wamepokea, wamesikia na kuona hayo (3:17).

Je! kwa kusema hivi si amejaa kiburi? La! sivyo. Kwanza, Paulo alikuwa na haki ya kusema hivyo kwa kuwa amemtumikia Kristo mia kwa mia, tena kwa hali na tabia zile za Kristo. Pili, kwa sababu wakati ule Wakristo hawakuwa na Maandiko ya kuwaongoza. Mwongozo wao ulikuwa kielelezo cha Paulo na Mitume wengine. Mara kwa mara Paulo alilitaja jambo la "mapokeo" au maagizo aliyokuwa amewapa (1 Kor.11:2, 23; Gal. 1:9; Kol.2:6; 1 The.4:1-2; 2 The.2:15). Baadaye mapokeo hayo yaliingizwa katika Maandiko ya Agano Jipya. Twaona katika k.9 ametumia neno "kuyapokea".

Watu waliojenga maisha yao juu ya mafundisho na kielelezo cha Paulo na wenzake walibarikiwa. Waliisikia amani ya Mungu mioyoni mwao, pamoja na kuwa na Mungu wa amani pamoja nao. Baraka hizo zilikuwa na uvutiko mkubwa kwa watu "kuyatafakarini hayo" (k.8) (2 Kor.13:11; 2 The.3:16).

4:10-20 Shukrani za Paulo kwa vipawa walivyomletea

Alipokaribia kuufunga Waraka Paulo aliona vema awashukuru kwa vipawa alivyopokea mikononi mwa Epafrodito (4:18) hasa kwa sababu Epafrodito alikuwa akirudi kwao (2:25). Inawezekana amekwisha kuwashukuru ila aliona vema awashukuru tena. "sasa mwisho mmehuisha fikira zenu kwa ajili yangu kama vile mlivyokuwa mkinifikiri hali yangu, lakini hamkupata nafasi" Si wazi kama walishindwa kumfikia na vipawa au walishindwa uwezo wa kumsaidia, ila Paulo hakutaka walisumbukie neno hilo, kwa kuwa yeye mwenyewe hakuona shida. Kutokana na mambo yaliyompata alikuwa amejifunza kutokujali hali za nje kuhusu kula na kuvaa nk. alikuwa radhi na hali yoyote, kwa kuwa macho yake yalimtazama Kristo na uaminifu wake.

k.13 "naweza mambo yote katika Yeye anitiaye nguvu"
Aliushuhudia ushindi juu ya mambo hayo, jinsi alivyotiwa nguvu na Kristo. Kwa hiyo, kwa upande mmoja alijaa shukrani kwa Wafilipi katika kumletea vipawa na hasa kwa ushirika wao ila hakutaka wafikiri kwamba alivitegemea vipawa vyao au alitaka wamletee tena.

k.14-16 Alithamini sana jinsi walivyoshirikiana naye katika dhiki zake. Hata zamani zile za kwanza walimletea msaada. Kushiriki kulikuwa katika kutoa na kupokea (1 Kor.9:11).

k.17-18 Hasa kitu alichotafuta si vipawa kutoka kwao bali wao kupata baraka ya kiroho, baraka kutoka kwa Mungu. Paulo alihesabu vipawa walivyomletea kuwa harufu ya manukato kama sadaka zilizotolewa na Waisraeli wakati wa Agano la

Kale. Imekuwaje avihesabu hivyo? Ni kwa sababu walivitoa kwa moyo na kwa upendo, hali zimpendezazo Mungu (Yo.12:3).

k.19 Wengine huwaza kwamba Wafilipi walikuwa katika hali ya dhiki na umaskini wakati wa Paulo kuwaandikia, wakikumbuka picha ya makanisa ya Makedonia iliyoonyeshwa katika 2 Kor.8:2ku. Habari inahusu changizo kwa Wakristo maskini wa Yerusalemu. "..zaidi ya uwezo wao...walitoa vitu vyao..." Je! walikuwa wametoa kiasi cha kuuzidisha umaskini wao? kweli hatujui, ila twaona Paulo aliwatazamisha kwa Mungu, Mungu wake, yule aliyekuwa amemwezesha katika hali zote. Aliwaambia kwamba Mungu atawawezesha na kuwapa mahitaji yao. Paulo hakusema ni mahitaji gani, kama ni ya kimwili au ya kiroho, ila aliamini kabisa kwamba Mungu ni Mwaminifu, na katika uaminifu

wake atawajaza kwa kadiri ya (si kutoka kwa) utajiri wake katika Kristo. Nani awezaye kuupima utajiri wake? (Rum.11:33).

“katika utukufu” maneno hayo yahusu nini hasa? Je! yahusu kujazwa mahitaji? au yahusu “utajiri”? Utukufu na utajiri una maana ulio karibu. “ndani ya Kristo Yesu” Wamekuwa matajiri kwa njia ya Kristo maana wameunganika na Yeye aliye Tajiri (2 Kor.8:9) Wamejua hayo maana wamefunuliwa ujuzi huo wa utajiri (Kol.1:27; 2:3)

k.20 Mambo hayo yalimfanya Paulo asikie kumsifu Mungu sana. “Mungu, Baba yetu, atukuzwe milele na milele” Paulo alisikia furaha ya ajabu sana alipotafakari wema na neema ya Mungu kwake na kwa Wafilipi.

4: 21-23 Salaam za kuagana

Paulo alitoa salaam zake na za wale waliokuwa pamoja naye. Miongoni mwao ametaja “wale walio wa nyumbani mwa Kaisari”. Tusiwaze hao kuwa wa jamaa ya Kaisari, bali ni watumishi na watumwa waliotumika katika Jumba lake. Kwa njia tusizozijua walikuwa wamekutana na Paulo au wamepata kusikia Injili na wamekata shauri la kumwamini Kristo. Katika salaam aliwaingiza wote na alituma salaam kwa wote, “mnisalimie kila mtakatifu” “watakatifu wote wawasalimu". Neno “takatifu” lahusu Wakristo wote si baadhi walio wazuri tu. Katika Waraka Paulo ametilia mkazo jambo la umoja na kwa kusudi alitumia neno “wote” kila wakati.

k.23 Kama kawaida yake aliufunga Waraka na “Neema ya Bwana Yesu Kristo” kwa sababu neema hasa ni baraka inayokumbatia baraka zote ndani yake na ni asili ya baraka zote.

M A S W A L I

1. *Una mawazo gani juu ya jambo la makanisa ya nchi zenye maendeleo kushirikiana na makanisa katika nchi zilizo na shida. Paulo alisema juu ya kutoa na kupokea kwa pande zote. Kwa hiyo makanisa katika nchi zenye maendeleo watoe nini na wapokee nini? Vilevile makanisa katika nchi za shida watoe nini na wapokee nini? Au kwa maneno mengine waweza kusaidiana kwa njia zipi?*

   (twajua kila nchi ina shida, ila hasa shida inayowazwa katika swali ni shida ya umaskini)

SWALI kuhusu WARAKA MZIMA
Umejifunza nini kutokana na Waraka huo:
(a) kwa upande wa watumishi wa Kristo?
(b) kwa upande wa Wakristo katika makanisa yao?
(c) Umepata maoni gani kwa Kanisa la leo?

WARAKA KWA WAKOLOSAI

YALIYOMO

UTANGULIZI
(a) Mji wa Kolosai na mwanzo wa Kanisa pale
(b) Mwandishi wa Waraka
(c) Mahali na Wakati wa Kuandikwa
(d) Shabaha ya Waraka

UFAFANUZI
1:1-2Salaam
3-8 Shukrani
9-14 Maombi ya Paulo kwa ajili yao
15-23 Nafsi na Kazi ya Yesu Kristo
24-2:3 Fungu la Paulo katika kazi ya Kristo

2: 4-23 Mafundisho ya uongo na Kweli ya Kikristo

3: 1 - 4:1 Taratibu mpya ya Maisha

4: 2-6 Mashauri mbalimbali
7-18 Salaam za kuagana

UTANGULIZI

(a) Mji wa Kolosai na mwanzo wa Kanisa pale

Kolosai, Laodikia na Hierapoli ilikuwa miji mitatu jirani katika Bonde la Lika (Lycus Valley) maili kama mia moja mashariki ya mji mkuu wa Efeso katika Jimbo la Asia Ndogo katika Dola ya Kirumi. Bila shaka wenyeji wa miji hiyo walishirikiana, pia Wakristo wa miji hiyo walishirikiana (2:1; 4:13,16). Katika miji hiyo Laodikia ulikuwa mkubwa na wa maana zaidi. Inaonekana Paulo alikuwa bado hajafika Kolosai na sehemu zile (2:1).

Walipataje kuisikia Injili? Ni Epafra mmoja wao aliyewaletea Habari Njema (1:7) na inaonekana yeye alikutana na Paulo na kupewa mamlaka ya kuwa mhudumu pale Kolosai. Paulo alimwita “mjoli wetu mpenzi” na “mhudumu mwaminifu wa Kristo” (1:7). Twajua Wakristo walikutana katika nyumba ya Filemoni (Flm.19). Je! Epafra alikutana na Paulo wapi? Hatujui, ila twajua Paulo alikaa kwa muda mrefu sana, kama miaka 3 huko Efeso katika Safari Kubwa ya 3, na ya kuwa kutokana na huduma yake wengi wa Asia walipata kusikia Habari Njema (Mdo.19:10). Inawezekana alipata kuokolewa kwa njia

ya Paulo ndipo Paulo akamwelimisha zaidi na kumrudisha nyumbani kwake ili afanye huduma pale.

Twajua Epafra alimwambia Paulo juu ya Wakristo na imani na upendo wao (1:8). Pengine alitafuta ushauri kwa Paulo kuhusu wengine waliokuwa wakileta mafundisho kinyume cha Injili.

(b) Mwandishi wa Waraka
Ni Mtume Paulo (1:1,23; 4:18). Timotheo alikuwa pamoja naye. Aliwataja wengine waliokuwa pamoja naye wakati wa kuandika Aristarko, Luka, Dema, Marko na Epafra.

Waraka unafanana sana na Waraka kwa Filemoni, katika kumtaja Timotheo kuwa pamoja naye, na hao wengine, na Arkipo (Flm.2) Tikiko alichukua barua hiyo mpaka Kolosai. Onesimo alikwenda pamoja naye, akirudi kwa bwana wake Filemoni (4:7-9).

(**c) Mahali na Wakati wa Kuandika Waraka huu** Paulo
alikuwa kifungoni huko Rumi (4:3,18; Mdo.28:30).
Alifungwa huko Rumi kwa miaka miwili na alitazamia kwamba ataruhusiwa. Kwa hiyo tarehe itakuwa kama BK.62/63 hivi. Twajua aliweza kupokea watu (Mdo. 28:30).

(d) Shabaha ya Waraka
Waraka huo hauwi mkali kama ule kwa Wagalatia. Umeandikwa kwa sauti ya urafiki na ya shukrani. Kweli hatari ipo, lakini haijaiva, kwa hiyo Paulo alitaka kuwahi shida na kuwaonya waamini kabla hawajachukuliwa na mafundisho mageni.
Shabaha ilikuwa kumsaidia Epafra na Wakristo wa pale ili wakabili wale waliokuwa wakifundisha kinyume cha kweli ya Injili. Inaonekana walikuwepo kundi la watu, huenda si wengi, ambao waliupunguza Ukuu na Utukufu wa Yesu Kristo. Ni vigumu kujua mafundisho yao hasa ila Paulo aligusa mambo ya Kiyahudi, ya Sabato na kutokula chakula fulani (2:16). Pia, huenda walikaza kutahiriwa kimwili, maana Paulo alisema juu ya tohara (2:11ku.3:11).

Pamoja na hayo inaonekana walichanganya hayo na mawazo ya Kiyunani. Katika filosofia za Kiyunani watu walifikiri kwamba kuna mashindano kati ya mwili na roho, wakidhani kwamba asili ya uovu ni katika mambo ya mwili na mwili ni kama kizuizi au gereza la roho, mema yakiwa na asili katika "roho" na roho imefungwa katika mwili. Hivyo wengi waliona dawa ni kuutawala mwili kwa nguvu kwa njia ya kujinyima n.k.

Kinyime cha mawazo hayo wengine walithubutu kusema kwamba si neno mwili ufanye nini, roho haiguswi, basi watu wawe huru kufanya lolote lile wanalotaka. Pia walifikiri malaika ni kati yao na Mungu na kwa mawazo yao Mungu

hakuweza kuhusika moja kwa moja na mwili na dunia hii mbovu. Kwa hiyo walifundisha watu kujinyenyekeza sana kana kwamba hawakustahili kumkaribia Mungu, badala yake wajiweke chini ya malaika na enzi zake na kuziabudu. Tusifikiri kwamba hawakumkubali Kristo, ila kosa lao kubwa lilikuwa hawakumpa mahali pake pa juu na pa kwanza kabisa.

Hasa walidai kwamba kwa mafundisho yao waamini wataikamilisha na kuitimiliza imani yao, wakielekeza watu kufikiri kwamba mafundisho ya Epafra na wenzake yalikosa kina, na ya kwamba elimu na hekima waliyofundisha ilipita ile ya Injili. Ni kama nyongezo. Mpaka leo waletao mafundisho mageni hudai vivyo hivyo.

Pengine walitumia njia fulani, labda ibada, kwa kuwaingiza wale waliokubali siri hiyo ya mafundisho yao, lakini Paulo alikaza sana “siri” ya Injili ni siri iliyo wazi na ni kwa watu wote (1:6; 25-28; 2:2-3).

Paulo alilenga kumkuza Kristo na kumwadhimisha mno hasa kazi zake za Kufa Msalabani, ili Wakristo watiwe moyo.

UFAFANUZI

1:1-2 Salaam
Paulo alianza kwa kutaja mamlaka yake ya kuwa Mtume mwenye haki ya kusema na Kanisa hili la Kolosai. Yeye alikuwa Mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu, si cheo alichojitafutia. Hakukaza kwa nguvu Utume wake kama alivyofanya kwa makanisa mengine kwa sababu iwapo shida ilikuwepo haikuwa kubwa. Ila ilikuwa vema wasomaji wa Waraka wafahamu kwamba yale aliyoyasema nao yalikuwa na mamlaka ya Kristo na iliwapasa kuyapokea maneno yake na mafundisho yake kama yametoka kwa Mungu.

Timotheo alikuwa pamoja naye na Paulo aliunganisha salaam za Timotheo pamoja na zake. Hakumwita Timotheo “mtume” ila ni “ndugu yetu". Paulo alikuwa Mtume, si kwa ajili ya uzuri wake, wala kwa wema wake, bali kwa “mapenzi ya Mungu” ni neema na rehema za Mungu tu zilizomfanya kuwa Mtume.

k.2 Barua ni kwa “ndugu watakatifu waaminifu katika Kristo” walioko Kolosai. Hao waamini waliishi pale Kolosai, mji mdogo na bila shaka walibanwa na majaribu mbalimbali yaliyowasonga kuishi kama wenyeji waliowazunguka. Ila hawakukubali kutiishwa nao. Walijitenga na maisha ya kawaida ya wenzao ili wamwishie Mungu wa kweli na kufuata kielelezo cha Bwana Yesu. “waaminifu katika Kristo” kwa maneno hayo Paulo alitaka kuwatia moyo wa kuendelea kumfuata Kristo. Baraka kubwa waliyo nayo pamoja na ndugu wote ni kuwa “katika Kristo". Utajiri wote wa kiroho ulikuwa wao wakiwa “katika Kristo".

Ndipo Paulo alituma zile salaam alizozizoea kutumia katika nyaraka zake. “Neema na amani” – neema ishara ya kukubalika na Mungu bila masharti, na amani, tunda la kibali hicho.

1: 3-8 Shukrani

Paulo na Timotheo walimshukuru Mungu sana kwa ajili ya Wakristo wa Kolosai kwa sababu walisikia habari nzuri juu yao, habari ya imani yao katika Kristo, na habari ya upendo wao kwa waamini wenzao. Kwa habari hizo njema walijua hakika kwamba ni Mungu aliyefanya kazi kati yao na ndani yao. Ilikuwa wajibu wao kumshukuru Mungu pamoja na kuwakumbuka daima katika maombi. Ingalikuwa rahisi kwa Paulo kuwapongeza kwa hayo, lakini alifahamu ni Mungu tu aliyestahili kutukuzwa na kupewa shukrani. (Is.42:8; 48:11).

Katika shukrani zake alimweka Yesu sawa kabisa na Baba kuwa washiriki wa Uungu mmoja.

k.5 Ni kitu gani kilichowasukuma kuishi kwa imani na upendo? Ni tumaini walilokuwa nalo katika Kristo, walijua kwamba maisha ya namna hiyo si bure, yalifaa kwa wakati wa sasa na zaidi kwa baadaye katika ulimwengu ujao. Ni Injili iliyoweka wazi tumaini hilo, ambalo msingi wake ni katika ahadi za Mungu. Mungu ameahidi kwamba Kristo atarudi tena, na ya kuwa watafufuka kutoka kwa wafu na kuishi katika uzima wa milele. Ahadi hizo walipewa na Mungu, hazitegemei neno lolote la upande wao, si kitu jinsi wao wenyewe walivyojisikia, haidhuru hali zao na mazingira yao yakoje, iliyopo ni kwamba wameahidiwa hayo na Mungu Mwenyewe ambaye hatawaliwi na jambo lolote. Zimewekwa akiba huko mbinguni, zi salama kabisa, haziguswi na kitu chochote. Kwa sababu ya tumaini hilo hawahitaji neno lingine kutoka kwa wale waalimu wa elimu nyingine.

k.6 Mambo hayo Wakolosai walisikia walipohubiriwa Injili ya kweli. Habari yenyewe waliipata kwa wahubiri ila ujumbe ulitoka kwa Mungu. Wengine walikata shauri kuupokea ujumbe huo nao wakazaa matunda katika maisha yao. Walijulishwa “neema ya Mungu” yaani Mungu kuwapokea bila masharti, bila kutazama hali zao, mradi tu, walikubali ni wenye dhambi wasioweza kufanya lolote kwa wokovu wao, wakawa tayari kumpokea Bwana Yesu na Kifo chake msalabani. Tena habari hiyo hawakuishika kichwani tu, bali waliipokea ndani ya maisha yao na kuiruhusu ifanye kazi kwa nguvu wakizaa matunda na kukua katika ujuzi wa kiroho. Habari hii njema ni ya kweli kabisa na inasambaa mpaka maeneo mengine na nchi zingine.

Paulo alitaka Wakristo wayapime madai ya waalimu wa elimu nyingine Je! ni kweli ya Mungu? Je! ni kwa ulimwengu mzima? Je! inazaa matunda mema katika maisha ya watu? Kama jibu ni siyo, basi, elimu hiyo si sawa na Injili waliyopokea. Lazima Injili izae matunda mema ili iwe Injili ya kweli.

k.7 Tena wampime mjumbe aliyewaletea Habari Njema. Ni Epafra mwenyeji wa pale pale, ambaye walimfahamu sana (4:12,13). Ni afadhali kusoma “kwa ajili yetu” badala ya “kwa ajili yenu". Ni dhahiri kwamba Epafra hakuhubiri Injili pale kwa kuamua mwenyewe kufanya hivi. Alifanya huduma yake kwa kusimamiwa na Paulo, inaonekana ni Paulo aliyemtuma pale, na zaidi alitumwa na Kristo na kuwa na mamlaka yake. Paulo alimwita “mjoli wetu mpenzi, aliye mhudumu mwaminifu wa Kristo".

k.8 Pamoja na kuwajulisha Injili Epafra alimletea Paulo ripoti juu ya maendeleo ya wale walioamini. Ripoti ilikuwa nzuri, walikuwa wakizidi kukua katika upendo (k.4) upendo usio na asili katika ubinadamu wao bali ni ule wa neema, upendo unaotokezwa na Roho Mtakatifu (Gal.5:22).

1:9-14 Maombi ya Paulo kwa ajili yao
Paulo alishuhudia kwamba tangu alipopata habari zao alimshukuru Mungu kwa ajili yao (k.3-4) na kuwaombea daima. Ilikuwa kawaida yake kufanya hivi, akitaja jambo hilo katika nyaraka zake.

Alifurahi sana kusikia habari za maendeleo yao mazuri ya kiroho, hata hivyo, alitamani wazidi kukua kiroho. Kwa hiyo, pamoja na kumshukuru Mungu alitaja mambo mengine ambayo alitaka wawe nayo, na mambo hayo yaliongoza maombi yake.

Jambo la kwanza lilikuwa “mjazwe maarifa ya mapenzi yake” yaani alitaka wafahamu zaidi na zaidi mapenzi ya Mungu, maarifa hayo si ujuzi wa kawaida, wala hekima ya dunia hii, bali ni hekima na ujuzi utokao kwa Mungu. Mapenzi ya Mungu ndiyo kiini cha maisha ya Mkristo. Kujua mapenzi ya Mungu ni kitu cha kwanza kinachotangulia na kutuongoza katika kuishi maisha ya kumpendeza Mungu. Lazima tufahamu ni nini anachotaka Mungu na kinachompendeza ndipo tufanye hayo. Katika Sala ya Bwana, Yesu alitufundisha kuomba “mapenzi yako yatendeke".

k.10 Maarifa hayo si ya kichwa tu bali ni maarifa ya kiroho ambayo kwayo watautimiza wajibu wao kwa Bwana, kiutendaji watafanya mapenzi ya Mungu katika maisha ya kila siku, watampendeza kabisa na daima watazaa matunda na kuzidi kujua mapenzi yake. Kadiri watakavyoendelea kufanya mapenzi ya Mungu ndivyo watakavyozidi kuupanua ufahamu wao wa mapenzi yake. Kwa hiyo ujuzi wa mapenzi ya Mungu ni msingi hasa wa kukua kiroho. Mkristo awe mtendaji wa Neno (Yak.1:22).

k.11 Mpaka hapa tumeona kwamba neno la kwanza katika maombi ya Paulo lilikuwa wafahamu mapenzi ya Mungu, ndipo neno la pili lilikuwa wayatekeleze ufahamu huo katika maisha ya kila siku. Ndipo neno la tatu lilihusu uwezo kwa hayo yote. Watawezaje kutimiza mapenzi ya Mungu katika kufanya matendo mema na kukua kiroho? Kwa kweli sisi wanadamu hatuwezi kuishi maisha ya

kumpendeza Mungu, lakini habari njema ni kwamba Mungu hutupa uwezo wote tunaohitaji, wala si kwa jambo moja tu, bali kwa kila jambo la kila wakati. Haidhuru twaitwa kufanya mambo magumu na kutumika kwa kujitoa sana hata hivyo uwezo upo wa kufanya hivyo.

Uwezo huo ni wa namna gani? watoka wapi? Jibu ni kwamba ni uwezo wa Mungu Mwenyewe, uwezo unaotoka Kwake, “kwa kadiri ya nguvu ya Utukufu wake". Ni vigumu kuona nguvu hiyo hasa bali kwa njia ya matendo yake makuu twaona matokeo yake, na wote watakaotaka kufanya mapenzi yake wataishiriki nguvu hiyohiyo. Na nguvu yake ni sehemu ya Utukufu wake. Kwa hiyo ni vema tuwaze nguvu yake si mambo yenyewe.

Ila tusifikiri kwamba uwezo wa Mungu ni kutuwezesha kufanya maajabu, la! uwezo huo ni kutusaidia kuwa na subira na uvumilivu na furaha. Tutasaidiwa kukazana katika maisha yetu ya Kikristo, potelea mbali twafanyiwa nini na kukutana na magumu gani, uwezo wa Mungu utatusaidia kuvumilia yote, huku tukifurahi kuwa Wake na kuishi kwa kufuata kielelezo cha Bwana Yesu (Ebr.12:1-2)

k.12 Halafu Paulo alitaja shukrani kuwa tunda moja la kukua kwa imani yao. Haikutosha yeye mwenyewe amshukuru Mungu kwa ajili yao, hata wao wenyewe walipaswa “kumshukuru Baba". Kwa nini? Ni kwa sababu Baba “amewastahilisha kuwa na sehemu ya urithi wa watakatifu katika nuru” maana yake wameletwa katika ushirikiano mzuri sana, wakishirikiana na Mungu Mwenyewe kwa njia ya Yesu Kristo, pamoja na kushirikiana na waamini wote, nao wanayo sehemu yao katika baraka za Mungu. Wamekuwa kama Israeli ya zamani wakati walipoingia nchi ya ahadi, nchi ya Kanaani, kila kabila lilipewa sehemu ya nchi kuwa urithi wake. “Katika nuru” watu wa Mungu ni watu wa nuru, wanamfahamu Mungu tofauti na watu wa dunia walio “katika giza” bila ufahamu wa Mungu wa kweli. Urithi huo umepatikana si kwa bidii zao, wala kwa uzuri wao, bali ni kwa neema, kwa sababu ni Mungu aliyewastahilisha kutokana na mapenzi yake na kazi ya ukombozi wa Bwana Yesu. Urithi umetoka kwa Mungu na Yeye ameamua ni akina nani watakaorithi huo urithi.

k.13 Mungu amefanyaje? Kabla ya wao kuweza kurithi kitu chochote, na kabla ya wao kushirikiana na Mungu, Mungu alikuwa amefanya jambo kubwa la maana sana. Aliwaokoa katika nguvu za giza. Hapo nyuma walitawaliwa na dhambi na maovu, na Shetani na enzi za giza. Ndipo akaja Jemadari Mkuu, akafanya vita na vitu hivi vyote na kuvishinda, nao waliwekwa huru mbali navyo. Zaidi ya kuwekwa huru Mungu aliwahamisha na kuwaingiza katika utawala wa mwingine, katika Ufalme wa Mwana wa pendo lake. Katika Ufalme huo pendo la Mungu linamulika daima, nao waishi “katika nuru” na chini ya utawala wa Pendo la Mungu, na yote aliyewafanyia Mungu ni kwa njia ya Mwana wake aliye mboni wa jicho lake.

k.14 Kwa kuunganika na Kristo wameushiriki ushindi wake na ukombozi aliofanya (Mk.10:45; 1 Tim.2:6; 1 Pet.1:18-19). Ukombozi wa gharama sana, kwa sababu Kristo alikufa kwa ajili yao na kwa sababu hiyo walipata msamaha wa dhambi zao. Kwa kusemehewa waliachiliwa deni, Kristo alilipa deni lao la dhambi. Kwa ukombozi wake walifunguliwa deni, na pingu za dhambi zao zilikatwa, hawawi chini ya uwezo wa dhambi, na kwa kusamehewa hata hatia ya dhambi zao imeondolewa. Hizo baraka kubwa zinawapa nia na moyo wa kumshukuru Mungu.

1:15-23 Nafsi na Kazi ya Yesu Kristo

Katika k.13 Yesu alitajwa kuwa “Mwana wa pendo lake Baba". Ndipo Paulo aliendelea kuandika juu ya Yesu Kristo, na kueleza kinaganaga Nafsi yake na Kazi yake, akimwadhimisha mno. Alifanya hivi kwa sababu walikuwapo wengine waliofundisha mafundisho yaliyomnyima Yesu sifa zake na kuupunguza Ukuu wake na Cheo chake.

k.l5-20 Ukuu Wake: Maneno hayo ni kama wimbo juu ya Kristo. Wimbo huu husimamisha ukuu wake na utangulizi wake katika mambo yote, katika ulimwengu mzima (k.15-17) na katika Kanisa (k.18-20).

k.15a Kwanza kabisa Paulo alisema kwamba Yesu ni “mfano wa Mungu Asiyeonekana". Ni Mwana, peke yake, aliyeweza kumfunua Mungu kwa ukamilifu. Tangu zamani wanadamu wamechonga sanamu za Mungu na katika kufanya hivyo wameuharibu Utukufu wake, maana Mungu Hai asiyeharibika hawezi kuonekana Alivyo hasa hali amebanwa katika sanamu zisizo na uhai, zilizotengenezwa na mikono ya wanadamu (Rum.1:23; Mdo.17:16,24,25,29). Lakini katika Yesu Kristo Utukufu wa Mungu umedhihirika, Yesu ndiye ufunuo halisi wa Mungu Asiyeonekana. Mungu hukaa katika Nuru isiyokaribiwa, hawezi kuonekana kwa macho ya wanadamu lakini katika Mwana twamwona Alivyo hasa. Yeye hushiriki katika Mungu na tabia yake (2 Kor.4:4; Yn.10:30; 14:9).

Wanadamu waliumbwa katika sura na mfano wa Mungu (Mwa.1:26) na kwa sababu hiyo iliwezekana kwa Nafsi ya Pili ya Mungu kufanyika mwanadamu Yesu Kristo, na hivyo Asiyeonekana aliweza kuonekana (Yn.1:18; Ebr.1:3). Hakuna malaika aliye na haki ya kudai hivyo.

k.15b “Mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote” Maneno hayo hayana maana ya Yesu kuwa upeo wa Uumbaji na kusema aliumbwa la! Si mzaliwa wa kwanza katika mfuatano wa uumbaji, bali ni wa kwanza kwa maana ya kuwa “wa juu kabisa” na “bora zaidi". Yesu hakuumbwa, daima huwa “Mwana atokaye kwa Baba” ni Mungu Mwana, kabla ya uumbaji wa aina yoyote kufanyika. Yesu ni Mungu Mwana aliyekuwa ndani ya Baba na kama Baba hakuwa na mwanzo vilevile Mwana hakuwa na mwanzo. Vifungu vinavyofuata vinaweka wazi ukweli huo.

k.16 Ni kwa njia ya Yesu Kristo na kwa ajili yake uumbaji wote ulifanyika (Yn.1:1-3). Vyote vinavyoonekana na vyote visivyoonekana, hata malaika, shetani na malaika zake, enzi na mamlaka mbalimbali, vyote ni chini ya utawala wake. Yeye Yesu ndiye lengo la kweli la viumbe vyote, viliumbwa kwa kumtukuza Yeye na kuyatekeleza makusudi yake ya milele. Kwa hiyo tangu mwanzo hadi mwisho uumbaji umefungamana naye. Hawezi kulinganishwa na kuwekwa sawa na malaika na enzi zingine, maana Yeye ni wa juu kabisa.

k.17 Kifungu hicho chaweka wazi ukweli wa Yesu kuwepo kabla ya uumbaji wote. Yeye ni wa milele, uumbaji si wa milele, uumbaji ulikuwa na chanzo chake. Katika cheo chake cha kuwa Mungu Mwana atokaye kwa Baba hakuna wakati ambao hakutoka kwa Baba, Yeye huwa na cheo cha kipekee kabisa cha kuwa juu ya na kabla ya vyote vilivyofuata. Pamoja na kuwa njia na sababu na lengo la Uumbaji wote Yeye hushika yote na katika Yeye yote hushikamanishwa. Kwa sababu ya dhambi kuingia mafarakano yalitokea kati ya wanadamu, na kati ya wanadamu na uumbaji, na katika uumbaji wenyewe, na ni Yesu tu afanyaye yote kutokuachana na kutengana kabisa. Kwa ukombozi alioufanya upatanisho umefanyika, na hatua kwa hatua amani hurudishwa. Tutatazama neno hilo tena katika k.20. Iliyopo ni Yesu ni Mwumbaji, tena ni Mhifadhi wa viumbe vyote.

k.18 Baada ya kuonyesha Yesu kuwa “Bwana wa Uumbaji” Paulo aliendelea kuonyesha Yesu kuwa “Bwana wa Kanisa” na “Kichwa chake". Neno “kichwa” linaonyesha umuhimu wa Kristo kwa Kanisa. Kanisa huushiriki uzima wake, kama viungo vya mwili vyaushiriki uzima wetu na kichwa. Mwili bila kichwa hauna kazi! Kanisa bila Yesu halina kazi!! Yesu kama Kichwa cha Kanisa anaongoza na kutawala mambo yake na ni wajibu wa viungo vyake yaani waamini kumtii. Kwake Kanisa lapata umoja wake na kutekeleza makusudi yake.

Kwa hiyo inayotakiwa, si kwa Kanisa kupanga mambo yake vizuri, ila ni kwa watu wake kumtii Bwana wao.

"naye ni mwanzo” “mzaliwa wa kwanza katika wafu” Yaani Yesu ni mwanzo wa uumbaji mpya wa kiroho, kwa sababu Yeye ndiye wa kwanza kuishinda mauti na kutoka kwa wafu hali hafi tena (si kama Lazaro aliyetoka kwa wafu ndipo baadaye akafa tena) Kwa kuishinda mauti ameyasimamisha madai yake ya kuwa asili ya uzima, naye ni mtangulizi wa wale wote ambao watafufuka baadaye. Alifufuliwa katika hali ya kutokuharibika, nasi tutafufuliwa vivyo hivyo. Yeye ni Bwana wa Uumbaji, Bwana wa Kanisa, Bwana wa maisha yetu, Yeye ndiye Mkuu na Mtangulizi katika yote.

k.19 Mungu alipendezwa na utimilifu wote kukaa ndani ya Kristo, yaani ndani yake ulikaa utimilifu wote wa Mungu, alikuwa Mungu Mwanadamu. Ubindamu wake haukupunguza Uungu wake wala kuwa Mungu Mwana hakumfanya

apungukiwe katika neno lolote. Mungu alifurahi kumwona Mwana wake kufanyika mwili kwa ajili ya ukombozi wetu.

k.20 Ndipo mawazo ya Paulo yalitazama neno la upatanisho. Kama tulivyoona hapo nyuma, dhambi ilipoingia, mafarakano yalitokea, na Mwana alikubali kuwa mpatanishi na kutenda tendo kuu la upatanisho kwa njia ya Kufa kwake kwa ukatili sana pale Msalabani, ili afanye amani. Aliichukua ile laana ambayo ilikuwa yetu akaibeba pale Msalabani akafa kwa ajili ya dhambi zetu (Gal.3:13ku) ili sisi wenye dhambi turudishwe katika uhusiano mwema na Mungu.

Upatanisho huo ulihusu "vitu vyote" si wanadamu tu, yaani uumbaji wote (Rum.8:20ku). Tokeo lake litakuwa mbingu mpya na dunia mpya ambayo haki yakaa ndani yake (2 Pet.3:13) ndipo waasi wote ama ni wanadamu, ama ni malaika, ama ni mashetani, au nini vitafungiwe nje. Maneno "kufanya amani kwa damu ya msalaba wake" yaweka wazi mahali na wakati wa huo upatanisho kufanyika, ni jambo lililotokea kweli kihistoria.

k.21 Paulo aliendelea kwa kuyaonyesha matokeo ya mambo hayo makuu katika maisha ya waamini. Hapo nyuma hawakuwa na uhusiano mwema wala ushirikiano na Mungu, walikuwa adui zake, hawakumwaza vizuri, pia walifanya mabaya, wakiishi kinyume chake katika nia na matendo yao. Ndipo badiliko kubwa lilitokea, walipatanishwa na Mungu kwa njia ya Msalaba wa Kristo, na sasa wamekuwa rafiki zake, watu wa nyumbani mwake, watu walio na uhusiano mwema naye, uadui umeondolewa, uasi umekwisha, wamesamehewa dhambi, hamna tatizo kati yao na Mungu wao.

k.22-23 Lengo la baadaye ni kwamba waletwe mbele za Mungu, watakatifu, wasio na mawaa wala lawama. Lengo hilo ni jema sana ambalo kwa hakika litatimizwa mbeleni. Ila kwa sasa yawapasa kukazana katika imani yao, wasikubali kushawishiwa na kuacha tumaini lao la kufika mbele za Mungu, wajue kwamba mwishowe watakuwa safi kabisa kabisa, watu wasioshtakiwa neno lolote. Na jambo hilo lahusu wengi zaidi yao, maana Injili itaendelea kuhubiriwa ulimwenguni kama ambavyo imekwisha kuhubiriwa na Paulo, Epafra na wengine.

1:24 - 2:3 Fungu la Paulo katika kazi ya Kristo

k.24-25: Mateso yake: Hapo Paulo alisema juu ya dhiki na mateso aliyoyapata katika kuitimiza huduma yake ya kuhubiri Injili. Wakati wa kuandika alifungwa gerezani (4:18). "kwa ajili yenu" iwapo Paulo hakuhubiri Injili pale Kolosai alihesabu kwamba mateso yake yalikuwa kwa ajili ya Kanisa zima ambalo Kanisa la Kolosai lilikuwa ndani yake. Alifurahi, si kwa mateso yenyewe bali kwa sababu yalikuwa kwa ajili yao. Katika Agano Jipya mateso na furaha vimefungamana (Mt.5:10-12; 1 Pet.4:13; Rum.5:3).

Aliposikia habari ya wengine wa pale kufundisha yaliyo kinyume cha kweli ya Injili hakuweza kusimama kando. Aliona amewajibika kuwasaidia waamini wa kweli na kuwaandikia barua hiyo na kwa njia yake kuwapa mafundisho ya kina sana juu ya Kristo ambayo yatawasaidia kupambana na mafundisho ya uongo.

Paulo aliyafurahia mateso yake na alisema “nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo kwa ajili ya Mwili wake, yaani Kanisa lake". Maneno hayo yana maana gani? Kamwe tusiwaze kwamba ulikuwepo upungufu wowote katika Mateso ya Kristo kuhusu Kifo chake cha Ukombozi, maana twaamini kabisa kwamba pale Msalabani alitoa dhabihu iliyo kamili, timilifu na ya kutosha kwa dhambi za ulimwengu wote. Kwa hiyo, ni mateso gani ambayo Paulo aliyasema? Liko wazo la Kristo kuwa bado anateswa katika mateso ya watu wake. Paulo alipoteswa Kristo naye aliteswa kwa sababu Paulo na Kristo kwa njia isiyoelezeka wameungana. Mateso hayo ni kwa ajili ya Kanisa, ambalo ni Mwili wake Kristo. Paulo alipokwenda Dameski, akakutana na Yesu njiani, Yesu alimwuliza “Sauli, Sauli, mbona waniudhi"?, Paulo aliteswa katika mwili wake na Kristo ndani ya Paulo aliteswa, kusudi Kanisa lake lijengwe. Kristo alipoteswa katika mwili ilikuwa kwa ajili ya ukombozi. Katika mpango wa Mungu mateso ya Paulo yalikuwa njia ya kuwakamilisha wateule wake, kwa sababu Mungu amekusudia iwe hivyo.

Maana nyingine yaweza kuwa kwamba yale yaliyopungua si katika mateso ya Kristo bali ya Paulo. Paulo akiwa na nia ya kuyashiriki mateso ya Kristo na kufanana naye katika Kufa Kwake alifahamu jambo hilo ni jambo linaloendelea (Flp.3:10) Mateso ni njia ambayo kwayo yeye mwenyewe hupata kuonja zaidi na zaidi mateso ya Kristo katika maisha yake. Mateso yanayopata Kanisa ni kwa ajili ya kulikamilisha, wala si njia ya kuongeza chochote kuhusu Kristo na ukombozi wake.

k.25 Iwapo Paulo hakuhubiri Injili pale Kolosai, hata hivyo alihusika na Kanisa la pale kwa sababu aliwekwa na Mungu kuwa Mhudumu, na amekuwa hivyo kwa faida yao. Kuhubiri kwake ni kama njia ambayo kwayo Mungu alitimiza makusudi yake yaliyodhihirishwa katika Neno lake, na faida yao ilikuwa kuelezwa vizuri yote yaliyomo katika Injili.

k.26-29 Siri ya Kristo
Tangu zamani ujumbe wa Injili ulifichwa, na vizazi vyote vilivyotangulia hawakuifahamu. Ila sasa siri hii imefunuliwa “kwa watakatifu wake” kwa hiyo si wote ambao wataigundua ila wale tu walioweza kuitambua vizuri. Ila tusiwaze kwamba wengine wamenyimwa kwa kusudi. Yesu alitaja habari ya siri hii katika Mifano (Mt.13:11 Lk.8:10). Katika Dan. 2:19,28,29 twasoma juu ya siri fulani ambayo ilifichwa katika mashauri ya Mungu na kufunuliwa kwa watumishi wake. Siri ambayo Paulo alikuwa akisema ni siri gani? ni kuhusu WaMataifa kuwa warithi wa ahadi ya Kristo kukaa ndani yao. Wayahudi waliamini kwamba Masihi atakaa kati yao ila walishindwa kuamini kwamba Masihi wao atakaa kati

ya WaMataifa, neno hilo lilikuwa geni kabisa kwao. Lakini ndivyo ilivyo. Maana katika Injili twasoma juu ya kupambazuka kwa siku mpya ya mwanga mkuu itakayowamulikia WaMataifa (Mt.4:15-16; Lk.2:32).

Jambo hilo limeelezwa na maneno “jinsi ulivyo utajiri wa utukufu wa siri hii” Mungu hutaka watu wake wajue na kulistaajabia neno hilo. Ni neno la “utukufu” na ni ufunuo wa jambo ambalo Mungu alikusudia tangu milele na kulifuatia katika historia yote mpaka lilipotimia katika Kuja kwa Kristo. Katika mpango wa Mungu WaMataifa wameingizwa na kushirikishwa Habari Njema ya Kristo na kazi yake sawa kabisa na Wayahudi watu wake wa zamani. WaMataifa wamekaribishwa nyumbani mwake na kuketi pamoja na mababa kama Ibrahimu n.k. Paulo aliongeza neno “utajiri” kuhusu utukufu huo wa siri hii. Ni kama Utukufu wa Mungu umezidi, tabia yake ya kuokoa imewekwa wazi kabisa. Neno “utajiri” linaelekeza mawazo yetu kuona thamani kubwa ya kumjua Kristo maishani mwetu, Yeye ni “hazina kuu” Yeye ni “lulu nzuri” ambayo kwa ajili yake ni vema kuuza vitu vingine vyote ili tuipate (Mt.13:44;46). Kristo ndani yetu ni tumaini la utukufu, katika Kristo tunayo ahadi ya uzima wa milele na kushirikishwa baraka zote za Mungu kwa utimilifu baadaye. Tukiwa na Mwana tunao huo uzima tayari (1 Yoh.5:12).

k.28 Hapo Paulo alisema “sisi tunamhubiri” akiwaingiza watu kama Epafra, Tikiko waliotumika Kanisa la Kolosai. Alibagua hao wenye ujumbe wa kweli na wale wenye ujumbe wa uongo waliojaribu kuingiza Injili iliyokuwa tofauti na ile ya kweli. Paulo aliwaza huduma yake na ya wenzake kuwa na mambo matatu. Kumhubiri Kristo, kuwaonya watu, na kuwafundisha, tena si kwa jumla tu, bali kwa mmoja mmoja. Walimhubiri Kristo bila kurahisisha madai yake, bila kuleta mambo mepesi mepesi tu, na bila kujipendekeza kwa watu. Waliwaonya watu juu ya dhambi zao ili waletwe kwenye toba la kweli. Pia, walifundisha watu mafundisho ya kina ili wapate kuelewa yaliyomo katika Injili. Shabaha yao ilikuwa kumleta kila mtu mtimilifu katika Kristo, hawakuridhika na matokeo ya juujuu. Walitafuta kumhudumia kila mtu, na bila shaka ilichukua muda kufanya hayo yote. Yawezekana wale waliofundisha kinyume cha Injili walijikusanyia kundi na kuwaza kwamba hao wa kundi lao ndio wa pekee walio na ujuzi wa kipekee.

k.29 Katika kufanya huduma hiyo waligharimiwa sana, waliishi kwa taabu ya kukosa nafasi za kula, kupumzika, kushirikiana na jamaa na rafiki. Paulo alitaka Wakristo wa Kolosai wafahamu kwamba yeye alikuwa akijitahidi sana na kujitaabisha kwa ajili ya huduma aliyopewa na Mungu. Bila shaka ushuhuda huo uliwasaidia kutia maanani mambo aliyowaandikia. Ila iliyopo ni kwamba iwapo alijitoa kufanya kazi hasa alifanya kwa kuwezeshwa na Mungu, Mungu alimtia nguvu ndani, hakutegemea uwezo na nguvu zake mwenyewe. Kweli Mungu alimwendesha na kumwezesha.

2:1-3 Paulo alitaka Wakristo wa Kolosai na Laodikia (4:15,16) wafahamu kwamba iwapo yeye hakupanda makanisa yao, hata hivyo, alikuwa na mzigo juu yao na juu ya maendeleo yao. Daima aliwaombea, alitaka kujua habari zao, na zaidi alitaka kuwasaidia, hasa aliposikia kwamba wako wengine walioleta mafundisho yaliyokuwa kinyume cha ukweli wa Injili k.2-3: Hasa alitaka mioyo yao itiwe nguvu, wawe imara, kwa sababu ilikuwa rahisi wapoe kwa kubumbuazwa na hayo mafundisho waliyosikia. Tena walihitaji kushikana katika upendo wasikubali kuingiliwa na hao wengine, dawa ni kuzidi kushirikiana na kutafuta kujua zaidi na zaidi habari za Kristo ili ufahamu wao wa kiroho ukue mpaka wawe na uhakika juu ya Kristo na utajiri wake, ambaye ndani yake imesitirika hekima na maarifa ya kiroho. Kusema imesitirika siyo kusema hekima na maarifa hayo ni mbali hata hawawezi kuyapata, la, bali ni kama yamefanana na vito ya thamani ndani ya mashimo ya madini, mashimo ni wazi ila vito vya ndani vyapatikana kwa kuchimba kwa bidii. Mafundisho ya hao wengine hayakujengwa katika Kristo. Hazina ya kweli ni Kristo. Yeye ndiye “ile siri” (2:2) na Paulo amekwisha kuonyesha ukuu na utangulizi wake katika 1:15-20. Hawana haja ya kutafuta “hekima” au ujuzi mwingine nje ya Kristo wala hamna faida katika kuufuatia.

2:4-23 Mafundisho ya uongo na Kweli ya Kikristo

2:4-5 Hapo Paulo aliwaonya waamini wajihadhari na wale waliotaka kuwadanganya hali wakitumia maneno laini ili wawashawishi kujali mafundisho yao. Inaonekana walikuwa wabingwa katika matumizi ya maneno. Kweli Paulo alikuwa mbali nao kimwili, hata hivyo, alijisikia kuwa yupo pamoja nao, kwa roho, bila shaka kwa sababu alikuwa akiwaombea daima na kumshukuru Mungu kwa ajili yao. Kwa sababu ni Wakristo yeye na wao wamo pamoja katika Kristo. Aliandika kama anawaona.

Mpaka hapa walikuwa wameshikana vizuri katika pendo, bado hawajakubali kuvurugwa na hao wengine, na Paulo aliifurahia hali yao njema, na imani yao thabiti, imani iliyowekwa katika Kristo. Waliishi kwa utaratibu, yaani walimfuata Kristo kwa pamoja, kama safu ya maaskari waendao vitani bega kwa bega.

k.6-7 Kumpokea Kristo kulikuwa chanzo tu, sasa walipaswa kuendelea “katika Kristo". Walikuwa wameipokea Injili ya kweli ambayo kiini chake ni Kristo Mwenyewe. Walikuwa wameyapokea mafundisho, pamoja na kumpokea Kristo Yesu Bwana – Kristo, Mwana wa Mungu; Yesu, Mwokozi, na Bwana, mkuu wa maisha yao ambaye iliwapasa kumpa utiifu wao wote. Sasa iliyotakiwa ni kuendelea katika imani hiyo siku hadi siku. Paulo alitumia mifano miwili, mmoja wa mmea, na mmoja wa jengo. Mmea huwa imara na kukua kwa sababu mizizi yake imewekwa ardhini. Wao nao walikuwa na mizizi yao katika Kristo, ilitokea hivyo wakati walipompokea na kuunganika na Kristo Aliye asili ya uzima wao. Vilevile kama jengo wameshikamana katika Kristo. Hivyo wameimarika kwa sababu mizizi yao imo ardhini na kama jengo kila siku wanaishi katika Kristo. Na hayo yote yametokana na mafundisho

waliyofundishwa na wale waliowahubiri Injili. Hivyo wajibu wao ni kumshukuru Mungu kwa ajili ya hayo yote, kusudi wasijione na kukosa unyenyekevu.

2:8-15 Katika sehemu hiyo Paulo amedokeza yaliyomo katika hayo mafundisho mengine lakini hakuyafafanua kabisa. Alitumia neno “angalieni” kuwaonya waamini juu ya “elimu ya bure na madanganyo matupu". Lazima wawe macho kabisa kwa sababu hao watu walitaka kuwateka mateka.

k.8 Yawezekana ni mtu mmoja aliyeongoza mafundisho hayo. (k:4) Iwapo mafundisho yalionekana kuwa “elimu” hata hivyo ilikuwa bure, hamna kitu ndani yake, hamna kweli, ilikuwa tupu. Haikuwa na nguvu ya kubadili maisha ya mtu, tofauti na Injili iliyo “nguvu ya Mungu” (1 Kor.1:18). Tena, ilikuwa madanganyo matupu, ilionekana na kudai kuwa na kitu, lakini, kumbe ilikuwa “tupu” kama hewa ndani ya kipuluzio. Haikuleta tumaini la uzima wa milele, wala baraka ya msamaha wa dhambi, wala kuleta mtu kwenye uhusiano mwema na Mungu. Ilikuza ujuzi wa kibinadamu, kinyume cha Injili iliyokuwa “ufunuo” wa Mungu.

"mafundisho ya awali ya ulimwengu” maneno hayo yana maana gani? Si wazi Paulo alikuwa akisemea nini. Huenda ni kuhusu ulimwengu wa roho, mamlaka na enzi zake na wakuu wa giza na majeshi ya pepo wabaya (1:16; 2:10; Efe.6:12). Wazo hilo limetokea kwa sababu Paulo alifanya ulinganifu na Kristo “wala si kwa jinsi ya Kristo” kwa hiyo inaonekana ni zaidi ya mafunzo ya kwanza kuhusu uumbaji na vitu vilivyoumbwa. Paulo alifundisha kwamba Kristo alikuwa na utukufu na nguvu juu ya roho mbaya n.k.(Gal.4:8-9) hivyo Wakristo hawakuwa na haja ya kuogopa wala kuwa mateka ya kitu kingine chochote, maana wao ni mali ya Kristo aliyeshinda Msalabani (2:15).

Wengine wamedhani maneno hayo yanahusu elimu ya nyota, yaani unajimu, maana katika siku zile wengi waliamini kwamba nyota na mwezi zinatawala matukio katika maisha yao.

k.9 Hapo Paulo amesema makuu kumhusu Kristo. “Katika Yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya kimwili". “Katika Yeye” mambo yote humzunguka na kumtegemea Kristo, Yeye ni kiini cha yote. Maneno ya ajabu yafuata “unakaa utimilifu wote wa Mungu” yaani Kristo amejaa Mungu, ni Mungu kamili, ni Mungu Mwana, hakupungukiwa katika Uungu wake hata kwa nukta moja, ni zaidi ya kusema Kristo amejaa tabia za Mungu, Uungu mwenyewe unakaa katika Kristo.

Ukweli huo unaandamana na Kufanyika Kwake mwili. Katika Yesu twamwona Mungu hasa (Yn.1:1,14) Kwa njia ya Kristo Mungu amepata kujulikana na utimilifu huo unaendelea kukaa hali Yesu amepaa kwenye utukufu wa juu.

k.10 Kwa kuwa utimilifu wote wa Mungu unakaa katika Kristo, hasa matokeo ni makubwa kwa watu wake. Wao wametimilika katika Kristo, nao wamekuwa washiriki wa tabia ya Uungu (2 Pet.1:4 Yn.1:16). Hawana haja ya malaika au enzi fulani kuwa kati yao na Mungu. Kutokana na Anguko (Mwa.3) dhambi iliingia na wanadamu wenye dhambi husikia kupungukiwa (Rum.3:23) wanahitaji kitu cha kuliziba lile pengo lililotokea kwa sababu ya uasi wao. Ni Kristo peke yake awezaye kuliziba pengo hilo na kuujaza upungufu huo na kufanya maisha yetu kuwa na maana kwa kutuelekeza kwenye mapenzi ya Mungu.

k.11 Kwa nini Paulo aliingiza neno la tohara. Inaonekana wale walioleta elimu hiyo nyingine walisema kwamba watu wakitaka kuingia katika shirika lao ni lazima watahiriwe. Twajua neno la kutahiriwa kwa Wakristo wa KiMataifa lilizuka mapema katika Kanisa; makanisa ya Galatia yalisumbuliwa sana na neno hilo, na shauri lilikatwa katika Baraza Kuu la kwanza la Kanisa lililokutana kwa shabaha ya kulijadili swala hilo (Mdo.15:1ku) Walikata shauri kwamba ubatizo watosha.

Paulo alitaja tohara nyingine “tohara ya Kristo” si ile ya kimwili, bali mateso yake Msalabani alipovua mwili wake wa nyama. Hata katika Agano la Kale mkazo ulikuwa juu ya moyo wa ndani (Yer.4:4; 9:25. Tazama Rumi 2:23-29).

k.12 Kwa njia ya ubatizo waamini walizikwa pamoja na Kristo ishara ya kuachana na maisha yao ya nyuma na kufufuliwa pamoja naye kwa maisha mapya wakiweka imani yao katika Mungu aliyemfufua Yesu kutoka kwa wafu, ambaye kwa nguvu zilezile atawafufua ili waishi maisha mapya. Ubatizo hauna maana nje ya kushirikiana na Kristo. (1 Pet.3:21). Hakuna tendo lililoonyesha nguvu ya Mungu kuliko tendo kuu la kumfufua Mwana wake kutoka wafu. Na hao waamini hawakuwa na haja ya kutafuta nyongezo lolote.

k.13-14 “na ninyi” kabla ya hayo hao Wakristo wa Kolosai walikuwa “wafu” kwa sababu ya dhambi zao, walikuwa wenye dhambi nao walitenda dhambi. Pia wengi wao walikuwa WaMataifa, watu wasiotahiriwa, watu walio mbali na Mungu (Efe.2:1ku 11-12) watu wasio na tumaini lolote.

Lakini badiliko kubwa limetokea, kwa njia ya Injili ya Kristo wamehuishwa katika Kristo, wamesamehewa makosa yao na kuletwa karibu na Mungu katika ushirikiano mzuri naye. Kitu kilichowatenga, yaani dhambi, ilikuwa imeondolewa. Kristo katika Kufa Kwake alilipa deni lao la dhambi na kufuta “hati iliyoshtaki” akifa mahali pao na badala yao na kuchukua hukumu iliyokuwa haki yao. Iliitwa “hati” kwa sababu kila kosa na kila dhambi ni uvunjaji wa sheria za Mungu. Mungu alikuwa ndani ya Kristo akiupatanisha ulimwengu na Nafsi yake (2 Kor 5:19) na kuifuta ile hati na kuiondoa ili kisiwepo kizuizi chochote cha kumzuia Mungu na wanadamu wasishirikiane kwa njia ya Kristo. Sheria haina uwezo wowote kuwahukumu. Kwa hiyo wamewekwa huru mbali

na sheria na desturi za kidini. Msalaba ndio msingi wa msamaha wa Mungu kwa dhambi za watu.

k.15 Katika Kufa Kwake Kristo alizishinda enzi ya nguvu za giza. Mungu alionyesha wazi kwamba ameshinda adui zake, enzi na mamlaka za giza, nazo ziliondolewa nguvu yao ya kumdhuru Kristo na watu wake. Siku ya tatu Kristo alifufuka na walinzi, jiwe, na muhuri havikuweza kumzuia asitoke kaburini. Siku zile Jemadari Mkuu aliyeshinda vitani aliporudi alifanya maadamano makubwa akiwatembeza mateka yake hadharani ili authibitishe ushindi wake wazi, na Paulo aliona Yesu amefanya vivyo hivyo katika Kufufuka Kwake.

2:16-23 Uhuru wa Kikristo
Inaonekana wale wa elimu nyingine walijaribu kuingiza sheria kuhusu vyakula na vinywaji na sikukuu na sabato n.k. Pamoja na hayo walifundisha watu kunyenyekea na kuabudu malaika. Iwapo ni vigumu kujua walifundisha nini hasa twaelekezwa kufikiri kwamba waliwaza malaika kuwa wajumbe kati ya Mungu na wanadamu na kama ni hivyo Kristo aliondolewa mahali pake kuwa Mjumbe pekee kati ya Mungu na wanadamu. (1Tim.2:5). Bila shaka ndiyo sababu ya Paulo kukaza sana Ukuu na Upekee wa Yesu na kumwadhimisha mno.

k.16 Kutokana na Ushindi wa Kristo waamini wa Kolosai wasikubali kutiwa utumwani na hao waliojaribu kuingiza sheria juu ya vyakula na vinywaji na sikuukuu n.k. Kristo amewaweka huru, wameokolewa kwa neema, hawana haja tena ya sheria. Hati ya sheria imegongomewa Msalabani na kufutwa. Mbona sasa wakubali sheria nyingine?

k.17 Vitu hivi vilifanana na vivuli tu, lakini hamna haja ya vivuli tena kwa sababu Kristo amekuja (Ebr.10:1ku).

k.18 Hapo Paulo alisema juu ya jambo lingine lililoletwa na hao watu kuhusu kuabudu malaika n.k. Iwapo unyenyekevu ni tabia moja ya Kikristo yenye sifa hao watu walifundisha watu kunyenyekea isivyo halali kwa kuabudu malaika. Katika kuabudu malaika walikuwa wamemkataa Bwana Yesu aliye pekee Mpatanishi kati yao na Mungu, ambaye walipaswa kumnyenyekea. Licha ya kuwa mnyenyekevu mtu aliyekubali kuabudu malaika alikuwa amejaa kiburi, kwa kuwa ujuzi wake ulikuwa wa kibinadamu tu, hali akitegemea akili zake na maoni yake tu, kinyume cha ufunuo wa Mungu katika Kristo. Tena alijitia katika hayo, maana yake alikazana kuendelea kufanya hivyo bila kujirekebisha.

k.19 Paulo alirudia kutumia mfano wa mwili (1:18). Kristo ni Kichwa cha Kanisa na ni dhahiri kwamba hao waliotaka kuwashawishi Wakristo walikuwa wameacha kumshika Kristo. Kama wangalimshika Kristo wangaliendelea kushikamana na Wakristo wengine katika Mwili mmoja, lakini walileta matengano, dalili ya kuwa hawakuwepo katika Mwili wa Kristo.

Dalili moja ya mwili kuwa chini ya Kichwa ni katika viungo na mishipa na misuli kufanya kazi kwa pamoja. Kanisa lapata uzima wake na nguvu zake kwa Kichwa chake Kristo hali Wakristo wameungana na Kristo. Katika Efeso 4:15- 16 neno kuu ni upendo (2:2). Mapenzi ya Mungu ni kwa Kanisa kukua. Kanisa si chama kilichoundwa na wanadamu wala haliendeshwi kwa mbinu za kibinadamu. Kanisa ni Mwili wa Kristo na Yeye ni kichwa chake na maisha ya Kanisa yamtegemea Yeye na mapenzi yake.

k.20 Ilikuwa upuzi kwa Wakristo kujitia chini ya sheria mbalimbali kwa sababu wameungana na Kristo ambaye katika Kufa kwake alizishinda enzi na mamlaka za giza na kuwatoa katika utawala wao. Wakikubali kuishi kwa sheria watakuwa wamekubali kuishi kwa kawaida na kanuni za dunia hii wala si kwa maisha mapya katika Kristo. Huzuni ni kwamba hao waalimu wa uongo hawakuishi maisha ya uhuru na ushindi.

k.21-22 Kuishi katika dunia kwa upande wa dini ni kuishi kwa sheria za “msishike, msionje, msiguse". Inaonekana wale wengine walileta sheria kali hata kugusa kulikatazwa. Twajua Wayahudi walipiga marufuku vyakula kadha. Paulo alisema kwamba hayo hayakuwa na shabaha yoyote, kwa sababu vitu vyenyewe kama chakula na kinywaji ni vya muda tu, ni vitu ambavyo vyatoweka wakati wa kuvitumia; havina faida idumuyo wala kwa uzima wa milele tofauti sana na waamini ambao wataishi milele. Tena asili ya maagizo na mafundisho hayo ilikuwa wanadamu si Mungu. Wanadamu walijichukulia mamlaka hii ambayo ilikuwa ya Mungu.

k.23 Katika kifungu hicho Paulo alijumlisha mawazo yake. Kwa nje mafundisho hayo yalionekana kuwa na hekima, kwa kuwa watu walinyenyekea kwa ibada na kwa kujinyima kwa ukali n.k. Shabaha yao ilionekana kuwa njema, hata hivyo Paulo alisema kwamba hayo yote yalikuwa bure maana hayakuwagusa kwa ndani wala kuziponya tamaa zao za mwili. Yalifanya watu kuwa na kiburi na kujiona na unyenyekevu wao haukuwa wa kweli, hawakuwa tayari kujinyenyekeza kwa Mungu na kuwa watiifu kwa Yesu Kristo. Asili ya mambo yao si katika mapenzi ya Mungu wala hayakupatana na Ufunuo wake katika Kristo.

3:1 - 4:1 Taratibu Mpya ya Maisha

Ilikuwa desturi ya Paulo kuweka msingi wa theologia ndipo kujenga juu yake mafundisho ya maadili. Katika sura zilizotangulia Paulo ameeleza Wakristo kuwa “watu walio katika Kristo” “watu waliokuwa wafu kwa dhambi” “watu waliofufuka kwa maisha mapya". Kuanzia sura ya tatu ameeleza maisha yaliyo wajibu wao kwa upande wa maadili na utendaji.

3: 1-4 Shabaha mpya kwa Watu Wapya: Katika 2:20-23 Paulo alisema “basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo..” ndipo alianza sura ya tatu na maneno “basi ikiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo..” Ni ukumbusho wa ubatizo ambao ni

mlango wa kuingia Kanisa na kuishi kama Mkristo, na ubatizo ni tendo la nje la kuonyesha kwamba huyo aliyebatizwa amekufa pamoja na Kristo kwa maisha ya nyuma, mfano wa Kristo kuifia dhambi, na ya kuwa amefufuliwa pamoja na Kristo kwa maisha mapya katika Yeye.

Hivyo waamini wa kweli wamehuishwa ili waishi tofauti na wengine, ni kama wanapumua hewa nyingine, “ya juu” hali wakiishi kwa shabaha mpya na kupima mambo tofauti na hapo nyuma. Mambo ya juu, yaani ya Mungu, ya kiroho, yataongoza na kutawala maisha ya Mkristo akifuata kielelezo cha Bwana Yesu ambaye sasa yuko mkono wa kuume wa Mungu, mahali patakatifu, penye uwezo, pa maombi. Kwa hiyo “kutafuta yaliyo juu, Kristo aliko” ni kutafuta kuwa safi katika maisha ya kila siku, pia kuwa na nguvu ya kuyashinda majaribu, na kuzidi kuomba kujaliwa msaada wa Mungu.

k.2 Mkristo awe na nia mpya, awe amekaza mawazo yake kwa Kristo na mambo ya kiroho, badala ya kuwaza mambo ya hapa duniani, mambo ambayo yanapita. Mambo ya juu ni kweli na ya milele, yana maana kubwa itakayodumu. Tuzingatie maneno hayo mawili “yatafuteni” (k.1) na “yafikirini” (k.2).

k.3-4 Sababu ya kufanya hivyo ni kwamba walikufa. Lini? Kristo alipokufa Msalabani walihesabiwa kuwa wamekufa pamoja naye. Sasa maisha yao yamefichwa katika Kristo na katika Mungu, hayaonekani wazi. Wamezaliwa upya kwa Roho wa Mungu, wamekuwa viumbe vipya, na ule uadui uliokuwa kati yao na Mungu umeondolewa, na kwa sababu hiyo wamwishia Mungu. Wamekuwa kama watu waliohama, hawapo ulimwenguni, ni wafu, kwa sababu iwapo miili yao imebaki hapa, mawazo yao na nia zao na maisha yao yamefichwa ndani ya Kristo. Ndipo Kristo atakaporudi katika utukufu mwingi, ataonekana wazi, ndipo wao walio watu wake watashiriki “Kufunuliwa Kwake". Kwa hiyo Paulo ametaja hatua tatu “kufa pamoja na Kristo, kufufuliwa pamoja na Kristo, na kufunuliwa pamoja na Kristo” Mafundisho hayo yanafanana na mafundisho ya Bwana Yesu katika Mathayo 10. Mitume walishirikishwa uwezo na mamlaka yake k.5 watashiriki mateso yake k.16: 24-25; 32-33; 40-42. Upo umoja wa ajabu kati ya Kristo na watu wake.

Lazima Wakristo wa Kolosai wafahamu sana kwamba maisha yao ya zamani hayana kazi tena, yamekwisha, yamekufa, na ni katika kuwaza hivyo watashinda, kwa sababu kwa kiroho ndivyo ilivyo hasa. Kwa hiyo maisha yao yote yatawaliwe na Mungu na mapenzi yake. Kristo ni uhai wao, ni zaidi ya kusema wapata Kwake uhai wao, kweli yenyewe ni Yeye Ndiye uhai wao, Yeye ndiye anaishi ndani yao.

3:5-11 Kufisha utu wa kali
Ina maana gani “kufisha” kwa sababu Paulo amekwisha kusema kwamba walikufa pamoja na Kristo? Mkristo ameitwa “kufisha” yaani kufanya vita na

tamaa zake mbaya. Alipokufa pamoja na Kristo aliunga mkono na Mungu kwamba dhambi haina haki ya kuwemo maishani mwake, hatakubali dhambi imtawale tena. Kwa hiyo budi afanye juhudi katika maisha ya kila siku kuishi kwa ukweli huo kwamba dhambi imepigwa marufuku, maana Mkristo bado angali anaishi katika mwili na katika ulimwengu huu. Kwa vyovyote atashambuliwa na majaribu mbalimbali na lazima aseme “la” mwili unapomdai kufanya kinyume cha imani yake, afishe matakwa yake. Ila ni vema kukumbuka kwamba hatafanya vita hiyo katika nguvu zake, kwa kujitegemea tu, ila atajaliwa nguvu za Kristo na kumtegemea Yeye. Viungo vyetu vyaweza kuwa vyombo vya kutenda mema au kutenda mabaya (Rum. 6:12-13) Ndiyo sababu Paulo alisema “vifisheni viungo vyenu” lugha hiyo ikionyesha kwamba mtu apaswa kujitawala kwa ukali kama Yesu alivyofundisha (Mt.18:8ku).

Ndipo Paulo alitaja dhambi mbalimbali zinazofanywa na viungo vyetu vinapopewa nafasi ya kuinuka na kutenda mabaya. Katika orodha hiyo zipo dhambi za kutenda pamoja na dhambi katika mawazo na tamaa zetu zilizo asili ya kutenda kwetu. Wengine wasingalihesabu “kutamani” yaani choyo kuwa mbaya.

Katika Agano Jipya ziko orodha za matendo mabaya na matendo mema na zingine zinafanana kama zile za Wakolosai, Waefeso, na 1 Petro. Yawezekana Kanisa lilikuwa na mapokeo ya mambo hayo yaliyotumika kufundisha Wakristo wakati wa ubatizo wao.

k.6 Ili watu wautambue uzito wa dhambi hizo Paulo aliingiza onyo juu ya ghadhabu ya Mungu. “huja” ni kama hukumu inayotokea wakati huo (Rum.1:18-32 hasa k.24, 26, 28: 1 Kor.5:10-11; 6:9- 10; 1 The.4:3-6). Mungu hujiingiza na kwa uamuzi wake akata shauri la kuwaacha watu waendelee kujiharibu na kujichafua ili iwe dhahiri kwamba wamestahili hukumu itakayowapata baadaye.

k.7 Paulo aliwakumbusha wasomaji wake ya kuwa hata wao wenyewe waliishi “katika dhambi” ila sasa wamehuishwa na Mungu na kuishi maisha mapya.

k.8 Paulo aliendelea kuwafundisha kuacha dhambi zingine akitumia mfano wa kuvua nguo. Wavue nini? hasira, ghadhabu, uovu, matukano, matusi, uongo. Katika hizo ziko dhambi za kuhusu ulimu, kiungo kile kidogo chenye nguvu. (Yak. 3:1ku).

k.9 Paulo alirudia kuonyesha tena sababu ya kuacha mambo hayo. Ni kwa sababu “wamevua utu wa kale” ni kama wametupa nguo chafu za zamani na kuvaa “utu mpya". Ni sawa na “kufa pamoja na Kristo". Hawawi tena “katika Adamu” wamehamishwa, wamo “katika Kristo". Mkristo hawezi kuwa kama alivyokuwa.

k.10 Kinyume cha “kuvua” wapaswa “kuvaa” utu mpya, na huo utu mpya daima hufanywa upya kwa uwezo wa Mungu ili Mkristo azidi kufahamu vizuri na kuishi maisha anayodaiwa na Mungu. Mkristo hurudishiwa uwezo wa kutambua haki kama ilivyokuwa kabla ya Anguko (Mwa.3) kwa sababu katika kuwaumba wanadamu katika sura na mfano wake Mungu alitia ndani yake kitu cha kupimia na kuongoza maisha yake, Yesu alisema “mwe mkamilifu kama Yeye alivyo Mkamilifu” (Mt.5:48).Habari Njema ni kwamba Mungu, kwa njia ya Kristo anafanya kazi ya kuurudisha ule mfano wake ulioharibika wakati wa Anguko. Ndani ya Kristo uumbaji mpya unatokea. Si jambo la kuvua na kuvaa tu, hasa ni Mungu anayehuisha watu ili wavue na kuvaa, wao huwa viumbe vipya katika Kristo (2 Kor.5:17).

k.11 Zile dhambi zilizotajwa katika k.8-9 ni zile zinazosababisha utengano na mafarakano katika jamii. Paulo alifundisha kwamba katika “uumbaji mpya” yaani katika Kristo watu wake hawataishi kwa kanuni na kawaida ya wenzao. Hao hujali zile tofauti kubwa katika jamii ya watu, ya utaifa, ya mila, ya ustaarabu, ya elimu, ya hali n.k. Lakini katika Kristo tofauti hizo hazina maana yoyote. Haidhuru mtu ni wa taifa au kabila gani, haidhuru anayo elimu au siyo, haidhuru ana cheo au siyo, katika Kristo kila mtu ni sawa na wenzake kwa sababu wote ni wenye dhambi, na wote huhitaji ule upatanisho uliofanyika Msalabani. Bila shaka Paulo alikuwa akiwalenga Wakolosai waliovutwa na mambo ya Kiyahudi, pamoja na wale waliovutwa na mambo ya Kiyunani. Yawezekana alitaja “mtumwa na mwungwana” kwa sababu Onesimo alikuwa mtumwa mtoro wa pale na Filemoni alikuwa bwana wake.

Kusema “bali Kristo ni yote na katika yote” ni kuonyesha kwamba Yeye ni juu ya utaratibu wa watu, hata mtu hupata maana yake ya kweli kutokana na uhusiano wake na Yeye kuliko uhusiano wake na mtu mwingine. Kila mtu huwa tofauti na mwenzake, ni wa kipekee, na utofauti huo haufutwi au kumezwa anapokuwa katika Kristo, hata hivyo wote hupata umoja wao katika Yeye.

k.12-17 Kuvaa utu mpya
Paulo alikuwa ametaja habari za “utu mpya” (k.10) na katika sehemu hiyo aliendelea kwa kufafanua maana yake. Alianza kwa kuwaeleza Wakristo kuwa watu wapya wa Mungu, wateule, watakatifu, watu wa Agano Jipya wakikanyaga nyayo za Watu wa Mungu wa zamani, yaani Israeli. Ni wateule wa Mungu kwa sababu wamechaguliwa na Mungu ili wawe watakatifu wapendwao. Mungu amewachagua na kuwatenga kwa kusudi la wao kuishi maisha matakatifu, na kufanya mapenzi yake, wawe mali yake. Ni wapendwa wake, kwa sababu Mungu katika kuwateua ameweka pendo lake juu yao. Kwa hiyo Mungu huwadai tabia na hali za kiroho (1 Yoh.4:11).

Ndipo Paulo aliorodhesha hali na tabia njema walizodaiwa; rehema, utu wema, unyenyekevu, upole, uvumilivu, kusameheana na kuchukuliana. Hizo ni

kinyume cha dhambi zilizotajwa katika k.8-10; dhambi za utu wa kale. Katika zamani zile unyenyekevu na upole zilikuwa tabia zilizodharauliwa sana zikihesabiwa kuwa tabia za wanyonge.

Kuchukuliana na kusameheana ni hali ambazo Paulo alitaja mara nyingi katika Nyaraka zake. Hizo zilitakiwa sana ili watu waishi katika amani. Utayari wa kuchukuliana na watu ulikuwa lazima, ni kama mafuta katika mashini ukilainisha uhusiano kati ya watu. Vilevile kusameheana badala ya kulaumu kulikuwa dawa nzuri ya kujenga ushirikiano mzuri, kwa kuwa mtu akidai haki tu uadui utatokea. Hasa hali hizo zawezekana kwa sababu ndivyo tutendewavyo na Mungu na Bwana Yesu. Kuna uhusiano mkubwa kati ya Mungu kutusamehe sisi na sisi kuwasamehe wengine kama isemavyo Sala ya Bwana. Tabia hizo ni kama nguo mpya za kuvaa.

k.14 Zaidi ya hayo yote Paulo alionyesha kwamba iko nguo nyingine ya kuvaa, pengine aliwaza vazi la nje au mshipi, na nguo hiyo ni upendo. Tabia itakayosaidia hasa ni upendo. Paulo alisema ni “kifungo cha ukamilifu". Upendo unafungamanisha tabia zile zote pamoja na kuleta ukamilifu. Ni lengo la hali ya juu kabisa kuishi katika uhusiano mkamilifu na ni lengo la kweli kwa sababu Kristo aliye mzima wetu ni mkamilifu na sisi tu Mwili wake (Mt.5:48).

k.15 Amani ya Kristo. Amani kama upendo ulikazwa sana na Bwana Yesu na kutajwa sana na Paulo. Ni kipawa cha Bwana Yesu kwa watu wake (Yn.14:27). Yesu anataka tuwe na amani mioyoni mwetu na kuwa na amani kati yetu. Amani hiyo ina kazi ya “kuamua” ni kama filimbi ya ndani. Neno lililotumika ni lile kwa “mwamuzi wa michezo". Kama jambo ni sawa amani itatulia ndani, kama jambo si sawa amani itaanza kuondoka moyoni, kama kulia kwa filimbi.

Tena twahitaji kuwa watu wa shukrani, tukitambua baraka za Mungu na rehema zake kwa udhaifu wetu. Pia tukiwa na moyo wa shukrani kwa Mungu tutajua kwamba kila kitu chema kimetoka Kwake, hivyo tutajifunza unyenyekevu na huo unyenyekevu utatusaidia kuishi vema na wengine, hatutakuwa na kiburi na majivuno, na chuki n.k. Pia tutakuwa wepesi wa kutambua wema wa wengine na kumshukuru Mungu kwa ajili yao.

k.16 Neno la Kristo, yaani Injili na mafundisho yanayopatana nayo. Paulo aliwaambia Wakolosai waruhusu Neno la Kristo kukaa kwa wingi katika mioyo yao, ili wapate hekima ya kufanya yampendezayo Mungu. Inaonekana mafunzo hayo yalikuwa kwa njia ya uimbaji katika ibada, wakishirikiana kwa pamoja. Nyimbo zao ziwe na mambo mawili; mafunzo ya kweli ya kuwajenga kiroho; na maonyo ya kuwaelekeza kwenye njia nzuri na kuwarekibisha. Tena hawaimbi kwa faidi yao tu, bali kwa Mungu na utukufu wake. Tena wataimba “kwa neema” kama watu walioletwa kwenye ushirikiano mwema na Mungu na

kwa zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni watajifunza zaidi habari ya neema hiyo, hivyo watazidi kujengana.

k.17 Paulo alifunga sehemu hiyo kwa kuonyesha wajibu wa kila Mkristo kufanya kila jambo, ama ni neno, ama ni tendo katika Jina la Bwana Yesu. Maana yake alete kila jambo chini ya uongozi wa Kristo ili kila jambo lipatane na tabia na mapenzi yake. Wajibu huo hupatana kabisa na msingi wa Waraka ambao ni Yesu kuwa Mkuu na wa kwanza katika Uumbaji na katika Kanisa. Hatuwezi kutenga eneo la dini na eneo la maisha ya kila siku. Kwa njia hii twakiri Yesu ni Bwana kwelikweli. Lakini iwapo tumetumia neno wajibu, siyo kusema ni wajibu wa kutulemea, la, hata kidogo, maana tutafanya wajibu huo katika hali ya kumshukuru Baba tukiwa watoto wake waliowekwa huru hali tukimtegemea atujalie neema ya kutusaidia.

3:18-4:1 Mashauri kwa nyumba za Kikristo
Swala kubwa lilikuwa “wake za Kikristo waishije na mume zao"? kwa sababu katika zamani zile hawakuhesabiwa wanazo haki sawa na mume zao. Paulo alisema kwamba walipaswa utii, ila ni utii wa namna ile “ipendezavyo katika Bwana” hivyo uhusiano wao katika ndoa uwe unaongozwa na uhusiano wao katika Kristo. Iliwapasa waume wapende wake zao. Kwa hiyo, kwa mke ni utii na kwa mume ni upendo, na bila shaka utii katika mazingara ya pendo la mume na katika kumpenda Bwana ni utii usiowalemea wake. Shida fulani ikitokea kati yao waume wasiwe na uchungu kwa wake zao. Kwa hiyo Paulo hakuona kwamba mke ni chini ya mumewe, kila mmoja alidaiwa kuishi kufuatana na usawa wao katika Kristo.

k.20-21 Kuhusu watoto na wazazi wao Paulo alisema kwamba watoto walipaswa utii katika mambo yote. Tena uhusiano wao unaongozwa na uhusiano wao katika Bwana. Watoto watii wazazi wao kwa sababu ni watoto. Kwa upande wa wazazi Paulo alikuwa na neno kwa baba zao kwamba wasiwakandamize na kuwatazamia kufanya mambo yasiyo haki kuwadai, kwa sababu bado wangali ni watoto Ni juu ya wazazi kuwafahamu vizuri watoto wao, na uwezo wao, kusudi wasije wakawakatisha tamaa kwa kuwatazamia mambo kupita uwezo wao.

k.22-4:1 Walikuwapo watumwa wengi sana katika zamani zile. Paulo aliona njia ni kutafuta kuleta nafuu katika hali yao na kutibu uhusiano wao na mabwana wao. Wakati ule Kanisa hakuona vema kuamsha siasa ya kuufuta utumwa wala kupiga vita juu yake. Ilikuwa dhahiri kwamba Kanisa lisingaliweza kufaulu maana lenyewe lilikuwa changa bila uwezo wowote wa kukabili jambo kubwa la kiasi hicho.

Paulo aliwaambia watumwa kuwatii mabwana wao katika mambo yote. Alisema hivyo iwapo Utumwa haukuwa halali. Paulo hakukabili swala la uhalali wa Utumwa bali alikuwa na mzigo juu ya uhusiano kati ya mtumwa na bwana

wake. Watumwa walihesabiwa na kufanyiwa kama “vitu” na “mali” lakini Paulo alikaza ya kuwa walikuwa “watu wenye nafsi” na alizungumza nao kama watu walio na haki zao katika shirika za Kikristo na kama ni waamini wenye wajibu zao za Kikristo. Alisema “kwa mwili ni bwana zenu” na kwa sababu hiyo mabwana walikuwa na mamlaka juu ya watumwa wao.

Watumikaji? Wawe wanyofu wa moyo na kutumika katika hali ya kutoa utumishi wa kweli, wakifanya si kwa kujipendekeza wala kwa wakati wa kuonekana tu, wala kwa juujuu, hata wanapoachwa peke yao wafanye kazi vizuri, hata wakikandamizwa vibaya waendelee kufanya kazi vizuri, hali wakimcha Bwana na kuhesabu kwamba wanamtumikia Yeye kwa njia hiyo. Wanaye Bwana aliye juu yao na juu ya mabwana wao wa kimwili naye huwaona kila wakati na kila mahali, pia yeye hufahamu ugumu na dhiki wanazopata na Kwake watarithi uzima wa milele na baraka zake. Kwake wao ni watoto wa kurithi. Watawezaje kufanya kwa moyo huku hawapati mshahara? watasaidiwa kwa kukumbuka kwamba wanamfanyia Bwana Yesu, kwa sababu ndivyo ilivyo hasa, Paulo alisema wazi “mnamtumikia Bwana Kristo” Tena Paulo alionya kwamba kwa Mungu hamna upendeleo, adhulumuye atahukumiwa. Huenda maneno hayo yalilenga mabwana wakali. Bila shaka mashauri hayo yaliwasaidia kuelewa namna ya kuishi wakiwa watumwa walio Wakristo.

4:1 Hapo Paulo aliwageukia mabwana walio Wakristo akiwakumbusha kwamba wao wanaye Bwana mbinguni, hivyo wawafanyie watumwa wao kwa haki na adili. Iwapo ni mabwana, pia ni watumishi wa Bwana Yesu. Kwa hiyo watumwa na mabwana walidaiwa na Kristo kuishi kama ilivyo wajibu wao katika Kristo. Bila shaka mafundisho hayo yalipanda mbegu ambayo baadaye iliota katika utumwa kuondolewa katika jamii ya watu. Watumwa na mabwana wataishi hivyo kwa neema ya Kristo, wote wakihitaji msaada wa Bwana.

Yafikiriwa Paulo alisema hayo yote kwa sababu barua hii ililetwa na Tikiko aliyesafiri pamoja na Onesimo yule mtumwa mtoro. Paulo alikuwa akimrudisha kwa bwana wake Filemoni, Mkristo wa pale Kolosai.

4:2-6 Mashauri mbalimbali

Paulo alikaza umuhimu wa maombi, na jinsi ya kuomba kwa kukesha na kushukuru ili wasifanye mradi tu. Wakolosai wadumu na kukesha katika kuomba, kwa sababu ni rahisi kulegea na kuvutwa upande. Wakristo wakaze nia zao ila maombi yachukue nafasi ya kwanza katika maisha yao ya Kikristo. Pamoja na maombi wawe watu wa shukrani, kwa sababu shukrani huburudisha mioyo wanapokumbuka mema yote waliyoyatendewa na Mungu. Ndipo Paulo aliomba wamkumbuke yeye na wahudumu wengine waliokuwa pamoja naye katika kazi ya kuhubiri Injili ili wapate nafasi za kumtangaza Kristo, hasa yeye Paulo katika hali ya kufungwa kwake. Tena alitaka mahubiri yake yaeleweke vizuri, aseme wazi kusudi watu waufahamu ujumbe anaowaletea.

k.5-6 Hapo Paulo alisema juu ya hali zao mbele ya wasioamini ya kwamba wawe na hekima katika matumizi ya wakati na katika mazungumzo yao. “kukomboa wakati” ni kulinda sana wakati uliopo ili wapate faida kubwa kwa kushika nafasi zozote za kumshuhudia na kumtumikia Kristo.

Pia waseme maneno yenye maana, maneno safi, maneno yaletayo baraka. Maneno ya kutoka moyoni ambamo Kristo ameweka makao yake ndani. Wafikiri kwanza ili maneno yamfaa msikilizaji wake na mwenye maswali ajibiwe kwa kumjenga.

4:7-18 Salaam za kuagana

k.7-9 Waraka huu utapelekwa kwa mkono wa Tikiko. Yeye pia aliupeleka Waraka kwa Waefeso (Efe.6:21-22). Paulo alimthamini sana akimwita ndugu mpendwa, mtumishi mwaminifu, mjoli wangu katika Bwana (Mdo.20:4; 2 Tim.4:12; Tito 3:12). Tikiko atawapasha Wakolosai habari zake na za wale waliokuwa pamoja naye, ili wawe na habari kamili juu yao. Kwa kuwa Paulo alikuwa kifungoni walikuwa na wasiwasi juu ya yatakayompata ila ilionekana kwamba alitumaini kwamba atafunguliwa (Flm.22). Watafarajika kwa kufikiwa na Tikiko.

Onesimo atarudi Kolosai pamoja na Tikiko. Aliishi pale akiwa mtumwa wa Filemoni lakini alimtoroka na kufika Rumi. Hapa alikutana na Paulo na kukata shauri kumkumbali Kristo. Alikuwa amekaa na Paulo na kumtumikia, na Paulo alimwita ndugu mwaminifu mpendwa. Paulo alikuwa ameuhakikishia ukweli wa imani yake. Habari zake zimeandikwa kwa kirefu katika Waraka kwa Filemoni.

k.10-11 Ndipo Paulo aliwataja Wakristo watatu wa Kiyahudi waliokuwa pamoja naye na kupeleka salaam zao. Mmoja aliitwa Aristarko (Mdo.19:29; 20:4; 27:2) Paulo alisema “aliyefungwa pamoja nami". Je! alifungwa kimwili au ni lugha ya Paulo kueleza jinsi alivyofungwa naye kiroho katika utumishi wa Kristo. Hatujui. Epafra aliitwa hivyo (Flm.23).

Halafu Paulo alimtaja Marko, mjomba wake Barnaba. Paulo hakupendezwa na Marko zamani, alipomwacha yeye na Barnaba katika safari ya kwanza, akakataa kumchukua tena (Mdo.13:13; 15:36ku) lakini sasa walikuwa wametengeneza shida yao. Inaonekana Paulo ameisha kuwaandikia Wakolosai juu yake kwa sababu ilitazamiwa atafika kwao. Hatuna habari yoyote kumhusu Yesu aitwayo Yusto.

k.11 Paulo alisema ni hao watatu tu waliotenda kazi pamoja naye. Hakuwa na maana ya kwamba ni hao tu kwa sababu aliendelea na kutaja Wakristo wa KiMataifa. Alitaka kuwatofautisha hao watatu na wale Wakristo wa Kiyahudi ambao daima walimpinga kuhusu tohara kwa kudai ni lazima kwa waamini.

Alisema walikuwa “faraja kwangu” kwa maneno hayo twatambua Paulo alikuwa mwanadamu sawa na sisi, alisikia huzuni na upweke alipopatwa na vipingamizi mbalimbali, na alikiri kwamba alisaidiwa na kutiwa moyo na wale waliosimama pamoja naye.

k.12-14 Paulo alimsifu sana Epafra (1:7; Flm.23) Alikuwa mtu wa maombi akifanya bidii, yaani alijitoa kabisa kuwaombea hata kiasi cha kuugua, kama Yesu alivyougua Gethsemane. Alikuwa na mzigo sana juu ya maendeleo yao ya kiroho akitamani kwamba wakamilike na kuthibitika katika mapenzi ya Mungu. Asingaliweza kuomba neno bora kuliko hilo.

Kwa sababu alikuwa amepanda mbegu ya Neno la Mungu pale, alitamani sana iote na kuzaa sana. Pia hakuwa na mzigo juu ya Wakolosai tu, hata aliwaombea waamini wa Laodikia na Hierapoli, miji iliyokuwa karibu na Kolosai. Huenda ni yeye aliyepanda makanisa yao.

k.14 Luka pia alituma salaam zake. Paulo alimwita “tabibu mpendwa” ni hapo tu tumepata habari ya Luka kuwa tabibu. Dema alitajwa pamoja na Luka. Hatuna habari nyingine juu ya Dema ila ile ya kusema kwamba baadaye alimwacha Paulo kwa kupenda ulimwengu wa sasa (2 Tim.4:10)
k.15-18 Katika sehemu hiyo Paulo alituma salaam kwa Wakristo wa Laodikia na kwa kanisa lililokutanika katika nyumba ya Nimfa. Wakati ule Wakristo walikutanika katika nyumba zao. Majengo hayakujengwa mpaka muda mrefu baadaye. Paulo alitaja Waraka kwa Laodikia, ni upi? kwa kuwa hatunao Waraka huu katika Agano Jipya.

Kuna mawazo mawili kuhusu jambo hilo. La kwanza ni Waraka huo kuwa umepotea. La pili ni kwamba ni Waraka kwa Waefeso . Kwa nini ifikiriwe ni Waraka kwa Waefeso. Kwa sababu watu hufikiri kwamba Waraka kwa Waefeso haukuwa Waraka kwa palepale tu, bali ulikuwa Waraka wa kushirikishwa makanisa yote yaliyozunguka Efeso. Sababu moja ni kwamba neno Efeso (Efe.1:1) halipo katika nakala za zamani sana, kwa hiyo watu huwaza kwamba nafasi iliachwa kwa mahali kuingizwa. Pia hauna salaam za binafsi, tena Tikiko ametajwa kuwa mpelekaji wake (Efe.6:21)

Tusemaje? Kwa jinsi Paulo alivyosema inaonekana zilikuwapo Nyaraka mbili, mmoja kwa Wakolosai na mmoja kwa Laodikia na ya kwamba wazisome zote mbili.

k.17 Arkipo alitajwa katika Filemoni 1. Je! alikuwa na huduma gani? Pengine alikuwa ameshika nafasi ya Epafra wakati wa Epafra kuwa pamoja na Paulo. Paulo alimwagiza kwa uzito kutimiza huduma aliyopewa katika Bwana. Kama alikuwa Kolosai ilimpasa awe macho kwa sababu ya kuwapo kwa wale waliotaka kuingiza mafundisho yaliyo kinyume cha Injili. Inaonekana kazi yake

ilikuwa ya maana kwa sababu barua hiyo itasomwa hadharani mwa watu na jina lake litatajwa wazi.

k.18 Kisha Paulo alifunga na salaam zake ambazo aliziandika kwa mkono wake mwenyewe, dalili ya kuwa alikuwa ametumia mkalamani. Aliomba wamkumbuke na kumwombea kwa ajili ya kufungwa kwake, alihitaji neema na uvumilivu. Bila shaka ndani ya ombi lake alitaka waombe kuhusu tumaini lake la kufunguliwa na kufika kwao. Mwishowe alitumia maneno aliyoyazoea sana “neema na iwe pamoja nanyi".

M A S W A L I

1. *Je! ni kweli kwamba upo uhusiano mkubwa kati ya Maadili na Imani? Onyesha kwa kutoa mifano jinsi Imani ya mtu inavyomwongoza katika kutenda kwake.*

2. *Ni mambo gani hasa katika Imani ya Kikristo yanayomsukumu mwamini wake kuishi maisha mema?*

3. *Je! mtu aweza kuwa Mkristo peke yake na kuendelea kiroho bila kushirikiana na wengine? Au Ushirikiano wake na wengine una sehemu kubwa katika maendeleo yake ya kiroho? Toa mawazo yako.*

4. *Kol.1:15-23 Kwa maneno yako mwenyewe andika mambo makuu Paulo aliyoyasema kumhusu Kristo, Nafsi yake na Kazi yake.*

5. *Kol.2:15 Katika kifungu hicho Paulo amesema kwamba Kristo alishinda vitu mbalimbali. Weka vitu hivi katika maneno yako mwenyewe na kwa kuwaza vitu vinavyowatisha watu wanaoishi mahali pako.*

6. *Kol.3:1ku. Paulo alisema “mlikufa pamoja na Kristo na mlifufuka pamoja na Kristo”. Alikuwa na maana gani? Yaani walikufa na kufufuka lini na kwa namna gani? Eleza.*

7. *Ndipo, onyesha matokeo ya hayo kuwa nini katika maisha ya Mkristo, yaani ataishije? avue nini? avae nini?*

8. *Kol.3.11 “Hapo hapana Myunani wala Myahudi, kutahiriwa wala kutokutahiriwa, mgeni wala mshenzi, mtumwa wala mwungwana”. Andika kifungu hicho kwa kuyabadili maneno kama Myahudi na Myunani na yale mengine ukiwaza matengano au ubaguzi hata uadui uliopo mahali pako na katika nchi yako.*

9. *Je! Ni katika mambo gani Kanisa bado halijafaulu kuuondoa ubaguzi mbalimbali? Eleza.*